# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

Verbatim Report of

DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

MSAMBWENI CONSTITUENCY

HELD AT DIANI SECONDARY SCHOOL

ON

**14 OCTOBER 2002**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, MSAMBWENI CONSTITUENCY, HELD AT DIANI SECONDARY SCHOOL ON 14TH OCTOBER 2002**

**Present:**

1. Dr. Swazuri Mohammed - Commissioner

**Secretariat Staff in Attendance**

1. Noor Awadh - Assistant Programme Officer
2. Lydia Morah - Verbatim Recorder

The meeting started at 10.16 a.m.

**Mohammed Budzo:** ….(*vernacular*). Kwa hivyo tunaomba Maalim mmoja atuwekee dua.

**Speaker:** Amin Amin Amin Amin Amin.

**Mohammed Budzo:** Basi ndugu zangu tunawakaribisha na nafurahi vile mmealikwa na mkaitikia huu mwito. Kwa hiyo, hapa si mambo mapya zaidi ni hali ya kufuatilia yale mambo yetu tuliokuwa nayo kuhusiana na mambo ya Katiba. Nafikiri tulikuja hapa tukatoa maoni yetu na ma-Commissioner wetu walizunguka Kenya mzima, sisi watu wa Msambweni tukabahatika kuwa na vituo viwili moja ikiwa ni hapa hapa tulipo ambacho ni kituo cha Diani, na chengine kilikuwa huko Msambweni Jomo Kenyatta. Yale maoni yenu yalienda yakakusanywa mahali pamoja na yakawekwa katika kitabu ambacho ndivyo hivyo

magazeti mengine mlionayo ama mliopatiwa mkononi, wanayaita draft report. Kwa hivyo tunawaomba tuwe watulivu kidogo halafu bila shaka tutamkaribisha Commissioner wetu ambaye ni Dr. Swazuri, kijana wetu hapa hapa Kwale naye bila shaka atatupatia yale mengi na mengine ambayo pengine hatuyajui. Kwa hayo, karibu Daktari.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Salaam Aleykum?

**Audience:** Aleykum Salaam

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Mwalamkaze.

**Audience:** Salaam.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Haya, sisi tumekuja hapa kama alivyosema Bwana Councillor, kutimiza ahadi tuliyoiweka kwamba tutakusanya maoni yenu halafu tuandike reporti, halafu tuwaletee muje muisome, halafu tuizungumzie ndio hivi tumekuja. Kwa hivyo taratibu tutakayofuata ni kwamba nitawasomea maanake kuna wengine hawakuweza kusoma, wengine wameipata hivi sasa lakini tutawasomea kwa ufupi, summary au mkhatasari wa ile Katiba inasema nini, halafu nitawapatia nafasi watu wachangie. Kama kuna mahali hamwelewi, kama kuna mahali si hivyo mlivyotaka, kama pana pahali pamepungua, kama kuna pahali hatukuandika. Sasa leo ni nafasi yenu. Sio mwisho wa hapa, baada ya sisi kuondoka leo Coordinator Bwana Mwero atafanya vikao tena. Vikao ambavyo vitajadili kwa undani zaidi hii Katiba, halafu yale maoni yale pia bado tunayataka tuyaandike halafu ndio mswada ule ambao tutakua tumeuandika ya majadiliano haya ndio utaenda kwa kikao cha kitaifa.

Kikao cha kitaifa kitaanza wiki mbili zijazo, tarehe ishirini na nane, tunavyootazamia lakini itategemea mambo mengi ya wanasiasa. Kwa hivyo huo ndio utaratibu wetu na ndio sababu tumekuja hapa. Kwa hivyo, kwa sababu ya kwamba hii draft, huu mswada kidogo unataka kuangaliwa kwa makini. Mimi nitapitia wote kwa mwanzo nitaanza kuwaeleza yale mambo ambayo tumebadilisha mwanzo, yale mambo ambayo ni mapya. Mambo ambayo ni mapya katika Katiba hii, tunayoipendekeza…..(vernacular)

**Mohammed Budzo:** Naomba tuwe watulivu vitabu mtapatiwa, tuwe watulive ili Bwana Commissioner atueleze vizuri. Haya tuwe watulivu vitabu vikiletwa tutapatiwa, tuwe watulivu lakini.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Kwa hivyo kama kawaida, mwanzo tutaanza na yale mambo ambayo tunayakuta ni mapya. Hayapo katika Katiba ile ya sasa tunapendekeza yawemo, baada ya hapo tutaenda kifungu kwa kifungu kuwaeleza kwa ufupi tumefanya nini, tumeandika nini na pengini kwa nini tumefanya hivyo. Basi sasa uwanja na wenu, hii sio Katiba tayari mpaka nyinyi wenyewe mkubali.

Haya, jambo la kwanza wale wanaoweza kusoma Kiingereza watakuta kwamba hii Katiba imeandikwa kwa lugha nyepesi, sio lugha ya kisheria. Wananchi wengi walitaka Katiba iandikwe katika lugha ambayo kila mtu akisoma anaelewa, hiyo tumefanya. Jambo la pili, tumesema kwamba Katiba lazima itaandikwa kwa lugha ya Kiswahili, nafikiri mmeona hiyo repoti, imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Huo mswada wenyewe nafikiri huo unafanyiwa tafsiri utakuja pia kwa lugha ya Kiswahili, na ile ya mwisho tutakayoitoa kwa wananchi baada ya kupitishwa pia nayo iko katika Kiswahili. Hayo ni mambo ambayo ni mapya katika duru hii ya kuandika Katiba, na kulingana na upande wa lugha kataka Katiba yetu tunapendekeza kwamba sasa lugha ya taifa itakuwa ni Kiswahili. Hilo ni jambo jipya ambalo zamani lugha ni Kiingereza. Lugha rasmi ya Kikenya ni Kiingereza na Kiswahili lakini lugha ya taifa sasa officially ni Kiswahili.

Jambo jingine ni kwamba Katiba hii ya sasa mpya itakuwa na utangulizi, Preamble. Ile Katiba ya zamani ilikuwa haina utangulizi. Katika utangulizi ule tunasema kwamba tunaangalia masilahi ya wananchi, mambo ya haki za wananchi ndizo imetiliwa mkazo zaidi katika Katiba hii, kinyume na mstari miwili au mitatu iliyoko katika Katiba ya sasa au ile ya zamani. Jambo jipya jingine ni kwamba, kwa sababu hiyo Katiba imetengenezwa na wananchi. Tulizungumza na wananchi wakatoa maoni yao, halafu tukaandika Katiba; kinyume na ile nyingine ambayo iliandikwa na watu kidogo na wenyewe ambayo wamekuwa wakiangalia ni Wabunge. Sasa hii ni Katiba yenu, mambo yote tulioyaandika hapo yanahusiana na maoni ya wananchi sio chombo cha Serikali tena hii, sasa ni chombo cha wananchi wenyewe. Hiyo ni tofauti kubwa kabisa kwa sababu ukiangalia sana Katiba yote inalenga mwananchi. Katiba yote sasa inalenga uhuru na uwezo wa mwananchi katika kuendeleza Serikali yake. Zamani au Katiba hii ya sasa lazima kila kitu kitoke kwa Serikali, Serikali itafanya, Serikali imesema, Serikali namna hii, sasa ni wananchi ndio ambao wamepewa uwezo huu.

Halafu katika Katiba hii, kitu kipya tumesema kwamba ni lazima tuwe na usawa wa kila mtu mbele ya hii sheria. Hakuna mtu ambaye yuko above the law, hakuna mtu ambaye sheria haimpigi au haimfuati. Tukitunga sheria yetu kusema tusifanye kitu fulani basi ni watu wote kutoka Rais mpaka chini, mpaka mtoto mdogo ni watu wote, tumesema tuko sawa. Halafu jambo jipya tumesema katika Katiba hii, kila sehemu tunayoisoma inasema Wakenya hawatabaguana tena. Ubaguzi wa haina yoyote kama ni wa rangi, kama ni wa kikabila, kama ni wa kijinsia, akina mama na akina baba, kama ni wa umri, wazee na vijana ubaguzi huu hatuutaki. Kama ni wa eneo, watu wa sehemu hii na sehemu nyingine hatutaki ubaguzi huo, kama ni wa dini, yote hayo tumeondoa, watu wote wako sawa na kila mtu anaweza kufanya anavyotaka kulingana na sheria. Hilo ni jambo ambalo ni geni katika hii Katiba ya sasa.

Jambo jingine jipya ni kwamba tumeeleza jinsi ya, uraia, citizenship. Uraia sasa umekuwa na sheria zake za kupata uraia, upande mwingine zimepanuliwa ziwe zaidi lakini upande mwingine tumeweka vikwazo zaidi. Wale ambao walikuwa hawezi kuwa raia kwa sababu mama yao si Mkenya sasa inawezekana. Kuna wengine walikuwa zamani mpaka mamako na babako awe ni Mkenya, sasa mzazi mmoja akipatikana basi, sasa unakuwa raia. Hilo ni jambo ambalo ni jipya na pia tukasema kwamba kuna nafasi ya wale ambao wanataka kuwa na uraia mara mbili, dual citizenship. Wale wanaotaka kuwa raia mara mbili sasa tumewapatia nafasi hiyo lakini pia tumeweka vikwazo. Ukivunja sheria uraia wa Kenya automatically unakutoka.

Halafu tukasema kwamba, haki za kimsingi, human rights sasa zimeandikwa wazi kabisa katika Katiba na tumeandika ni nani ambaye atatekeleza haki za msingi, ni nani ambaye atakuwa na jukumu la kufanya ili wananchi wawe na haki za kimsingi. Zote zimeandikwa kutoka haki za chakula, za watoto, za mavazi, za elimu, za kila kitu tumeziandika na zamani zilikuwa haziko.

Halafu upande wa Bunge, jambo jipya pale tumesema pale tumesema kwamba Bunge letu litakuwa na chamber mbili. Tutakuwa na Bunge la kawaida, wale Wabunge ambao tutawachagua; halafu tutakuwa na Upper House kama vile zamani wakati wa Lancaster. Tutakuwa na Upper House, hiyo ni tofauti ambayo tumeiweka. Halafu upande wa Bunge tena tumesema kwamba Bunge sasa limepewa kazi nyingi, nafasi zake za kazi zimepanuliwa, na kazi za Mbunge sasa zimeandikwa hawezi kufanya kitu ambacho hakiko katika Katiba. Tumeziandika, asipofanya pia tunajua kwamba kazi yake hajaifanya, hilo ni neno ambalo ni jipya tumeliandika. Tukasema pia kwamba ikiwa Mbunge hafanyi kazi yake wananchi wanaweza kumtoa, siyo Mbunge peke yake lakini kiongozi yeyote ambaye amechaguliwa na wananchi kama hafanyi kazi yake kabla muda wake haujafika huyo anaweza akatimuliwa. Tukasema pia kwamba, si lazima mgombeaji wa kiti awe ni mwanachama wa chama fulani. Independent candidates wanaruhusiwa, ukiwa unapata shida kupata uteuzi kupitia chama fulani uko na ruhusa sasa ya kusimama mwenyewe binafsi, ukataka kura ukapata.

Katika vyama vya siasa tumesema, tumeziekea kazi za kufanya katika Katiba. Vyama vya kisiasa kazi yao sio kufanya campaign wakati wa kura, vyama vya siasa vimeandikiwa kazi zao. Lazima vihusike katika maendeleo, kuna kura hakuna kura lakini chama cha siasa ni lazima kifanye kazi za maendeleo. Chama cha kisiasa ni lazima kiwe na uchaguzi regulary. Kila miaka fulani kulingana na ile Katiba yao na uchaguzi ule utasimamiwa na Electoral Commission na independent body, si chama chenyewe tena waoneane kule ndani. Hiyo tumeandika na tumesema vyama vya kisiasa ni lazima viwe na sura ya kitaifa, sio kwamba ni chama cha eneo moja, cha dini moja, cha kabila moja, cha family moja. Lazima chama cha kisiasa kiwa kinajumuisha wananchi wote wa Kenya ndio kitapata kusajiliwa na tena kusajiliwa kwa chama ni Electoral Commission ndio itasajili vyama hivi. Halafu tukasema kwamba, vyama vya kisiasa sasa vitakuwa vikipata fedha kutoka kwa Serikali. Vile ambavyo vitakuwa vinafuata ile misingi, vile vikwazo tuliviweka ukisoma hapo utakuta ni vikwazo vigumu kwa hivyo si kweli kama vitafika zaidi ya kumi, vitakuwa ni vichache sana. Vile ambavyo vitawahi kupita ule mtihani vitapata fedha kutoka kwa Serikali.

Halafu tukasema pia, Bunge imepewa uwezo wa kuchagua viongozi karibu wote sasa wa kitaifa. Sasa nafikiri hizi karatasi, mummy ungeziweka kule kwenye registration, mtu aki-register anapatiwa maanake kuna a lot of movements na hatutaelewana vizuri. Bunge sasa ndilo linapitisha au linateuwa watu wote wale, viongozi wa taifa, si ofisi ya Rais au si ofisi ya nani. Hakuna ruhusa kuchagua mkuu wa sheria mpaka ipitia Bunge hata kufuta pia. Kwa hivyo majaji wote ni lazima Bunge, mawaziri wote ni lazima Bunge, Chief Kadhi ni lazima apitie pale, nani, mkubwa Kilindini ni lazima Bunge, watu wote bora ni viongozi wa taifa kwanza Bunge likikubali ndio iwe, likikataa Bunge haiwezekani. Kufutwa ni hivyo hivyo, huwezi kusimama tu ukasema wewe leo sio Chief, haiwezekani mpaka liende Bunge wajadili waseme huyu hafai kufutwa atakaa. Unamtaka ni huyu na hamtaki ni

huyu, wakisema afutwe mtu Bunge ndilo linapatiwa uwezo sasa.

Halafu tukasema, utofauti nyingine wa Wabunge hawataweka mishahara yao. Hiyo sasa ni kazi ya Tume ya kuangalia mishahara. Tumebuni Tume mpya hapa ya kuangalia mishahara ya wafanyakazi wa uma na hao Wabunge, Rais, wote ni kundi hilo, kwa hivyo si kazi yao tena. Halafu tumesema, narudia tena kwamba Councillor au kiongozi yeyote, Mbunge, Rais, aliyechaguliwa na wananchi kama hafanyi kazi yake tumetoa utaratibu wa kumwondoa kabla ya wakati wake. Halafu tukasema kwamba tumeunda ofisi ya Waziri Mkuu, yeye atakuwa na Manaibu wake wawili na tumesema atateuliwa na Rais lakini Wabunge ndio wanaamua. Ikiwa hafahi, ikiwa yuafaa, ni Wabunge ndio wataamua na kazi zake tumeziweka. Kazi za Rais pia sasa tumeziandika, ziko katika Katiba tunajua Rais ndiye afanye nini, asifanye nini. Makamu wa Rais tumemwekea kazi zake, yule Prime Minister tumemwekea kazi zake, Deputy tumemwekea kazi zake. Kila mtu na wajibu wake, ndio maana tumesema powers tunaziondoa ofisi moja tunazigawanya kwa kila mtu.

Pia kulingana na hapo tumesema Mawaziri hawatoki kwenye Bunge, Mawaziri watakuwa ni watu mbali na Wabunge. Ukiwa unataka Ubunge upiganie Ubunge, kazi ya Bunge iko. Ikiwa unataka Uwaziri, wale Wabunge watateuwa Mawaziri, watapigania kura wao wenyewe Wabunge uwe Waziri, na tumesema Waziri ni lazima awe ameelimika katika taaluma ya ile Wizara. Waziri wa Barabara awe ni Engineer wa barabara, Waziri wa Afya ni Daktari, Waziri wa Elimu ni Mwalimu namna hiyo. Halafu tukasema Rais ni lazima achaguliwe na asilima hamsini au zaidi ya wananchi wote. Ikiwa hatapata wale wanaopigania hakuna ambaye amepata 50% halafu huna ishirini kwa mia katika mikoa zaidi ya nusu ya Kenya basi sasa itabidi wale wawili ambao wamekuwa number one na number two hao wataenda kwa kura ya mara ya pili na atakayeshinda pale basi, huyo ndiye Rais. Pia Rais tumesena anaweza kushtakiwa kama amefanya madhambi katika kazi yake anaweza kushtakiwe na akipatikana ana makosa achukuliwa hatua za kisheria, moja wapo ni kumtoa mamlakani.

Halafu tumesema kwamba tumetoa Serikali nguvu zake, Unitary State ile ya sasa tumeitoa, sasa Serikali tumezifanya, Serikali ile moja ipo lakini sasa haina nguvu. Kwanza tuna Serikali ya kijiji, Village Government iko sasa. Juu yake kuna Locational Government iko, halafu juu yake kuna District Government, halafu tuna Serikali ya Majimbo, Regional Government, Provincial Council, halafu ndio sasa kuna ile Serikali ya juu. Vile vile ambavyo tumesema powers zitoke kwa ofisi ya Rias tuzigawanye. Mamlaka pia tumeyatoa kwa Serikali ile sasa tumepeleka kila mahali. Tutaeleza zaidi ni vipi, wale walikuwa wanasema wanataka Serikali ya Majimbo, nafikiri siku ile mlilia sana hapa, sasa Serikali ya Majimbo ipo ingawaje haikuandikwa hapo. Hilo neno Majimbo utalitafuta sana hapo hutalipata kwa sababu tukisema Majimbo watu wengine hulielewa vibaya, wamelipaka matope lile jina, majimbo ni kufukuza watu. Kwa hivyo hatukuandika maksudi, ndio mkasema “anauchengu bure, hata hakuna Majimba, hata hakuna nini, hapana.” Yapo lakini neno hilo Majimbo limeleta farakano, sisi tinavyoilelewa huku watu wa Pwani ni tofauti na kule wenzetu wanavyoelewa. Wakisikia hivyo ni kwamba sisi tunawazuia, hapa sasa tumesema tusiandike likini lipo.

Halafu tumesama, kwa sabau ya kwamba Serikali zitakuwa ni nyingi na majukumu yake wananchi walilia kwamba wanaonewa

sana na Provincial Administration tumeiondoa. Hakuna Provincial Administration kwa hivyo ikipitishwa Katiba hii, Machifu, ma-Assistant, ma-DO, ma-DC watakuwa wanarudi ofisini kwao ili kupewa kazi za kufanya.

Mahakama tumesema kwamba, mahakama tumetengeneza mahakama ya juu zaidi. Supreme Court. Kuna mahakama ya kawaida na mahakama ile ya resident, halafu kuna mahakama ya High Court, halafu sasa kuna Court of Appeal, halafu tumeweka nyingine zaidi. Kwa hivyo wewe kesi yako yaweza kupanda gari zote hizo kaka hujapata suluhisho pale basi kutakuwa kuna shida hapo na Majaji kama nilivyosema wote watachaguliwa na Bunge. Na tukasema umri wa ku-retire Majaji ni miaka sitini na tano badala ya miaka sabini na nne. Mahakama ya Kadhi, tumeunda mahakama za Kadhi sasa zimekuwa nyingi, Makadhi wa kitaifa tumeweka thelathini sasa badala ya sita wale walioko sasa. Tumepanua sasa ni thelathini tutawagawanya lakini ni thelathini halafu kuna Kadhi Mkuu ambaye atachaguliwa na Judicial Service Commission pamoja na Waislamu wenyewe. Sasa ni Waislamu ndio watachagua Chief Kadhi wao, halafu tumesema court itakuwa na pahala pa kukata rufaa, Appeal Court na ni Waislamu ndio watakaa kwenye Appeal Court sio Wakristo kama inavyokuwa hivi sasa.

Halafu pia tukasema kwamba kuna Tume tumeiunda iko chini ya Tume ya Human Rights lakini human rights ni Tume kubwa tumeiunda lakini ina sehemu moja ya muhimu sana ambayo wananchi walitaka, inaitwa Public Defender au Ombudsman. Pale ambapo kama umedhulumiwa na mfanyikazi wa Serikali au mtumishi wa uma unaweza kuenda kumshtaki na akachukuliwa hatua. Maneno yote kama yanakosekana unaenda pale na atachukuliwa hatua. Hii ni kwa sababu watu walisema polisi wanaonea watu sana, wanadhulumu watu, kesi zinakuwa zinapelekwa hivi na hivi kwa hivyo tumeondoa hiyo. Tumetengeneza hiyo complaints body ambayo itakuwa kazi yake ni kusikiliza mashtaka ya wananchi.

Halafu tukasema polisi wale Administration Police sasa hawapo tena ikipitishwa Katiba hii. Tutawatia kwenye regular police, ile polisi ya kawaida na ile ya polisi ya kawaida tumaifanyia marekebisho pia. Tumeweka sheria, kazi zao tumeziandika, kazi ya polisi ni nini, utumishi wao tumeuandika kabisa kwa hivyo wewe utakuwa unatembea na Katiba yako lazima unajua. Akinishika hivi namwonyesha kwamba hii si kazi yake. Akinifanyia hivi namwonyesha hii si kazi yake. Zimeandikwa sasa zao na tumewawekea sheria ngumu wafuate polisi ili waweze kurekebisha yale malalamiko ya wananchi walikuwa nayo. Halafu tena majeshi, defence: Majeshi tumesema sasa yata-report sana kwa Bunge ingawaje Rais atakuwa ni Amiri Jeshi Mkuu lakini wale sana watakuwa repoti zao wanapeleka Bunge. Bunge ndilo lina-control Armed Forces.

Halafu upande wa ardhi kwanza tumeunda Tume ya Ardhi ku-replace Commissioner of Lands, kwa sababu malalamiko yalikuwa ni kwamba ofisi ya Commissioner inatumiwa sana na wakubwa kunyakuwa ardhi za watu au kuwapatia watu title ambapo hawafai au kufanya double allocation. Shamba moja hiyo lakini watu sita wana vyeti halafu mnawachiwa vita na ile kesi haishi. Inapelekwa huku, inapelekwa huku, kila mtu akija, au kunaandikwa barua huko huko mtu anapewa cheti anakuja hapa na kukuondoa, hiyo ardhi ni yake na wewe mwenyewe umeishi pale milele na milele. Sasa tumeunda Tume ya kitaifa ya ardhi na tukasema kwamba umilikaji wa ardhi tumeugawanya mara tatu. Ardhi ya Serikali tumeitaja, ardhi ya private land yaani ya mtu binafsi tumeitaja na ardhi ya wananchi. Ardhi ya wananchi ni ile trust land, sasa tumeitoa kwa County Council na kwa

Serikali tumeipeleka kwa wananchi wenyewe. Kama nyinyi Wadigo hapa mtaamua wenyewe akina nani watakuwa trustees wetu, nyinyi wenyewe mchaguwe nyinyi wenyewe. Tena si swala la County Council hilo sasa, limetolewa kule sasa nyinyi ndio mna haki ya kusema hii eka tano tutampatia fulani, heka mbili fulani akitaka mpeni, heka kumi ni za kaya, hilo ni jukumu lenu si jukumu la Central Government tena.

Pia kufuatana na hiyo, tukaweka sheria ngumu kuhusu mazingira, natural environment. Mtazisoma hizo sheria zote ngumu maanake principle yetu ni kwamba wananchi wakae katika mazingara safi. Jambo jingine jipya, tumesema hongo ya aina yoyote sasa ni kinyume cha sheria. Hongo mnajua liko na mara nyingi sana, tumesema sasa katika Katiba, sio katika sheria peke yake tumesema katika Katiba sasa hongo kutoa, kupokea, kutumia, kusababisha kutumia, mambo mengi, hayo yote ni hongo ile. Sasa utashtakiwa na kwa sababu nyinyi ndio walezi wa hii Katiba, ndio walinzi ni wao ndio wasema fulani amehongwa ndio maana akapata ile tender. Ukienda kwa yule Public Defender akienda akifanya uchunguzi akikuta ni kweli basi, ile tender inakuwa cancelled. Kwa hivyo Katiba ikipitishwa kama mtaendelea na kuhongana hongana kwa mahakama, kwa viongozi, kwa nani sasa makosa yatakuwa ni yenu sasa sio Katiba tena. Kwa sababu tumesema shida kubwa ni utekekelezaji, sio kule kwamba sheria hakuna. Sheria twazitengeneza sisi wenyewe halafu tunazivunja sisi wenyewe lakini siku zote tuna mtu wa kumlaumu. Kaka si askari ni Serikali na unajua Serikali huwezi kuenda kushika mtu mmoja kumwambia huyu ndio Serikali. Serikali inaenda ……(vernacular) lakini hunda kwae pole pole wamwambia bwana …….(vernacular) enda na mpango Bwana, ukitoka pale umkali kabisa …..(vernacular). Sasa ni wewe mwenyewe sasa, tumesema katika Katiba hii tunataka open democracy, mambo yote yafanywe weupe kila mtu akiona.

Jambo jingine jipya katika Katiba hii tumesema upande wa kura, nilikuwa nimeruka hapo. Kura zote sasa ni za siri, hakuna kura ya mlolongo, hakuna kura ya kuinua mikono, kura ni ya siri kwa sababu tumesema Serikali tunazipeleka chini zaidi. Serikali ya chini kwa mfano ya vllage au ya location itafanya kazi zote mbili, za Councillor na za Chifu. Sasa hatutaki Chifu ajue ni nani aliyempigia kura au ambaye hakumpigia kura, yule administrator wa location, akijua hivyo kazi itakuwa haifanyiki. Sasa ndio tumeweka kipengele kwamba kura zote ni za siri hata mkienda kwenye mikutano ya cooperative ni siri, mikutano cha kikundi cha akina mama ni siri, mikutano ya uchaguzi wa Mbunge siri, uchaguzi wa uchama siri, ijulikane lakini matokeo ndio yataelezwa.

Pia tukasema kwamba katika upande wa kura madebe ya kura yatakuwa transparent, yale ambayo unaona kule ndani, limejaa au liko nusu au bado. Madebe meusi tumeondoa haya na tukasema zitahesabiwa katika kituo, majibu yatoke pale pale, unaondoka na hesabu tu pale. Basi yale hata akikaa akifanya nini lakini hesabu yetu tayari tuko nayo hapa amepata kumi, pale amepata tano, tunamjulisha, kule amepata ishirini tunajua. Tukifika Msambweni tunajua huyu ashatoka. ***(Laughter).***

Hayo ndio mambo ambayo ni mapya tumeyaeleza katika Katiba mtasoma nyinyi wenyewe kwa uangalifu zaidi. Wale ambao walipata hii Katiba mapema nafikiri wanakubaliana nami kwamba yale maswala yale yote tumeyazungumza. Wale ambao wameipata leo hawajaisoma tutawasomea kwa ufupi sana.

Haswa la muhimu ni kwamba wananchi wa Kenya ndio sasa wamepewa uwezo zaidi wa kuamua mambo yao. Wamepewa uwezo zaidi wa kuhusika katika maisha yao ya utawala kwa sababu ya kwamba mlitaka demokrasia saa muwe tayari. Kura zitakuwa zikipigwa kila siku kwa sababu sasa hakuna kuteuwa tena kwamba fulani ndiye Chifu, fulani ndiye fulani aah. Kila kiongozi sasa ni lazima atachaguliwa na wanaowachagua ni nyinyi, kwa hivyo sasa sio kwamba mlipigania mkapata hii fursa halafu kila mkiitwa mmwambia ….(vernacular). Tuna wakati Bwana, aah. Sasa kazi ni kwenu sasa, kwa sababu uwezo sasa ni wenu sasa. Kwa hivyo hapa kura zitakuwa ni nyingi sana, kutakuwa na kura ile ya location, kutakuwa kura ya kijiji, kutakuwa na kura ya wilaya, kuta kuwa na kura ya mkoa, kutakuwa na kura ya Bunge, kutakuwa na kura ya Rais, kutakuwa na kura nyingi sana. Mkiitwa mjitokeze halafu watu wengine watasema Mbunge hafahi, wakipatikana asilimia thelathini, wametia saini atatolewa itatakikana tena muje mpige kura tena. Pengine yule Councillor au Location Administrator naye ametolewa mtaitwa tena, mwezi ujao pengine wamemtoa mwingine. Sasa ni kazi hiyo sasa…(vernacular). Kazi hiyo sasa na public participation yaani nyinyi kujihusisha ni kwamba kila kitu mnaaangalia sasa. Kile ambacho mmeona makosa muwe mnasema tayari, hiyo ardhi yachukuliwa hiyo na kesi inaitwa, sio kukaa tu mkalalamika huku huku, mambo sijui hata sijui Bwana itakuwaje. Hakuna sasa, Katiba katika sura ya kwanza imesema hakuna itakuwaje ni wewe useme kwamba itakuwa hivi. Hiyo ni sura ya kwanza tumeandika hivyo, sovereignity and supremacy of the Constitution.

Halafu tumesema kwamba sheria za Kenya zitalindwa na wananchi wenyewe na mtu yoyote atakayevunja sheria ya Kenya ana haki ya kuhukumiwa kulingana na sheria hii ambayo tumepitisha. Sheria hii ikipitishwa ni kwamba, sheria zote za sasa ambazo zinakiuka hii sheria hii itarekebishwa, lazima zote ziwe chini maanake hii Katiba ndio sheria kuu katika wananchi wa Kenya.

Halafu pia katika Katiba hii tumeandika mipaka ya Kenya, tumaitaja Kenya ni eneo gani, ina kilometer ngapi ina-square kilometer ngapi tumeandika pia hapo. Halafu tukavitaja vile vigingi kutoka kila cha mwanzo cha Vanga ukikifuata fuata tumeandika pia na hesabu zake, ukiangalia huku nyuma tumeandika na hesabu zake. Kipindi cha kwanza uende mita mia moja utapata cha pili hapo, uende mita mia tano utapata cha tatu hapo. Ukiunganisha laini hiyo utapata map ya Kenya. Kwa hivyo mtu yeyote ambaye anataka kupigia ardhi yetu sasa tuna uwezo wa kumwambia hapa sio kwake, tumeiandika katika Katiba sasa Kenya ipo. Zamani ilikuwa haipo, wenasema tu kutakuwa na nchi inaitwa Kenya, hiyo ndio Katiba ya sasa inavyosema lakini Kenya yenyewe haijulikani ni hii.

Tumesema pia kwamba, (kule kule mzee ambapo unge-register ndio upate yale mambo haya, tumeziondoa hapa kwa sababu tusiingiliane hapa, kule kule). Upande wa vitu vya kitaifa tumesema kwamba mji mkuu bado utakuwa ni Nairobi lakini kifungu cha tatu tukasema kwamba, Serikali yenyewe ile iende ikaamua kama mambo fulani yataondolewa kule kupelekwa mahali kwengine siku zinazokuja, lakini kwa sasa bado Nairobi itakua ndio Capital.

Siku za kitaifa, sikukuu za kifaifa tuwewacha sikukuu tatu tu, tarehe moja June, Madaka Day, tarehe 12, December ambayo ina-combine Jamhuru Day and Uhuru halafu ile siku ambapo Katiba hii itapitishwa tunapendekeza iwe ni sikukuu, hizo zingine

zote haziko.

Pia tumetaja kazi za mwananchi, sio Serikali peke yake tumeandika katika kufungu nambari kumi na tano mwananchi kazi zake ni nini. Tumeziandika pale, usiwe wewe unatazamia kufanyiwa tu, hata wewe sasa tumesema ni nyinyi sasa mfanye kazi zenu, tumeziandika nyingi pale. Umoja wa kitaifa ni lazima uweko, demokrasia lazima muifanye, lazima muhifadhi mazingira, lazima muheshimiane, lazima muheshimu sheria. Mambo mengi lazima muwe wafanyakazi wa nguvu, sio kuzurura zurura ovyo ni lazima muwe mnaweka family zenu vyema. Ni kama sheria za dini tumezitia sasa katika hapo kwa sababu katika dini jukumu kubwa ni lako sio Mungu, ya Quran si ni hivyo? Ni wewe sana ndio kuifanya maanake kazi yako wewe ni kumwabudu Mungu sasa umewekewa zile kazi za kufanya. Hapa ndio hizo sasa, sio Serikali kwamba itufanyie, majukumu yetu yameandikwa pale. Halafu upande wa raia na uraia nafikiri tumeshausema.

Haki za kimsingi tumezitaja nyingi pale, sasa tumeziweka katika sheria. Umuhimu ni kwamba tunasema haki zile za msingi zifanyike au zipatiwe wananchi bila ya kuwadhuru wengine, na tumesema kwamba kwa mfano akina mama tumewapatia haki zao kwa hali ambapo inatakikana. Pahali ambapo inatakikana kwamba akina mama wawe na usawa, tumesema.

**(Interjection).**

**Speaker:** **(**Inaudible)

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Nafikiri watu wanapupa sana na hivi vitabu sasa kile nikizidi kueleza vitabu vinatoka halafu mnasimama, lakini nimesema kwamba mkhatasafi wake nitausoma, hivyo vitabu vitapatikana hata baada ya hapa.

Nilikuwa naeleza kidogo habari za haki za wanawake halafu tumesema kwamba haki za wanawake zitapeanwa pale inapotakikana kuzingatia na mila na dini lakini tu wasibaguliwa akina mama. Halafu wazee, haki za wazee pia tumezitaja mmesikila maoni kwamba vijana wengi hawaheshimu wazee, wazee wakifika umri fulani huwa watu wakiwaona hawataki kuwatia katika shuguli zao kama ambao walifanya makosa kuwa wazee. Kwa hivyo sasa tumesema wazee hawatabaguliwa au kutukanwa, wazee watakuwa wanahaki wanavyotaka katika maisha yao na wanahusika katika maendeleo kama wananchi wengine wa Kenya. Mkiangalia wengi hapa ni wazee lakini ukienda kwenye school committee wakionekana ni ya wazee, vijana wengi hua wanasema …(vernacular). Lakini hawa wana ujuzi wa mambo mengi sana kwa hivyo tumewawekea haki zao hapa.

Watoto ndio ambao wanahaki nyingi zaidi, ukiangalia kutoka thelathini na saba, lakini ni nyingi sana haki zao. Tumewekea lakini haki moja kubwa kabisa ambayo imekuja pale ni kwamba elimu yao itakuwa ni ya lazima na bure kutoka nursery mpaka standard eight kama mlivyosema. Na ile elimu ya kidoto cha nne, form one mpaka form four sasa tumesema irudishwe bei yake chini na Serikali iwe inatoa bursary zaidi pale. Watoto hawatakikani kufanya kazi, lakini mlisema siku ile akina mama

wanapeleka watoto kuuza mahamri na samaki, ile ni kazi sasa imeondolewa kabisa haitakikani. Kama wataka ukauze mwenyewe au mzee akauze. Tumesema kwamba watoto hawawezi kukaa bila ya wazazi wao, watoto kama wameshikwa jela pia ni lazima wapatiwa wakili na Serikali na tumesema watoto wote wapatiwe haki zao, watoto waliozaliwa kwenye ndoa na nje ya ndoa wote wana haki za kuishi maanake makosa sio yao.

Wale ambao wana vilema, persons with disability; tumesema hawa sasa wana haki ya kuwa na haki sawa na wananchi wote, wasibaguliwe kazini, wasibaguliwe shule, wasibaguliwe katika mambo yote, na vitu vyao vipatikane. Kwa mfano tumekuja pia na nakala za wale vipofu za hii Katiba tuko nayo, pia hao nao wapate wakasome, vitu kama hivyo. Tumesema kwamba sasa ni jukumu la Serikali kuwapatia wananchi ulinzi kamili, sasa umeandikwa haswa, ni jukumu sasa la Serikali kuwapatia wananchi ulinzi kamili. Hakuna detention without trial, kule kuwekwa ndani kuzuizini bila kushtakiwa ndio hakuna. Hakuna tuture, kule kupigwa, kuteswa mahakamani ili useme ule uongo lakini useme ni ukweli sasa hiyo tumeandika haswa hakuna tena.

Halafu kitu muhimu pale tukasema uhuru wa dini, uhuru wa dini ni kwamba tumeeleza dini ni watu wafuate dini zao vile zinavyosema zinavyotaka na watu wasibaguane kwa sababu ya dini. Watu waendeshe dini zao, wafanye haki zao za kidini wafanye ibada zao lakini tu iwe siingiliane na ile dini nyingine, na tukaeleza kwamba wale ambao wanaruhusa ya kuenda ijumaa wapewe ruhusa si kwamba utashtakiwa au utafutwa kazi maanake ya mkazi ukienda kuswali. Hiyo sasa ni haramu. Wakristo kuna wengine wanaenda Muskitini au Kanisani Jumamosi, sasa si sheria wao kuenda kazini Jumamosi wanaweza kuenda maombi na bado ni wafanyakazi.

Uhuru wa kijieleza, sasa mko na uhuru wa kujieleza mnavyotaka bora iwe tu sikuchocheana, kuchochea wananchi. Haki za kupata habari za Serikali, sasa kuna haki ya mwananchi kuenda ofisini akasema anataka kitabu fulani au unataka habari fulani. Unasikia kulileletwa kitu fulani ambavyo lazima wananchi tujue na sisi hatujuhi. Hapo sasa ni haki ya mwanchi sio kufanya vile….

Kwanza tumesema kwamba mwananchi ana haki ya kujiunga na chama chochote, kufanya campaign, si ya nguvu, kutumia nguvu. Halafu ana haki ya kujiandikisha kama mwanachama, kama mpiga kura kila siku sio mwaka wa kura peke yake. Kila siku kijana akipata miaka kumi na nane straight away yuenda kuandikishwa na kitambulisho na tayari hapo hapo kura. Basi kuna mwaka huo kuna kura, hakuna kura, lakini hiyo sasa ni haki ya milele, yaani wakati wowote vituo vitakuweko na watu wajiandikishe kupiga kura. Halafu tumesema kwamba kuna uhuru wa kufanya kazi, wafanyakazi wana haki ya kupata mishahara inayofaa, wana haki kufanya kazi katika mazingara mazuri ya kibinadamu. Wana haki ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi, wanahaki ya kugoma.

Halafu tukaja upande wa elimu nimesema elimu tumepeana ni ya bure. Tukaja upande wa maji, tukasema lazima wananchi wapatiwe maji. Tukaja upande wa fair administration, hapo ni lazima nitaje section 65. Mwananchi wa Kenya ni lazima awe anatawalwa kihaki na tukasema kwamba yule ambaye anafikiria kwamba hakutawalwa ki-haki ana haki ya ku-petition kuenda kushtaki kwamba uongozi huu mimi haunifai. Sasa si kinyume cha sheria tena kusema hicho wala sio kwamba utaenda pole

pole, kusema hii sasa itakuwa je jamani? Sasa umepewa haki hapa, kwamba ikiwa unakuta sheria unayoambiwa ufuate haifai utakataa na hapa 66 imesema huwezi kufungwa kwa sababu umekataa amri ambayo unafikiria ni ya …..

Halafu tumetoa haki za wale wanaoshukiwa, washukiwa wale. Wanaoshikwa tumesema kwamba haki zao ziwe za kimsingi wapatiwe, kwanza wasishikwe kwa kutumia nguvu. Ile kushikwa, usirwali imekamatwa hapa au imeshikwa hapa, sasa hakuna hiyo; ashikwe kibinadamu. Nimekuja hapa mimi nimetumwa nambari yangu ya uaskari ni hii, unatakikana uende Polisi. Mngoje Bwana nikavae surwali, mngoje nikavae shati langu tuende, haki hiyo sasa ipo sio kwamba ukose fulani wale jamaa waja pale halafu …(vernacular) lakini wewe uingie ndani ya gari uende. Sasa tumesema yule ambaye anashikwa ni lazima ashikwe na heshima, bado ni mwanadamu, mpaka tuhakikishe kwamba kweli yeye ana hatia sasa ndio vitu vingine vinafuata. Halafu tukasema wale washukiwa wasiwekwe kwenye cell na wale ambao tayari washahukumiwa, jela zao ziwe tofauti. Na tukasema kwamba ana haki ya kuita wakili wake, akisema hapa siondoki mpaka wakili wangu aje, huwezi kumguza mpaka wakili wake aje aseme haya sasa huyu nenda naye. Halafu tukasema kwamba mahakama ni lazima ziwe karibu na wananchi, na tukasema kwamba wananchi ni lazima wakikuta kwamba ile kesi inaenda si hivyo, tumetoa taratibu zake za kufuata pale, anaweza hata kunyamaza ikiwa anakuta ile kesi inaenda vile ambavyo analazimishwa anaweza kunyamaza pia na hakuna kitu ambacho Judge anaweza kufanya lolote.

Tukasema kwamba wale ambao watakuwa wameshikwa wamepelekwa cell ni lazima wapatikane wapatiwe haki zao. Kwanza akina mama na watoto wao waangaliwe kama mama ameshikwa na yuanyonyesha, mambo yake lazima yaangaliwe. Tumesema kwamba wale ambao watakwenda kulala cell kwa sababu wameshukiwa, wale lazima wapate kitanda kizuri, godoro nzuri, blanketi nzuri, choo safi, maji, chakula, matibabu ni lazima, sasa sio ile hiari ni lazima. Na kama hakuna dawa pale, kama una uwezo wa kutafuta daktari wako aruhusiwe pia kuja pale kukupatia dawa na kuenda zake, saa sita aje akupatie dawa aende zake. Tumesema haki pia za mtu kama huyu, kama ni mswali mina na uwe wa swala tano lazima apewe nafasi ya kuswali. Kama ni mtu wa kuenda Kanisani Jumapili hata huko prisons pia kuna Makanisa.

Halafu tukaja upande wa kura, nimeeleza kwamba kura zote ni za siri. Tumeunda upya ile Tume ya Uchaguzi. Tumesema Tume ya Uchaguzi sasa itakuwa na watu wasiozidi kumi wote na kila mkoa utakuwa na mtu mmoja. Tumesema kwamba umri wa kupiga kura bado ni miaka ishirini na moja lakini wale wanaotaka kupigania viti vya uchaguzi pia nao ni miaka ishirini na moja lakini anayetaka kupigania kiti kile cha National Council, ile Upper Chamber, wale ni lazima wawe na miaka thelathini na tano. Kazi za Tume ya kura tumeziandika katika section themanini na nne, wale tumewapatia kazi nyingi sasa na kazi kama nilivyosema za vyama vya kisiasa tumewapatia kazi zao pale.

Bunge kama nilivyosema sasa kutakuwa na Mabunge mawili: Bunge la kwanza litakuwa na wale Wabunge mia mbili na kumi wa hizi constituencies zilizoko sasa. Matuga, Kinango, Msambweni, Kaloleni, Mvita na kadhalika. Halafu tutakuwa na Wabunge tisaini ambao watachaguliwa, watateuliwa na vile vyama ambavyo zitakuwa zimepata viti katika Bunge na wale Wabunge tisaini ni mme - mke, mme – mke namna hiyo. Hao watakuwa wanaunda Bunge lile la kawaida, Lower House halafu

wale Wabunge wa Upper House, ile chamber ya pili ni Wabunge mia moja.  Kila wilaya katika Wilaya sabini itatoa mtu wake mmoja ambaye huyu atakuwa ni Mbunge wa Wilaya ya Kwale katika Upper House.  Hao ndio wanasema lazima awe na miaka thelathini na tano sio ishirini na moja, thelathini na tano maanake kazi yake ile ni Bunge ambalo watu wamekomaa ki-umri.  Kazi yao ni ku-check hii ni Bunge la hawa wenye huenda mbio hawa, hawa wako chini hawa, wakipitishia sheria mbovu ikifika kule yapingwa haiwezekani na zungumzeni tena.

Kwa hivyo watachagua watu sabini, kila wilaya mtu mmoja moja halafu thelathini wale wengine watakuwa ni akina mama. Wanne watatoka kila mkoa, mwachague nyinyi wenyewe, akina mama wanne, hapa Pwani mchague wanne.  Watapigania, watatangaza wenyewe mimi nataka, mimi nataka, mimi nataka, mwachague wanne.  Katika mikoa saba watakuwa ishirini na nane halafu Nairobi ni Wabunge wawili wale watakuwa thelathini na wale sabini itakuwa ni mia moja, hiyo ni Upper House.

Halafu tumesema sheria wanazopitisha lazima kwanza kupata theluthi mbili katika Lower House, theluthi mbili katika Upper House ndio imepita hiyo bila hivyo haiwezekani.  Kwa hivyo itakuwa si rahisi tena kupitisha mswada dakika kumi tu halafu umepita, itakuwa si rahisi tena.  Halafu wakishapitisha mswada ule kama uwe ni sheria, anayetia saini, sheria za Kenya mswada ziwe sheria ni Rais.   Lakini sasa tumempa muda, wiki moja tu kama umepitisha ule mswada uwe sheria ni wiki moja, akizidi wiki mbili awe ametia saini bila hivyo hiyo ni sababu ya kumtoa.

Bunge lile la chini, Wabunge wake watakuwa ni miaka mitano, mitano mitano.  Ile la wale waakilishi litakuwa ni miaka minne kwa hivyo itakuwa sasa hakuna vacuum, hakuna uwazi.  Bunge likivunjwa bado kuna jingine liko, wale wakiingia nao wale wanatoka, kwa hivyo itakuwa continous kazi tunaofanyiwa.

Sasa tunaenda upande wa utawala, Executive; Tumeeleza sasa kazi za Rais ni zipi, tumeeleza kazi za makamu wake, tumeeleza kwamba Rais lazima awe na miaka thelathini na tano mpaka sabini, isizidi miaka sabini.  Na tumesema Rais ni lazima awe ana shahada ya degree ya chuo chochote ambacho kinakubaliwa na wananchi wa Kenya.  Wale Wabunge wa kawaida watakuwa ni form four waliopita, form four with pass sio form four aliye-fail, tumesema form four aliyepita.  Tumesema Waziri Mkuu atakuwa na Manaibu wawili, wote watateuliwa na Bunge.  Tumesema kwamba Mawaziri watateuliwa na Bunge na hawatakuwa Wabunge yao wenyewe lakini watakuwa na nafasi wakiitwa kule Bunge wakaeleze Wizara yao imefanya nini, wanatakikana waende Bunge waeleze watoke waende zao, wawachie Wabunge kazi zao wao nao wafanye kazi zao.

Tumetoa sababu kwa nini hatutaki Waziri awe Mbunge kwa sababu Waziri akiwa Mbunge hima apendelee sehemu yake ya uwakilishi Bungeni au awatese wananchi wake wa sehemu yake.  Maanake akisema yuafanya kazi vizuri ya kitaifa hana time ya kuwa na nyinyi hapa, akisema hafanyi ya kitaifa ime-fail ana-concentrate na hapa.  Kama ni Waziri wa Maji, akisema maji yote yaende kwake yatakwenda kwake, ana nguvu, kama ni Waziri wa Afya akisema hosipitali zote ziende kwake, madawa zote, yawezekana.  Sasa ndio tukasema kila mtu afanye kazi moja, wawe Wabunge wawe Wabunge, tutawajua kama kweli wanafanyia watu wao.  Kama huyu ni Waziri yafaa kweli constituency yake basi ni Kenya nzima, awe ni Waziri wa Kenya

nzima. Na tumesema wale mao-fisa ambao wanateuliwa na Bunge, Permanent Secretary, wakubwa wa mashirikia, Majaji, wote wakiwa wemeteuliwa watafanya kazi kwa kipindi cha miaka mitano mitano lakini kasoro Majaji hawa wengine haizidi miaka kumi. Hata Mkuu wa Polisi pia tumesema sasa atachaguliwa na Bunge, mkubwa wa polisi atachaguliwa na Bunge, mkubwa wa prisons, jela, atachaguliwa na Bunge, mkubwa ma majeshi atachaguliwa na Bunge lakini hakuna kati yao ata-serve zaidi ya miaka kumi. Ukimaliza miaka kumi basi ni vizuri, awe amemaliza.

Mahakama tumeeleza vile ambavyo tunataka, kitu ambacho wananchi walisema ni kwamba kuna corruption nyingi pale, hongo kesi inapelekwa hivi hivi, au kesi zinaamuliwa nje ya korti au ni uwongo? Si mlituambia hivyo? Mtu wako ameshikwa lakini waweza kuenda kumtoa, hata kabla ya hiyo kesi au ile kesi inaamuliwa kinjia ingine lakini unasema wacha waamue halafu tutaonana na wazee. Akishtakiwa, afungwe miaka kumi, amefanya kosa kweli la miaka kumi lakini baada ya siku mbili tunaye hapa hapa maanake umeenda ukatoa elfu hamsini halafu anatolewa. Hayo yalisemwa na yanasemwa na yako kweli. Kwa hivyo, tumesema kwamba hongo haliwezekani na wananchi wenyewe ndio walinzi na Majaji wakipatatikana na mambo hayo tumeeleza taratibu zao za kuwaondoa. Tumesema kwamba hizi korti lazima ziwekwa karibu na wananchi, zisiwe kwamba lazima uelekee kilometer mia mbili ndio ufike kortini. Tulikuwa tunafikiria pia tuweke muda wa zile kesi kwamba kesi isikilizwe kupita muda fulani, bado tunajadiliana kwa sababu kuna kesi huwa miaka kumi. Kila ikifika tarehe, kila ikifika tarehe, kila ikifika tarehe mpaka sasa unachoka, mpaka yule aliyekuwa ameshtaki amekufa sasa haielezeki. Tunataka kuweka pia hiyo tarehe, muda fulani.

Halafu upande wa Serikali za Majimbo nimeeleza pale, nimesema kutakuwa kwanza na Serikali ya kijiji ambapo Serikali ya kijiji itabidi nyinyi wenyewe muamue kwamba mtafanya uchaguzi au mtafanya uteuzi. Hapo tumewacha wazi, kama mtasema yule

afaa ama yuafaa ni nyinyi wenyewe, kaka mtasema debe nyinyi wenyewe tutawaletea madebe. Wale watakuwa ni watu wasiozidi kumi lakini wasipungue sita. Halafu kuna Serikali ya location sasa, itakuwa inachagua watu wawili wawili katika kila kijiji, wawe wanaunda Serikali ya location. Kwa hivyo yale mambo ya mishahara ya wale village chairmen sasa imeshaingia automatically ndio wenye Serikali ile ya nyumbani ile ya chini kabisa. Lakini sio kwamba Serikali ni ya wazee, wananchi wenyewe wa kijiji kile ndio uamuzi ni wao, hatuwezi kuwaambia lazima wawe na umri huu, a, aah, nyinyi wenyewe mtaangalia. Halafu ile location itakuwa na administrator wake ambaye atachaguliwa na wananchi, huyu amechanganya kazi ya uchifu wa sasa na councilor. Huyu anachaguliwa na wananchi wenyewe.

Halafu Serikali ya wilaya, kila location itachagua watu wawili waende kwenye ile wilaya. Hapana, sorry, Serikali ya wilaya inachaguliwa na wananchi wote wa wilaya. Kwa mfano, Wilaya ya Kwale tunatakikana tuchague baina ya watu ishirini na thelathini. Serikali zote za Wiliya zitakuwa hasizidi thelathini, hazipungui ishirini lakini wale wanachama wa Serikali ile watachaguliwa na wananchi wenyewe. Halafu yule mkubwa wao ndiye District Administrator au District Governor huyo ni sawa sawa na Chairman wa County Council anachaguliwa na wananchi wenyewe mbali na wale wengine. Na huyo pia anaweza kutolewa kama anafanya ….(vernacular) pia mnaweza mkamtoa. Halafu Serikali ya majimbo sasa ni yenye

inachuguliwa kutoka zile Serikali za Walaya, wanachaguliwa watu wawili wale, wanaenda wanaunda Serikali ya jimbo wachague mkubwa wa jimbo ni nani, halafu ndio mambo yote, tumeyaeleza pale. Kazi zao pia tumezieleza, majukumu ya Serikali ya kijiji, ya wilaya, ya location, ya jimbo, zote tumeziandika sasa mtashindwa wenyewe. Kila kitu kiko mikononi mwenu musije mkasema haikuwezekana, aaa, sasa uwezo mmepewa. Tumeandika kazi za district ni nini, kazi za province ni nini, kazi za village ni nini, tumeandika.

Ardhi tumeeleza pale lakini kitu muhimu tumesema kwamba wananchi wenyewe ndio ambao watamiliki ardhi zao. Sasa musije mkauza nyinyi wanyewe maanake sisi tuna tabia hiyo, tunalaumu lakini tukipewa tunauza kwa bei ya duni kabisa halafu mnaanza kulalamika. Kwa hivyo tusije tukauza wenyewe halafu mkasema Serikali au watu hawa wanatuonea, sasa mmepewa jukumu pale. Kamati yenu mtachagua nyinyi wenyewe mkubali kwamba huyu anafaa hafai, nyinyi wenyewe Serikali haimo tena, mkitupa mtupe wenyewe. Lakini la muhimu kabisa tumesema kwamba katika ardhi ya Kenya hakuna mgeni ambaye anaruhusiwa na ardhi Kenya ambaye si raia wa Kenya. Sasa tumeondoa, wawe wanaweza kuwa na ardhi kupitia kwa lease peke yake lakini sio absolute ownership, wakaichukulie mkopo. Sasa tumekata, na lease yao ikizidi kabisa ni miaka tisaini na tisa peke yake lakini hakuna zaidi ya hapo. Kwa hivyo ni wananchi wa Kenya ndio watakuwa na uhuru wa kuwa na ardhi na hizi leaze ziki-expire, zikiisha National Land Commission inarudisha kwa wenyewe, wananchi wenyewe wale wataamua tumwongezee au tumpatie mwingine, au hatumtaki basi akae kae tu, wao wenyewe ndio wataamua.

Halafu tumesema kwamba katika miaka miwili baada ya Katiba hii kupitishwa, isipite miaka miwili. Kwanza ni lazima tutengeneze sheria zote za ardhi ziwe sawa maanake tuna sheria nyingi za ardhi zinaingiliana, zinapitana ili nasema hivi, ...ukifuata ile unagongana na ile, ukifuata ya Swazuri unagongana na hii. Tumesema kwanza tutazirekebisha zote. Halafu tumesema kesi za mashamba, kuna kesi nyingi sana za mashamba, tumesema kwamba tutengeneze njia ya kutatua matatizo ya mashamba kwa muda mfupi wa miaka miwili iwe imeisha. Habari ya kwamba kesi mpaka watu walioekuwa wanapiga na wamekufa, wajukuu wao nao waendelea na kesi hiyo hawajuhi pia wale walitetea nini lakini ni kesi wameirithi na bado kesi ile yaendelea, sasa tunataka tuiondoe. Halafu akina mama kurithi, upande wa ardhi tumesema hilo ni swala la dini na swala la mila lakini maswala yote yawe yasiwe yanakiuka sheria za Katiba. Isiwe inamdhulumu, tukisema ni dini ukienda kwa dini haiko lakini wao wasema ni dini au wasema ni mila lakini mila inapingana na sheria ya Katiba itakuwa ni makosa.

Halafu tumesema tena katika miaka miwili hiyo ikiwa kuna ardhi yoyote ilichukuliwa kiholela, ardhi ya uma au ardhi ya Serikali itafanyiwa uchunguzi, ikiwezekana irudishwe kwa wenyewe au kwa Serikali. Land grabbing, hiyo ndio tulikuwa tunasema ardhi inachukuliwa. Pengine mtu ana cheo katika Serikali halafu anachukua ardhi kwa kutumia ofisi yake, siku hizi unasikia majumba ya Serikali yanauzwa elfu kumi, sijui elfu hamsini. Wale hata wafanye nini Katiba ikipitishwa mambo yote yatarudishwa, rewind, waanze kuchunguza. Tumeandika pale katika kifungu cha nne, lazima mambo yale yaangaliwa maanake watu wamedhulumiwa sana na hili swala la ardhi.

Halafu tukaeleza pale katika (b), kwamba tutachungunguza mikataba yote ya ardhi. Hapa ndipo ambapo sisi tumefaidika

mambo ya Mazrui, mambo ya ten mile Coastal strip ile. Tumeandika pale yote itaangaliwa, sasa tutaangalia wataanza mwaka gani, kama ni elfu moja mia nane, elfu moja mia tatu kuchunguza hapo mpaka tuhakikishe kwa ardhi inarudishiwa wenyewe au wanalipwa pia. Imeandikwa hapo. Upande wa madini katika ardhi, wananchi waliuliza kwa nini Serikali inasemekana ukigundua madini ardhi si yako tena. Sasa tumeandika maana ya ardhi ni nini, ardhi ni ile iliyoko chini, mchanga yake na kitu chochote kinachopatikana pale. Kwa hivyo wakija kugundua mafuta pale sasa ni hiari yako kuelewana na yule ambaye atakuja, sio kwamba ikigundulika wewe tayari automatically unaondolewa maanake pamepatikana vitu pale, maanake wewe hukujua wala si makosa yako. Wala si dhambi ukae mahali ambapo pana dhahabu, sasa hii badala ya kwamba kuifanya ni bahati imekuwa ni hatia kwamba pale pana dhahabu, sasa tumeondoa hiyo. Ni wewe mwenyewe sasa, utafuata wewe mwenyewe.

Upande wa mazingira, hapa hakukuwa na shida nyingi sana kwa sababu Kenya inajulikana ndio nchi ambayo inamaliza mazingira yake kwa haraka zaidi. Tumeweka sheria nyingi sana na zinahusiana na wananchi kulinda mazingara yao, wanyama, misitu, samaki na vitu vingi pale tuliandika katika section 239.

Upande wa fedha, fedha za uma kwanza upanda wa kodi tumesema kwamba Bunge peke yake ndilo litapitisha ni kodi gani wananchi watoswa. Hata hii District Council ikipitisha kodi haiwi halali kwanza mpaka iende Bunge ijadiliwe. Kodi hizi ambazo zinakuja, mara leo ni hili, mara ni hivi tumeziondoa. Tukasema kwamba ule mfuko wa kitaifa utakuwa unagawanywa kwa sehemu zote za Kenya, tumeandika hiyo. Tumekuja pia kwa Central Bank, Benki ya Taifa ya Kenya, Benki Kuu ya Kenya sasa tumeitia katika Katiba. Katika Katiba ya sasa hiyo iko katika ministry na treausury, sasa iko katika Katiba. Tumawaeleza pia governor wake atakuwa ni nani ambaye tumesema atafanya kazi miaka mitano, atachaguliwa na Bunge, kama ni mzuri atapewa miaka mitano mingine. Kama hafai ataondolewa. Tumesema pia kazi ya Central Bank ni kutengeneza pesa, noti zile tukasema zisiwe na picha ya mtawala aliyepo. Mtaamua kama ni milima, Mt. Kenya, kama ni bahari, kama ni twiga hapo lakini kwa sababu sasa tutakuwa tukibadilisha Marais kila miaka mitano au miaka kumi. Tukisema kwamba picha ya Rais iweko baada ya miaka hamsini tutakuwa na Marais wengi sana.

Halafu tumeigawanya ofisi ya Auditor General, Controller and Auditor. Sasa Controller tumemweka mtu ambaye anaangalia upande wa makdirio ya fedha, budget. Budget sasa itakuwa inafanywa na wananchi, na wananchi watakuwa wanahusishwa katika budget. Sio Waziri wa fedha akae na watu wake ndio waje wasome budget, hapana. Siku ile ya fedha itakuwa kila mtu anajua kwamba tumejadili nini, kwa hivyo kutatokea nini. Kama ambavyo mlijadili hii Katiba mkatazamia kwamba siku hiyo utakuja ambiwa nini, itakuwa ni kama hivyo. Itakuwa sio ile ya ajabu kwamba mafuta imeongezwa bei, sukari imeongezwa bei hamjuhi, aah, sasa ni lazima wananchi washauriwe. Halafu kuna mlinzi wa fedha za uma tumeandika pale.

Upande wa Public Service, kitu muhimu ni kwamba ile Tume iliyoko ya Public Service tumeiongezea kazi na itachaguliwa na Bunge. Halafu kama nilivyoeleza Kenya Police Service tumeunda katika Katiba, polisi hawako tena office of the President sasa wako katika Katiba. Hawa tumewaandikia kazi zao, halafu pia prisons tumeziita correctional services, watu wa kurekebisha

sheria, taabia za watu pia nao tumewatia katika Katiba. Hata hawa mkubwa wao atakuwa amemaliza miaka kumi. Jeshi; majeshi haya matatu ya Army, jeshi la anga, jeshi la baharini yote tumeyaandika pale, halafu tukaunda Tume ya kitaifa ya security ambapo mkubwa wake atakuwa ni Rais, Makamu wa Rais, Prime Minister. Wote hao karibu watu kumi na mbili watakuwa wanakaa pale, kazi yao ni hakikisha usalama wa wananchi.

Halafu tukaweka pia taratibu na sheria za wale wanaofanya kazi za uma, Leadership and Integrity Code ni lazima. Tumeandika katika sehemu fulani pale kwamba viongozi wote kutoka Permanent Secretary mpaka Rais waeleza pesa zao wamezipata wapi, utajiri wao wameupata wapi. Halafu tukaunda Tume, nyingine zilizoko tumeziacha pale, nyingine tumeziongezea kazi. Lakini tumeunda Tume nyingine kama ile ya human rights ambayo itakuwa na kitengo cha akina mama, kitengo cha yule mtu wa kuenda kushtaki wananchi. Hizo tumezieleza kazi zao hapo, watachaguliwa na Bunge, wote hao.

Tumeunda Tume ya kuangalia mishahara ya uma, sasa hiyo itachaguliwa na Bunge. Tumeunda Tume ya kuangalia kwamba Katiba inarekebishwa, tumeiunda pale na Katiba inatekelezwa. Tumeiunda pale ingawaje tumesema ni ya muda wa miaka miwili. Halafu mwisho tumeeleza nani anaweza kubadilisha Katiba, tumesema kwamba Wabunge wataendelea kurekebisha Katiba kwa maswala yale madogo madogo lakini kwa maswala yale yanayohusu wananchi ni lazima tufanye kura ya maoni. Si ruhusu tena kuwa Bunge kubadilisha Katiba kwa maswala muhimu bila ya wananchi. Kwa mfano, kuhusu mipaka ya Kenya mpaka waje kwa wananchi, kama wanataka kubadilisha, kama wanataka kuiba nchi mbili za Tanzania, kuenda vita, kupigana wawashauri wananchi. Kuhusu uraia, mwananchi anapata vipi uraia? Sasa hiyo ni lazima waje tubadilishe vitu zote, sio wao peke yao. Uhuru wa wananchi pia wao lazima washauriane na wananchi. Serikali za Majimbo na Serikali za mitaa kama zinataka kubadilishwa sheria zake mpaka kura ya maoni.

Halafu tumeweka sheria pale kueleza kutafanyika nini wakati wa Katiba hii ya zamani, inaenda mwisho na Katiba mpya inaingia. Hatuwezi kuwa na ile kwamba, hii itoke, ile iingie siku hiyo hiyo ni lazima kutakuwa kuna uwasiliano vitu vingine vitabakia, vingine vitaenda pole pole mpaka tumalize muda fulani sasa itakuwa ile ya zamani yote imetoka na vile vitu vipya vyote vimeingia. Tumeandika katika sura ya ishirini.

Mimi nitakomea hapa, nimeitaja kwa ufupi ufupi, wale wana bahati ya kupata wameisoma wataona vile ambavyo nimeeleza, lakini wale ambao ninaona kila mtu amepata nakala yake ataenda kusoma halafu mtapata nafasi zaidi na coordinator kueleza zile mnavyotaka. Lakini kwa ufupi hayo ndio mambo ambayo mlisema tukaandike, tumejaribu kuandika hizo sasa ni nyinyi mseme. Ndivyo ilivyo, imepungua wapi, imeongezeka wapi na kadhalika. Haya karibuni.

Basi nitachukua yule ambaye anataka kuuliza au kuchangia atainua mkono, huwa nachukua watu kumi kumi kwanza. Kumi halafu nieleze, kumi nieleze, namna hiyo mpaka kila mtu ambaye anataka kuchangia awe amepata nafasi.

**Mohammed Budzo:** Basi kabla wale watu kumi hatujawachagua ni vizuri kujiulishana kwamba lazima tuelewe haya yote

yaliyosomwa ni yale ambayo tiliachangia siku zile na ningeomba tusichukulie kwamba ni Katiba tayari imeshabadilishwa. Tuelewane vizuri kwa sababu tusije tukaondoka hapa tukasema tayari kwamba polisi sasa hivi hana nguvu. Aah, sasa hivi tuko katika hali ya kuitayarisha ile Katiba mpya ambayo itachukua nafasi ya Katiba hii tulionayo, kwa hiyvo haya ni matayarisho tu ya Katiba mpya. Tumefurahi, tusije tukachukulia ya kwamba hiyo imechukua nafasi mara moja ama ni Katiba ishapitishwa, maana bado kuko na lile Kongamano kubwa la watu mia sita bado litajadilia likiwemo pamoja na Wabunge halafu ikipita hapo kwa kongamano hilo kubwa la kitaifa liende Bunge ndipo ikapitishwa iwe ni Katiba. Kwa hivyo tutachukua nafasi kuwajua wale watu kumi kwanza tuwasajili tuwajue majina yao, wawe wanataka kuuliza maswali yao ama pengine wako na maoni ambayo hawakuyaona kwenye mipango ya Katiba yao mpya. Wainuie mikono wale watu tuchukue watu kumi wa kwanza. Haya, Maalim nambari moja, Bwana Bakari nambari mbili, Bwana Mabwagizo tatu, Bwana Mkungu nne, ndugu yangu hapo tano, ndugu yangu hapo sita, saba, nane, Chairman tisa, wa kumi Mwalimu Barua, hao kumi wa kwanza. Haya, wa kwanza useme na jina lako maanake pia maswali yanakuja, wa kwanza ni wewe Maalim.

**Mohammed Masemo:** Jina langu ni Mohammed Masemo. Kazi yangu ni muhubiri.

**Mohammed Budzo:** Sawa endelea.

**Mohammed Masemo:** Asalaam aleykum. Nina furaha kupata fursa kama hii na vile vile tumewapa pongezi wale watu wa Katiba ambao wanaendelea na viongozi walio hapa, nyote kwa jumla. Basi mimi kidogo ningependa kuchangia katika swala langu ambalo nimeliona liko linaendelea na najua pengine lishaandikwa lakini kwa vile ni muhimu na linachukuliwa tangu Kenya tupate uhuru linaenda kiukoloni. Zile sheria za wakoloni zilizowekwa, kwa hivyo ningeomba niongeze kidogo tena hata kama kimeandikwa. Sehemu lenyewe ni la kuhusu usalama, yaani polisi. Hapa Kenya polisi sheria zao wanazofanya ni za ukoloni, mtu akitaka kushikwa anashikwa na polisi halafu yeye anaweza kumweka kule, na akimweka ndani pale si yeye ataandika statement. Atakuja mwengine ambaye hajui alishikwa vipi wala vipi ndiye ataandikisha kisha pia kule siku ya kesi mahakama pia huyu ataenda, kuna mwingine ambaye ndio wa kesi zingine pale ambaye anaitwa nani yule. Ndio yule criminal ataenda kuzungumza kuzindika yule Bwana na hivi hafai, asitoke, kitu kama hicho. Sasa kwa hivyo, maoni yangu ni kwamba, katika sheria hizi ninataka yule ambaye atamshika mtu, huyu huyu aende akamshtaki na kisha aende naye akamsimamia, wapi? Kortini, kizimbani, kama zilivyo sheria za nchi jirani vile wanavyofanya. Sasa itakuwa yule mwananchi ana uwezo wa kuzungumza lakini hana uwezo leo akishikwa hana uwezo wa kusema lolote. Maneno mawili tu, useme ndio ama hapana basi, hapana rumande ya wiki tatu. Ndio, una hukumiwa, kwa hivyo hilo ningeomba tuliongezewe. Asante.

**Bakari Athumani:** Mimi majina yangu naitwa Bwana Bakari Athumani Mwarang'ombe kutoka huko Muhaka, Kinondo Location, Msambweni Division, Kwale District, Coast Province, hapa ndio kwetu. Sasa kuhusu hii Katiba vile nilivyoisikia na vile nilivyochangia, sikusikia kabisa yale maoni yangu ambayo nilichangia hapa siku ile. Kwa sababu nilikuwa nimesema, sisi watu wa Coast tumetawalwa, tukatawalwa, tukatawalwa. Katibu tuna watawala wasaba. Kwa hivyo mpaka sasa maoni yangu mimi nilikuwa sitaki sisi watu wa Coast tunyimwe haki yetu, tuwe sisi pia ni watawala; sio President atokee Kenya au

Waziri atoke Kenya au pengine Permanent Secretary atoke Kenya, Chairman kama ni wa nini atoke Kenya, sisi watu wa pwani tuwachwe nyuma. Hiyo ndio nalaumu Katiba kwamba haikuweza kuandika maoni yangu na mpaka sasa nataka maoni hayo Katiba yachukuliwa kisawasawa ili sisi watu wa Coast tujulikane kwamba na sisi tuko katika Serikali.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** …(Inaudible)

**Bakari Athuman:** Hapana. Tunataka tupewe haki sawa na majimbo mengine.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** …(Inaudible)

**Bakari Athuman:** Haya, kwa hayo machache hayo ndiyo yalikuwa ni masikitiko yangu kwamba sisi watu wa Coast tumeachwa nyuma na Serikali ya Kenya. Asante.

**Mohammed Budzo:** Nambari tatu ni nani?

**Hamimi Mabwagizo:** Nambari tatu ni mimi hapa. Mabibi na Mabwana Salaam Aleykum. Mimi majina yangu kamili ni Hamisi Mwalimu Mabwagizo kutoka Kinondo. Kwa kweli maelezo ambayo tumeelezwa ni ya kuridhisha, pengine ningeomba Bwana Commissioner kuna kitu kimoja ambacho nataka mfano kiingie kwenye Katiba. Mambo ya uajiri. Mfano, katika sehemu yetu hii ya Diani ama mfano tukiangalia upande wa Coast, katika mahoteli yatu uwaajiri unatumika kimabaguzi. Wananchi ambao kwa mfano ni wengi katika sehemu ile ambayo kwa mfano hoteli iko, utawapata ni wachache kwenye hoteli ama kwenye chombo ambacho kiko hapo. Kwa hivyo tungependa wenyeji wa sehemu ile kwanza wawe wanapata nafasi nyingi kuliko wale wengine wa kutoka sehemu nyingine. Nilikuwa na hayo tu mimi.

**Cllr. Hamisi Masudi:** Mimi majina yangu kamili naitwa Councillor Hamisi Masudi Mwadhani, Vice Chairman Kwale County Council. Niko na maswala mawili, nafikiri Bwana Commissioner umezungumzia kuhusu elimu ya bure kutoka nursery school mpaka class eight lakini nafikiri matatizo sasa si kwamba eti ni mambo ya elimu ya bure, elimu ya bure inatangazwa kila siku. Na kuna vitu ambavyo vinaingizwa humo ndani na sijavisikia hapo, mambo kama ya kipesa, ni njia moja ambayo inatumika, pesa zinatumika. Kuna njia moja, harambee wazazi kuitiwa harambe saa zote watoto wanafukuzwa lakini sijasikia hapo. Kwa hivyo Bwana Commissioner ukisema ni bure nafikiri vitu kama hivyo vingeingizwa, vitolewa ndio viwe ni bure.

Halafu swala langu la pili ni kuhusu mambo ya…umesema kuna Mabunge mawili, moja liko na Wabunge mia mbili na kumi na moja liko na tisaini. Mimi kwangu naona ni kama ni kushangaa kwa sababu …

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** …(Inaudible)

**Cllr. Hamisi Masudi:** Sikuelewa vizuri nafikiria. Ni Bunge moja la watu mia tatu. Sasa basi nafikiri kuzungumzia hapo hapo tu. Nafikiri hii Serikali yetu ilifuta watu wengi sana kazi tena watu wadogo wadogo ambao wanapata mshahara mia tatu ama ni shilingi elfu tatu, shillingi elfu tatu, shilingi elfu nne. Kwa hivyo naona ajabu Wabunge ambao wako sasa, mia mbili na ishirini na mbili, leo Tume hii inakubali waongezwa wafike mia tatu na ambapo wanapata laki nne na kitu. Kwa hivyo naona hapo lazima paangaliwe, afadhali Wabunge kwanza wapunguzwe. Madiwani wakati huu wanapunguzwa na mishahara ni elfu kumi na moja tu, leo Wabunge wanaongezewa kwa hivyo naomba hiyo Tume iangalie hilo tatizo. Badala ya kuongeza Wabunge wapunguze kwa sababu kwanza hawafanya kazi, wakitoka hapa Sunday, hawarudi mpaka sijui Friday, mwenye kufanya kazi ni huyo Councillor badala ya kuongezwa na Machifu wao mnasema pia wafutwe na Wabunge wanaongezwa naona hapo hakuna usawa.

**Mohammed Budzo:** Nambari tano.

**Hamisi Mkungu:** Kwa majina naitwa Hamisi Mkungu. Swali langu liko katika uteuzi wa Mkuu wa Mkoa. Tumepata ya kwamba wale waakilishi wawili wawili kutoka kila Wilaya ndio ambao wakikaa kule watateuwa Mkuu. Kwa hivyo sisi au mimi ninasema kwamba yule mwakilishi hatatuwakilisha kisawasawa katika majukumu ya wananchi, kwa hivyo tunaonelea vile ambavyo Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Kata na Mkuu wa Kijiji anachaguliwa moja kwa moja kupitia kura za wananchi, hata yule mkuu wa Wilaya badala ya kuteuliwa na wale wachache, achaguliwe na kura za wananchi. Hiyo ni moja.

Pili, tunasema kwamba katika mabaraza swali la kupewa nguvu Serikali zile za wilaya halijaguzwa vizuri kwa swala lile la investors. Tunaomba Serikali za wilaya na Serikali za mikoa zipewe nguvu kutafuta investors kwa sababu kuna maswala muhimu ambayo yakiachiwa Serikali kuu huwa kidogo yanaleta utata.

Kitu kingine kimeenda kwa upande wa ardhi, swala la kusema kwamba lease kwa wale ambao si wananchi wa Kenya au si raia wa Kenya. Lease, ule muda waliopewa ni kubwa kwa hivyo tunataka badala ya miaka tisaini na tisa ambao ni umri wa mtu, awe mtu anashikilia lease kwa miaka hamsini na tano tu.

Kitu kingine ni kupata ufafanuzi, kwa sababu tumeambiwa kwamba kutakuwa na Serikali hizi nne, kijiji, kata, wilaya na mkoa halafu na zile Bunge zetu mbili lakini hakujawekwa uwazi kuhusu swala la Local Government. Sijasikia vizuri kuhusu swala la Local Government jinsi Madiwani watakavyoteuliwa kwa hivyo naomba swala hilo liwekwe peupe.

Katika hali ya ugawaji sasa rasilimali, tunasikia kwamba kutakuwa na kiwango maalum kwa sababu hii ni Katiba tungependa kile kiwango kitajwe, ili kule ambapo kunapatikana rasilimali nyingi wawe wanatambua kwamba tutakuwa tukihifadhi sehemu fulani na sehemu nyingine itaenda kule ambapo pia itagawanywa.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Sema chenye unataka.

**Hamisi Mkungu:** Mimi nataka 30% zibaki halafu ndipo zile zitakazoenda ni 70%, itagawanywa tena itakuwa ni 35%, 35%.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Itagawanywa kwa nini?

**Hamisi Mkungu:** Kwa Serikali kuu, 35% sasa inarudi kwa Mkoa, halafu mkoa wenyewe unajua, lakini mwanzo wale ambao wamapata ile rasilimali, mwanzo ibakishe badala ya kurudisha halafu ndipo iletewe, ibakishe mwanzo.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** …(Inaudible)

**Hamisi Mkungu:** 30% mwanzo.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Ibaki wapi, kwa wilaya ama kwa ….

**Hamisi Mkungu:** Mwanzo lazima kutakuwa ni Wilaya lakini bado hatugawanya kwa … wala nini, mwanzo wilaya. Wilaya lazima itaenda mbele. I mean, sorry, mwanzo ni kijiji kwa sababu kijiji kimepata rasilmali, mwanzo, si ndio hivyo imepatikana rasilimali halafu kijiji kiwe kinabakisha zake. Ile ambayo itabaki ni ngapi? 70%, sasa 70% itaenda kwa Location, Location wanapata sasa ile yote, ndipo inagawanywa halafu inaenda kwa division. Ushaelewa? Yaani, ninachomaanisha ni kwamba lazima tutambue kwamba wale ambao wana rasilmali wamefaidi zaidi kuliko…badala ya kuwachwa hivyo.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Hii lease ungependekeza iwe na muda gani?

**Hamisi Mkungu:** 55 years, yes. Kwa hayo machache au mengi.

**Mohammed Budzo:** Numba sita.

**Saidi Nzaro:** Mabibi na Mabwana, Asalaam Aleykum. Majina yangu kamili ni Saidi Edward Nzaro, mimi ni mfanyibiashara tena ni mwenyekiti wa kikundi cha maendeleo Ukunda Sub Location. Nashukuru sana yote tuliozungumza mengi yamechukuliwa na pia nashangaa kwa nini kuna watu wanapinga hii Katiba iliyochapishwa au iliyo-draftiwa. Kwa kweli yote ni sawa lakini kuna vipengele vidogo vidogo, kwa hivyo ni yule Coordinator awe kila mara atakuja asikize maoni yetu na kutueleza vile tutafanya, na kwa kweli tunashukuru kwa sababu Katiba imerudishwa kwa wananchi wenyewe.

Kuna kipengele kimoja cha kuwa, tunashukuru Identity Card na voting zichukuliwe wakati moja, lakini kuna hii passport, passport iwe hapa ndani kwa sababu passport ni taabu sana kupata. Hiki pia iwe ni siku moja mtu anapatiwa akifika umri wa miaka kumi na minane.

Pili ni muda wa kusikizwa kesi, huu naomba hii watu wa Katiba watujulishe na isizidi miaka miwili, iwe kesi imemalizika kwa sababu makesi zinachukua muda mrefu sana. Kesi inachukua miaka kumi, hii inaleta corruption. Halafu hii lease nimesikia msemaji mwingine akisema miaka hamsini na mitano, hii naona ni mingi sana. Kabla sijasikia nyinyi watu wa Katiba mfikirieni mingapi hapo lakini naona kama miaka thelathini hii inatosha kabisa, halafu mwenyewe mtu anachukua mali yake. Halafu muda wa kesi umezungumzwa na haya yote kuhusu muda wa kesi kwa sababu hizi kesi za mashamba huwa pia haya, sina mengi nashukuru. Naomba wale wanapinga hii Katiba waisome kwanza kwa sababu wengi hatujajua hii Katiba inasemaje lakini sasa vile tulivyoelezwa kwa ufupi mengi ni hayo yale tuliozungumza. Asanteni.

**Mohammed Bodzu:** Nambari saba.

**Japhet Mukomba:** Mimi kwa jina naitwa Japhet Wande Mukomba, Mwenyekiti wa Amani Herbal Clinic, Tiba Asili Afrika. Marenya Kenyalo, Mazombo Location katika Msambweni Division. Jambo la kwanzo ambalo nililisikia likitajwa na wenzangu labda hawajalichangia ni madini. Nafikiri wakati tuliokuwa tunapendekeza hali ya mali ya kiasili tulizungumza kuhusu ugawaji sawa na mpaka hivi sasa sijaona kama ushatekelezwa katika Katiba. Tulisema ugawaji sawa, tuwe na kamati zetu kutoka mashinani mpaka national level, hapo hatujasikia kama tumetajiwa. Pia tajiri ambaye anahusika na sehemu kama hizo ambazo zimegunduliwa kwamba anaweza kuchimba. Ahakikishe kwanza ameelewana na wananchi wa pale, ili wananchi wa area hiyo wawe wanaweza kufaidika na mali hiyo kwa kugawanya 30% ya mali hiyo, iwe ya wananchi pale na 70% igawe yeye ni Serikali ili wakishirikiana kwa uwajiri lakini 30% iwe ni ya wananchi wa pale. Tajiri akifika pale ahakikishe amelipa mwananchi wa pale 30% ya ile mali au 30% ya ile mali iko pale iwe inauzwa na wananchi wenyewe kupitia kwa tajiri.

Jambo la pili ambalo hatujajulishwa ni uchaguzi; uchaguzi kwangu vile ninapendekeza ni kwamba ufanywe chini ya Katiba hii ambayo tunarekebisha sasa, uchaguzi usifanyike kwa Katiba ambayo inaendelea wakati huu kwa maana itatutatiza.

Jambo la mwisho ni malipo ya uzeeni; unakuta wazee ambao walishataafu kama mwaka wa sitini na nane kuja hivi wanatatizika kwa malipo yao. Wengi wao wanapata malipo ya chini sana na hata hivyo hakujarekebishwa malipo ya wazee mpaka wanatatizika kimaisha hata kusimamia familia zao. Katika uma wameongezwa mishahara yao lakini wazee ambao wameshtaafu hawajafanyiwa jambo kama hilo mpaka sasa. Kwa hivyo katika Katiba mimi napendekeza iweko, kila review ya mwaka lazima wazee nao waongezwe pesa zoa, si wabaki kama vile walivyokuwa wakati wa ukoloni. Asante sana.

**Mohammed Budzo:** Nambari nane.

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Nani alikuwa nambari nane?

**Julius Mutangili:** Mimi naitwa Julius Mutangili, kisha Civic Education Provider Msambweni Division. Kwanza mimi natoa

shukrani kwa Commission kwa yote ambao yameletwa hapa kwa sababu nilikuwa mmoja wa wale ambao tulikuwa tunaendesha education na mengi ni yale yamesemwa. Nashukuru kwa sababu wale wakiyasikia au draft wakiona watafurahi. Nina mambo kama mawili machache tu. Ya kwanza ni juu ya Mahakama, High Court powers katika koti hizi za Walaya, hilo ni pendekezo langu kuwe na assessors, sikusikia ikisemwa. Assessors wazee, kwa sababu hakuna hapo, pale huwa wanasaidia kama mtu hana wakili na hakuna wazee wengine wanaangamizwa. Hiyo ndio moja.

Ile ingine ni mambo ya watoto, yamezungumzwa lakini nasikitika kuna moja sikusikia, hao chokora wamewekwa wapi. Kwa sababu sasa tuna group mbili ya watoto, wale walio nyumbani na wale wako huko town. Kwa hivyo nilisikia mazungumzo au Katiba kaka inazungumzia wale wako nyumbani, je Serikali au Katiba imepangaje juu ya hawa?

Ile ingine ni Commissions zote si ati ni hii peke yake, zimetungwa nyingi au zimechaguliwa nyingi na Rais na zimezunguka huku. Kuna mambo mawili, kwamba unakuja kusikia kuna Commission fulani ambayo imeteuliwa na imekuwa Pwani na ilikuwa kuonana na wananchi na imeonana na watu wachacha. Tena wakienda, hapaionekani mabadiliko kama hii ya mashamba na zingine na zingine. Mimi mapendekezo yangu kuongeza kwa Katiba ni kungekuwa na moja ingine kubwa ya hizi zote ya ku-follow up. Commissions zikichaguliwa zikitumwa Pwani, ikitumwa wapi, kuwe na ingine juu ambayo haina uhusiano na ambayo ina uhuru, ambayo imechaguliwa na Bunge yaani kwani inajitegemea. Ifuate yale imetekeleza, imejulisha wananchi wote, wametoa mawazo, wamekuwa na nafasi, sikuja leo halafu wanatangaziwa leo halafu ni kesho.

Ile nyingine Katiba ikishamalizika, nashukuru kwa sababu ilikubalika iwe kwa Kiswahili lakini hapo ndio nilikuwa nauliza, wananchi watapataje kwa sahabu wakati ya ile Katiba nyingine ambayo ilitengenezwa Lancaster House 1963 iliwekwa Nairobi tu, mahali haionekani. Hawa ndio wanaikuta wakati mtu akishikwa na polisi ndio law unaipata pale, au ukipelekwa kortini na hatujaletewa na hujui. Ukisema hujuhi hiyo unaambiwa hata kama hujuhi imepitishwa na nashukuru kwa sababu wananchi wameletewa, ile ilitengenezwa na watu wachache.

Ile nyingine ni school yaani kwa vile mapendekezo ya wannachi yamekubalika, Nursery mpaka eight iwe bure lakini kuna vitu vingine hapo kati kati kama yaani kamati ya PTA wanachangia mambo mengine halafu wanatoa mambo mengine. Yaani gharama zingine na badala ya kuita wazazi na kujulikana vizuri wanafukuza watoto na huko ukiuliza wanasema Katiba iko au sheria iko, watoto wasifukuze na unawaona nyumbani. Sasa hiyo inakuwaje sasa, unaona hao njiani?

Ya mwisho, imezungumzwa kutoka nursery au shule ya msingi mpaka secondary, je university? Kuna maoni iliketwa ya kupunguza ni ile sasa ikiwa kutoka secondary ndio watapunguza kidogo fees. Je naye kuna nini… moja ambapo kulikuwa na mapendekezo. Katika university kuna tatizo linaingia hapo, mtoto au yule mwanafunzi akiwa university anapewa loan na ile loan mnamwambia mzazi a-sign, anaambiwa a-sign na yeye mzazi ameumia ana gharama huko nyingi. Katika mapendekezo ilikuwa mtoto au yule mwanafunzi wa university apatiwe msaada na loan kama ni sehemu zingine wapunguze na akipewa loan a-sign mwenyewe halafu akimaliza apewe kazi na Serikali. Apatiwe kazi halafu akipatiwa kazi hatalia atakuwa akilipa. Je, huyu mzee

mali imemalizika anafuatwa hata shamba imeenda, itakuwaje? Yangu ndio hiyo. Asante.

**Rashid Mohammed:** Kwa majina, ndio kuzizi mpaka useme majina manne au matatu. Rashid Mohammed Barua, natoka Msambweni. Kwanza nasikitika kwamba nimechelewa lakini maswali yangu yanakuja hapo nilipokuta, sitarudi nyuma wala sitauliza na nini. Swali langu la kwanza au maoni yangu ya kwanza nataka kuunga mkono ufanisi wa Tume hii ya Katiba ilivyofanya. Nakubali kwamba ni sawa, wale wanaopinga wapinge kwa kibinafsi lakini mimi kama mwananchi mnyonge nakubali kwamba haki yangu imelindwa.

La pili, ni hii habari ya lease, wenzangu wamezungumza na kile mimi nimekuta lakini nataka kusema kitu kimoja. Lease kuna periods tatu, kuna 33, 66 na 99. Hizi ndizo periods za Katiba hii ya zamani sasa sisi yule Bwana aliyesema hamsini mimi nakataa hamsini, tungechukua kipindi kimoja tu cha 33. Nachukua kipindi cha miaka thelathini na mitatu kwa sababu tuna 33, 66 na 99, 33.

Kitu kingine, mwisho kabisa ulisema kwamba nani atakayegeuza au anaweza kugeuza Katiba. Ukataja ni Parliament, kama ni mambo madogo madogo, wakikwama warudi huku kwetu. Lakini mimi neno kukwama silikubaliwi, mimi nasema au napendekeza kwamba wao waweze tu, wapewe uwezo tu wa kuongeza Katiba lakini tukisema na mambo madogo madogo, mpaka ikifika miaka kumi mengine watakuwa wamemaliza yote na tukiuliza watasema si mlisema mambo madogo madogo na sisi hatuyajuhi. Hayakuwa spelt out, kwa hivyo kama ni kuongezea Bwana Mwenyekiti. Ningependa yale mambo madogo madogo yaongezewe, a, b, c, sawa sawa hata mjinga kama Barua akiyaona ajue haya ndio yaliyowaambia au sivyo utakuta kama Katiba yetu ya mwanzo ilivyogeuka hivi, mpaka tukawa sasa tunataka Katiba nyingine. Ni kwa sababu ya uchafu ule wa kuwa walikuwa wana haki, sisi tunasema haki hiyo na itolewe huko kwao iwe kila kitu kwetu. Kwa hayo machache nasikitika ningekuwa na mengine lakini nimechelewa, I could not gather anything mpaka hata vitabu hapa naambiwa vimekwisha. Lakini Mwenyekiti ikiwezekana nitakupa kwenye hicho chako. Asante. ***(Laughter)***

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Kwanza Bwana Masemo unaeleza habari ya masikitiko yako kuhusu askari wanavyoshika watu, wana aandika statement. Tulikuwa tumeshapitia hayo, umekuja kuchelewa lakini tumeeleza wazi wazi haki za askari kushika mtu na mshukiwa na haki za mshukiwa yule. Sasa mambo hayo uliyataja katika Katiba hii hayapo, ni hatia kushikwa kuandika statement ambazo wewe hukufanya lakini unalazimishwa usema kwamba ulishikwa na bhangi na wewe pengine unatoka Msikitini. Pia watu huandikiwa hivyo, tumesema hayo mambo hayo sasa hakuna. Ikiwa unataka kwamba yule mtu aende na aliyemshika ndiye aende mpaka kortini tumeshaweka wazi hapa jinsi ya kufanya mtu akishikwa.

Na mwenzako Bakari Athmani Mwarangombe hata wewe umechelewa lakini tumesema kwamba, wewe siku ile ulilia sana na tape yako tuko nayo hapo ukasema kwamba.

*(Interjection)*

**Bakari Athumani:** …(Inaudible)

**Com. Dr. Swazuri Mohammed:** Basi wacha nikujibu, uliposema mimi sikukuiingilia mbona unaniingilia? Ukasema kwamba tunataka Serikali ya Majimbo tujitawale wenyewe, tufanye vitu vyote wenyewe. Tumeeleza hapa kabla hujaja kwamba Serikali ya Majimbo ipo, na tukasema kwamba uteuzi wa kitaifa na majukumu yote ni lazima uzingatie eneo. Ikiwa Mawaziri ni kumi na tano watagawanywa kwa mikoa, ikiwa Manaibu ni kumi na tano, tumeandika hapa watagawanywa kwa mikoa. Ikiwa kuna wakubwa ambao watachaguliwa wa uma, wale wataenda kwa mikoa. Tumeeleza hapa kila kitu na ni jukumu la Majimbo yenyewe na Wilaya kuhakikisha kwamba wanafanya haki zao. Zile haki ambazo tunasema tumenyimwa sasa ile lawama itabaki kwa district na kwa region sio tena kule juu. Temeeleza kazi, majukumu ya region ni nini, majukumu ya district ni nini. Ukiangalia pale hatukusema kwamba lazima Rais yule awe huyu, lazima awe lakini tumeeleza ya kwamba ni wale wananchi wenyewe wa sehemu ile ndio watachagua. Kama ni kazi jukumu limepewa district ndio itaandika wafanyakazi wake, sasa kama nyinyi wenyewe mtaandika watu wengine shauri yenu, hamwezi kumlaumu mtu maanake uwezo mumepewa.

Mabwagizo, employment haya ndio hiyo narudia. Ukiangalia schedule ya kazi za Serikali ya wilaya utakuta uandikishaji wa wafanyakazi ni wao. Wao ndio wana haki ya kuandika wafanyakazi na wao ndio wanahaki ya kupitisha sheria zile ndogo ndogo za kuandikia wafanyakazi hata hotelini penye wao bora sheria ile isipinge Katiba. Hapa, hapa Kwale wanaweza kutunga sheria zao kwamba pakiwa na kazi ni lazima iwe kadha na kadha lakini sheria hili isiwe tu inapinga Katiba. Hiyo ni yao, sasa nyinyi wenyewe ndio mtashindwa wenyewe.

Mwanzani Councillor, free and compulsory education. Sasa tumesema kwamba jukumu la huduma zote, Serikali ihakikishe kupitia kwa Serikali hizi za chini haswa district ndio ina kazi sasa kama vile zamani PWD, County Council, VLDB ndio imerudi sasa. Si zamani ilikuwa kila kitu kinaitwa ni County Council, sasa ndio hii sasa. Kwa hivyo kama ni free education sasa ni ile Kenya School Equipment Scheme sasa, wao ndio wataleta kila kitu, hakuna haja ya ku-charge tena wananchi. Ukiangalia katika kazi za wilaya hiyo ni kazi yao moja.

Kwa hivyo tena umesema Wabunge wapunguzwe kwa sababu hawana kazi, kilio cha wananchi wengi Bwana Mwanzani ni kwamba watu wanataka utawala karibu, kwanza wanataka waongezwe. Nafikiri watu wengi hapa walisema hata hii Kwale inataka nafasi tano, sita za Ubunge, sikusikia watu wakisema hawa watatu ni wengi sana au tuwapunguze, aah. Kwa sababu nambari ya watu inazidi na watu wanavyozidi kuongezeka Mbunge mmoja hawezi tena ile idadi, kwa hivyo watu wengi wamesema waongezwe. Kwa hivyo ndio tumesikia vilivyo hivyo na wewe umesema kwamba wanalipwa pesa nyingi na hawana kazi za kufanya hawafanyi kazi. Sasa tumesanyisha hapo, tumesema kwanza kazi yao kwa sasa ni full time. Sio ile Jumanne, Juma tano ijumaa, sasa ni Monday mpaka Friday ili tukakupatia nguvu wewe ukimwona hafanyi kazi unamtoa. Zaidi ya hivyo ni vipi tena, hata waalimu pia kama hamwendi kazini mna sheria zenu. Wewe kama mfanyikazi unasheria zako, ukikosa kazini utafutwa kazi, ndio hiyo sasa.

Hamisi Mkungu, Provincial Governor achaguliwe na wananchi hiyo tutaweka na investors pia hiyo imekuwa ni kazi ya district lakini pia tutaenda kuongeza. Upande wa lease, kwa kweli lazima mjue kuna lease mara mbili hapa, kuna lease ya yule mgeni ambaye si Mkenya. Tunasema tumpokonye haki yake ya kuwa na shamba mpaka afanye lease halafu kuna lease za sisi wenyewe hapa hapa. Kama umepewa Government land, pia kule kuna lease, unaweza kukodi ardhi ya Serikali kama mwananchi ndio hizo 33, 66 na 99. Zamani zilikuwa za 999. Sasa hii lease tunayosema sisi ni ile ya mwananchi, yule mtu ambaye ni mgeni ambaye si raia wa Kenya. Kuna Wazungu hapa Wataliani, Wajerumani nini, sasa tunasema wale ndio isizidi miaka tisaini na tisa hatukusema hii ya humu humu. Kama unataka ardhi ya Serikali upewe lease, hiyo hatukuijadili. Tulijadili ile ambayo wananchi walilalamika sana kwamba wao hawana ardhi lakini kuna Wajerumani wanaeka elfu kumi. Tena wamepewa miaka mia tisa na kitu lakini mwanzo ilikuwa tumeweka miaka arubaini, sisi wenyewe tulipoandika ilikuwa miaka arubaini, lakini kukawa na malalamiko kwamba kuna wengine huwa wanaitumia vizuri ardhi ile kwa upande wa ukulima kwa hivyo tuwapatie miaka tisaini na tisa. Lakini ni swala ambalo mmeeleza kwa hivyo tutaenda kuangalia. Halafu sharing ya resources, kugawanya zile percentage wametoa hiyo ni sawa.

Said Edward: passport, ukisoma kitengo nambari kumi na sita, kifungu nambari kumi na sita imeeleza wazi wazi pale sasa passport ni haki ya mwananchi. Angalia 16 (i), c, utakuta kwamba hivyo ni vitu ambavyo ….(vernacular) si kitu cha kwamba ni favour tena, ni lazima mwananchi apatiwe akitaka. Maanake hatukusema kila mtu anayezaliwa apewe passport, wengine hawataitumia milele, si ni hivyo?

**Audience:** Ndiyo.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Kuna watu hapa hata wako hapa lakini hata Kinango hajafika, utampa passpoti huyo? Hapa hapa Kinango hata kufa hivyo hivyo hajafika, sisi wenyewe twajijua lakini tunasema kwamba ukiwa unataka passpoti usinyimwe ukifika pale upewe. Hiyo tumeandika nafikiri ukisoma 16, C. Halafu zile kesi umesema ziwe decided katika miaka miwili nimesema hiyo tunaiangalia, tunataka kuiandika.

Bwana Mukomba: nafikiri umekuja kuchelewa, Japhet sijui uko wapi, ameondoka. Amekuja kuchelewa na ameshaondoka, ndiye yule kule. Hilo swala la madini tulikuwa tumeshalijibu sisi kwamba sasa sio kwamba ikipatakina madini ni ya Serikali, aah. Tumesema sasa ni yako na yeye ameuliza hivyo. Akasema kwamba kitu ambacho hakukiona hapa ni kwamba uchaguzi ufanywe na Katiba mpya, hatuwezi kuandika hiyo sisi hivi ni vitu viwili tofauti lakini sisi maoni yetu hata sisi ni kwamba uchaguzi unaokuja ufanyika na Katiba mpya. Sisi kama Tume position yetu ni hiyo maanake ilikuwa haina haja basi kufanya hii kazi halafu tuweke kando tuendelee na hivi hivi. Haja ilikuwa na mabadiliko sasa kwa hivyo ilikuwa sisi pia tunaomba hivyo lakini funguo ile ina mtu fulani ambaye sisi hatuwezi kumlazimisha.

Retirement benefits; hilo ni swala ambalo kweli hatukuliangalia tutaenda kuliangalia kwamba mishahara ya mfanyakazi wa kawaidi ukiongezeka na yale marupurupu ya mzee aliye-retire naye pia yaongezeke, hilo tunalishugulikia.

Mambo ya district courts, Mzee Mitangili kwamba unataka assessors hilo tutalikwenda kuliangalia, tumeliruka hilo. Wale watoto wale chokora, hatukuwataja moja kwa moja lakini tumesema katika misingi ya kitaifa kwanza wananchi wa Kenya tunataka warudi kule kwa family. Katika Katiba ya sasa family hata haitajwi, sasa tumesema kwanza lazima tuzingatie jamii kwanza. Tutilie msingi umuhimu wa kuwa na jamii maanake tunataka kuondoa hizi nambari za watoto wale wa mtaani. Kwa sababu ikiwa tumeshikilia umuhimu wa jamii sasa mtoto atakayezaliwa yeye ni mtoto wa ndani ya jamii.

Hivi sasa tunakuta watoto wetu wengi wameacha misingi ya kijamii. Unasikia hizo zinaitwa, come we stay? Huku kwetu tunaita kinyumba, muweke kinyumba. Sasa huku kwetu ukimweka kinyumba kidogo social security yetu bado iko juu lakini kwa wenzetu imeisha wakishazaa mtoto, wakishakosana mtoto anatupwa kwenye street. Hiyo ni njia moja tumesema ya family ili tukasema kwamba sasa ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba watoto wote, hatukubagua pale tukasema mtoto wa family wala mtoto wa street wala nini tumesema watoto wote wa Kenya. Kushikilia na pia kutilia mkazo tukasema mtoto yeyote wa Kenya anayepatikana mtaani ambaye ana chini ya miaka minane hajulikani kwao ni wapi tunampa uraia wa Kenya. Tumeandika hapo katika sura hiyo, kwa hivyo hawa watoto pia tunawashugulikia ni watoto wetu sasa, Serikali ndio tumeipa Bunge ipitishe sheria kuhakikisha watoto hawa watasoma vipi, watapata malazi vipi, watapata chakula vipi na kadhalika.

Follow up Commission ndio nafikiri ni wazo nzuri tutaliangalia. Katiba isambazwe kwa wananchi wengi, tulikuwa na maoni kwamba hata ifundishwe shule kwa hivyo hiyo pia tunaishugulikia lakini kwamba itakuja kwa lugha ya Kiswahili. Hiyo inapatikana kila mahali, hiyo tumesema.

School fees, umesema kwamba huwa ni bure lakini ukienda kule sijui kuna PTA, hilo sasa tumeshalijibu kwa upande wa districts, wao ndio wataweka sheria na ndio watatoa mambo ya vifaa vya shule. Upande wa wale wanafunzi wa chuo kikuu, maanake unajua huwa ni vijana sana wa miaka kumi na sita, kumi na saba sasa ana-security gani? Hana hata kitanda kwa hivyo afadhali wewe mzee wake tunaweza tukakushika wewe tukakuminya minya tutakutoa kitu, lakini sasa yule yeye tutamwandika vipi? Kwa hivyo ile sababu ya kwamba wewe ndio u-sign ni kwa sababu ni watoto mno wale wengine huwa ni minors, chini ya miaka kumi na nane bado ni minor huyo kwa sheria ya Kenya. Lakini kusema kwamba wapatiwe kazi na Serikali halafu wakatwe hiyo loan yao hiyo ni sawa. Kwamza tumesema kwamba kuna haki ya mwananchi wa Kenya kupatiwa kazi.

Halafu Mzee Barua pale kwa bahati mbaya amekuja kuchelewa lakini anasema ataninyang'anya hii yangu ni sawa. Hizo lease ndizo hizo nimezieleza, pale niliposema kwamba wale Wabunge watabadilisha maneno madogo madogo pengine nimetumia lugha ambayo haeleweki, lakini vitu ambavyo wao wanaweza kubadilisha tumeziandika lakini vitu ambavyo hawawezi kubadilisha ni mengi sana. Kitu chochote ambacho kinaingiliana na sovereignty, uhuru sasa hii Katiba yote ni kuhusu sovereignty ya mwananchi wa Kenya. Ndio nikasema yale yamebakia ni mambo madogo madogo sana halafu C, (ii) kama watafanya hivyo vidogo vidogo vile viwe vikubwa tumeweka wazee pale, Bunge la Upper House. Ndio tukasema umri wao ni thelathini na tano mpaka sabini hao wengine ni ishirini na moja mpaka sabini. Wale kazi yao ni kuhakikisha kwamba, kwa

sababu wale wamechaguliwa na wananchi kutoka district mswada ukija kule wanahaki ya kuwaita tena jamaa wale waseme hivi, mwasemaje? Wanasema nenda ukakatae kabisa hatutaki maneno yao, yule anarudi kule anaambia wenzake wangu wamekataa, nyinyi mwasemaje wetu wamekataa. Ikiletwa kutoka Lower House inaambiwa hiyo tafutieni mengine lakini kama ni hilo haliwezekani, ndio maana tunaweka watu ambao kidogo wamekomaa kiumri.

Haya watu wengine kumi.

**Mohammed Budzo:** Haya tutaanza, Bwana ni nambari moja.

**Speaker:** Anza hapa.

**Mohammed Budzo:** Tumeanzia huko tunaanza hivi sasa. Bwana Chief nambari mbili ndugu yangu nambari tatu, nambari nne, nambari tano, nambari sita, nambari saba. Hapo ulikuwa wapi? Nambari nane, nambari tisa, nambari kumi kule mwisho. Nafikiri tumeshajua nambari zetu, unasimama, unataja jina lako unaendelea na swali lako. Nambariri moja.

**Abdalla Rashid:** Asaalam Aleykum waraha mutalilahi wataalha Wabarakatu.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Abdala Rashid:** Mimi jina langu naitwa Abdala Rashid Mwakuyumba kutoka Diani Location. Maoni yangu nachangia ya kwamba katika Pwani hii tunajulika kwamba sote tu Waislamu kwa hivyo katika Uislamu na misingi yake ya kidini, na jambo ambalo linatutiza sisi, tunatatizwa na mambo matatu. Jambo la kwanza ma-bar katika sehemu zetu za Pwani yamezidi sana tuna takriban kama ma-bar kama thelathini mbali na yale ma-bar yalio beach hapa hapa. Yenyewe hapa kwetu location hapa ni ma-bar zaidi ya thelathini.

Jambo la pili hivyo hivyo, ni kwamba wanawake wanatembea uchi kiasi cha kuwa hata ukitembea na baba mkwe wako….

**(Interjection)**

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Ngoja kwanza ndugu yangu, wakati ukitaja neno toa na maoni yako. Mfano umetaja bar nyingi watakaje? Ndio pale ile unataka ndio tunataka.

**Abdala Rashid:** Sawa. Kwa hivyo katika bar hizi ningependa bar hizi zitolewe.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Zote.

**Rashid Abdala:** Zote hatuzitaki katika hizi sehemu za hapa.

Jambo la pili, wanawake kutembea uchi: hatutaki wanawake watembee uchi wanawake wajihifadhi kama hivi alivyohifadhi huyu mama hapa. Jambo la tatu ni kwamba tuko na wanafunzi ambao wanasoma Madrassa na tuko na wanafunzi ambao wanasoma mashule lakini ajambu ni kwamba video zimekuwa nyingi kiasi ya kuwa watoto hawa hawasomi vizuri. Kwa hivyo ningependa kama watafanya video zao, wazifanye night video lakini si hizo za mchana kulingana na mazingira ya watoto vile tunataka wasome. Kwa hivyo ndugu zangu Waislamu wasiokuwa Waislamu yangu maoni mimi ni hayo. Asanteni.

**James Nyanje:** Mimi jina langu naitwa James Nyanje, Senior Chief Mwereni. Nina maswali mawili au maoni mawili. La kwanza ni upande ule wa village Government mpaka kufikia district na provincial Government. Kwa maoni yangu nimejisikia kwamba hali hiyo itahitaji pesa nyingi sana kwa sababu wale wa utawala uliopita kule mashinani kabisa wamefanya kazi kama polisi saa, zingine kama Majaji hali nyingi sana. Hali ikitokea hivyo sasa mabadiliko tunataka kuwe na polisi wengi sana huko mtaani ambapo Serikali ya sasa hawana. Kunahitajika kuwe na makorti kabisa mpaka level ya village, inahitaji Judge, pesa hizo zitatoka wapi, hiyo itafanyika kwa muda gani mpaka hii Katiba iwe sawa sawa?

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Maoni yako?

**James Nyanje:** Nimesema itahitajia askari wengi sana, polisi na makorti.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Maoni yako kwa hivyo iweko hiyo, tuliondoe?
**James Nyanje:** Iweko lakini ifanyike vile najifikiria itafanyika kwa sababu italeta shida nyingi sana kule.

Ya pili, ikiwa ni shule zitakuwa kutoka nursery mpaka standard eight ni bure na wazazi saa hii hawana mashule mazuri, inahitajika pesa za kuwa zijengwe shule kule kabisa za sawa sawa ndio heri ikiwa bure watakuwa wanapata ma-desk, watakuwa wana vyumba vizuri, lakini wakati huu ikiwa ni free mzazi hatakuwa ana-chajiwa pesa yoyote kutakuwa na shida. Kwa sababu hiyo bure ni kuwa hakutakuwa na ma-desk, hatutakuwa na majengo. Kwa hivyo inahitajika kabisa kuwe na pahali kutatoka pesa sijuhi zitatoka wapi na hii Katiba hii mpya. Hayo ndio yangu.

**Meshack Kaliti Makula:** Jina langu ni Meshack Kaliti Makula natoka Kinondo ya Chale, Location ya Kinondo. Yangu ni swali tu ambalo nahitaji ufafanuzi zaidi, katika hii Senate House ama hii Bunge ya juu. Nimeona kwenye hii draft kwamba baada ya kila district kutoa mwakilishi mmoja itakuwa na Wabunge sabini halafu tutakuwa na thelathini ambao wanahitajika zaidi ambao watakuwa ni akina mama kulingana na vile nimesikia. Swali langu ni hili, katika hawa thelathini ambao watatoka kutoka kwa kila Wilaya, je wakipatikana wanawake hapo je hao waume watupu halafu ndio sasa hawa thelathini wa wanawake hawa watachanganywa pia? Ikiwa ikiwa ni hivyo si hii itakuwa zaidi ni wanawake kwenye hiyo Bunge? Yangu ni

hiyo tu.

**Ali Hassan Mwakulonda:** Mwenyekiti, waliohudhuria, Salaam Aleykum.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Ali Hassan Mwakulonda:** Kwa majina naitwa Ali Hassan Mwakulonda mimi ni mwalimu, nina mapendekezo kidogo hapa. Kwanza nitazungumzia kuhusu education, nafikiri Katiba imepatia mamlaka Serikali za wilaya kushugulikia mambo ya nursery, ya pre-primary, primary na secondary, lakini haikutoa mwongozo wa college na university. Kwa hivyo ningependekeza pia lile jukumu la colleges na universities pia lipewe Serikali ya wilaya kwa sababu lile national Government nafikiri imeweza kuregesha nyuma mambo ya colleges na universities katika sehemu za mikoa mingine. Kwa hivyo nafikiri jukumu hili ikipewa Serikali ya wilaya huenda pia pengine zile sehemu zingine tukaweza kupata universities.

Ya pili ni upande wa ardhi, nina vipengele kama viwili hapa upande wa ardhi. La kwanza najua Commissioner ameeleza vizuri upande wa lease lakini nataka kutoa tu kipengele kidogo tu kwamba yule foreigner atakayepewa ardhi, ile lease iwe miaka ambayo imesemwa hapa watu wamependekeza, lakini mimi sitapendekeza hiyo miaka. Nataka kusema tu kwamba, ikiwa mtu yule amepewa ile ardhi halafu ile kazi yake ambayo alikuwa anataka kufanya imekwama katikati lease ile iishe pale pale. Tusingoje miaka tisaini na tisa au miaka sitini au miaka thelathini. Nimepewa ardhi mimi nilime mihogo, nimetengeza factory yangu ya muhogo baada ya miaka kumi factory imekufa, ardhi ni yangu. Nimechukua loan pengine milioni arubaini, nimechukua million ngapi, kwa hivyo yule mtu atakaye anapeana loan kwa bank kwa yule mtu foreigner ajue kwamba akishindwa ile business ardhi imekatika inarudi kwa wananchi.

Lingine ni land review: Katiba imeeleza kwamba, ifikiriwe upya mambo ya ardhi ama yaangaliwe tena mambo ya ardhi, upande wa Pwani, Rift Valley na sehemu zingine. Nafikiri haikutoa kwamba baada ya kufikiri upya au kuangalia upya zile ardhi zitafanywa nini. Kwa hivyo mimi ningetoa maoni kwamba na nitaongeza kipengele cha foreigner hapa kwamba kama ile ardhi ile iko Diani Location au iko Kwale District lakini yule alikuwa allocated hapo mwanzo ama baada ya kufanyiwa uchunguzi kwamba yule mtu alipewa ile ardhi kinyume na sheria ama si halali kuwa alikuwa apewe, kwamba ardhi ile iregeshwe moja kwa moja kwa wananchi. Na kama alifanya maendeleo yoyote katika ile ardhi iwe pengine Serikali ya wilaya itafikiria ile ya kum-compesate ili isiwe kwamba mtu amekosa ile ardhi na maendeleo yake katika ile ardhi halafu aondoke hivi hivi tunaweza kuleta mambo mengine lakini mtu yule awe compensated kidogo kulingana na vile ame-develop ile ardhi. Lakini ardhi ile asiambiwe ainunue tena wala namna gani, irudi moja kwa moja mpaka kwa Serikali ile ya wilaya.

Kipengele chengine, nafikiri ili Bunge limepewa mamlaka mengi kidogo kwa sababu Katiba kuna sehemu ambayo imesema ni Act of Parliament. Itaamuliwa na Act of Parliament, kugawanya rasilimali na nini na nini itaamuliwa na Act of Parliament. Kufanya nini itaamuliwa na Act of Parliament. Mimi ningeona kwamba hayo maoni yetu au ile kongamano la kitaifa wale

watakaochaguliwa katika Wilaya waone kwamba wamechukua maoni kama hivi kabla hawajaenda kule. Waje hapa wachukue yale maoni ili kwamba wakifika kule katika lile kongamano la kitaifa, yale maneno ya hawa watu ndio yataingizwa pale. Parliament yake iwe tu ni kuona kwamba ni kupitisha yale ambayo yamejadiliwa katika kongamano la kitaifa lakini si tena waende tena chini waseme eeh, hii nyilaya ipewe…. asilimia kumi, hii nyingine… Tukifanya hivyo itakuwa tumeitoa tena, nafikiri tulitaka kusema kwamba Katiba iwe….. mamlaka kutengeneza hizi, haki zote waeleze vile ilivyo ikifika kule Bunge iwe ni kupitisha. Ni hayo Bwana Commissioner. Asante.

**Suleiman Said Yeya:** Mimi kwa jina naitwa Suleiman Said Yeya. Mimi ni mwanasiasa na naunga mkoni Katiba hii kwa sababu asilimia sabini na tano ni manifesto ya shirikisho. Isipokuwa kuna vipengele fulani ambavyo kidogo naviona na giza. Swala la ardhi, kule bara kwa wenzetu utapata mashamba yale yaliokuwa na Wazungu ya heka kama elfu mia tatu, elfu themanini, Wazungu walipoenda yalichukuliwa na viongozi waliokuwa Serikalini na hawakuchukua kijinga, waliweka mizizi yaani wamechukua kabisa kabisa. Yaani na maandishi yote ya kuwa huna nafasi ya kumshtaki. Kimaoni yangu, ninesema lazima tukate shauri kuwa mwananchi wa Kenya, ikiwa na nafasi apate heka mia mbili ili wananchi wengine ambao hawana uwezo wapate ardhi angalau nusu heka heka.

Swala la pili ni kuhusu dini: hizi dini zimekuwa ni kama vyama vya siasa, moja akiweka jukwaa hapa, moja anaweka pale. Sasa wananchi wanachanganyishwa ama wengine wanauziwa. Kwa mfano, ikiwa mna Msikiti Waislamu, mahubiri yenu mfanyie kwa Muskiti na ikiwa Wakristo na Kanisa lenu mahubiri ufanyie kwa Kanisa lenu. Yule ambaye anataka kuwa Muislamu aende Musikitini na yule ambaye anataka kuwa Mkristo aende Kanisani lakini sio kuweka magwaride, nini barabarani, karibu na Muskiti ama karibu na Makanisa. Kimaoni yangu hiyo inatatiza ama hatuyataki. Asanteni.

**Juma Hamisi Barua:** Salaam Aleykum Warahamatulahi Wabarakatu. Kwa majina naitwa Juma Hamisi Barua, Civic Education Provider wa Diani Location. Mimi yangu ni maswali tu kuhusu lease. Kwanza ningeomba hiyo Tume itufafanulie neno lease maana hiyo ni terminology, wachache wanaielewa na wengi hawaielewi.

Halafu pili, nataka nijue hii ardhi ikiwa-leased kama mwalimu wangu alivyopendekeza kwa miaka ile thelathini na mitatu baada ya kumalizika ile miaka thelathini na mitatu ardhi hii inarudi kwa nani? Halaru tatu, pia naomba nijulishwe ardhi ambayo iko leased, yule vendor au yule mwenye shamba aliyeshikilia anayohaki ya kuiuza? Asanteni.

**Salim Ali:** Habari zetu ndugu? Mimi sina mambo mengi isipokuwa ni kwanza naunga mkono Katiba mpya kwa haki ama uhuru kupatia wananchi wa Kenya.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Sema jina lako?

**Salim Ali:** Jina naitwa Salim Ali. Kwanza naunga mkono Katiba mpya kwa uhuru ambao imetupatia hivi kuweza kuzungumza

matatizo yetu ambayo yalikuwa yanatukereketa siku nyingi. Nafikiri kwanza nitazidi kutoa maoni yangu ya kwanza kufuma mishahara. Hivi nafikiri linatatiza si mishahara ule wa kuandikwa kwa mwezi hata huu mishahara wa kulipwa kwa siku yaani kibarua zile, wages. Ningeomba Katiba hii itupatie uhuru kutoka sehemu za ngazi za chini ama ngazi za juu ili kujadili mishahara za kila eneo la mfanyikazi kwa sababu imeonekana Kenya ni yenye kunufaisha the higher profiles while the low profiles are in loss. Ambapo utakuta Mbunge analipwa karibu milioni, mwananchi wa kawaida waiter, mwalimu, mwalimu mpaka leo anagoma. Mambo kama haya ni kwa sababu Government inasemekana iko na wakubwa lakini Government hakuna kwa watu wengine. Kwa hivyo ningeomba Katiba hii itunge Tume maalum ambayo itajihusisha kwenye ukarabati wa hali kama hii ya mishahara.

Pili, nitazungumzia kuhusu urithi ama mashamba: ilikuwa mara nyingi tumekuwa tukidai haki zetu baada ya wazazi wetu kufa ambayo nafikiri ni makosa. Nafikiri ni jukumu la kila mzazi kuona yeye yuko na watoto na watoto wale wamekuwa. Isiwe tu mpaka yeye afe pengine ndio uwezekane ushauri jinsi watoto wale watakapogawanya mali ile lakini iwekwe sheria. Nafikiri ni kama tukiangalia upande wa bara tunaona mtu akifika umri fulani mika ishirini na tano ama kabla ya miaka ishirini na tano kuna ule uzoefu wanaambiwa sehemu hii baba ni yako, wewe utakuwa ukianza kulima hapa kuenda huko. Sasa watu kama hawa wote wanakuwa kila mmoja, he has a mind, yaani ana zile akili za kufanya kutokana na mahali pale. Nafikiri ni kwamba mzazi yule anapofariki ni kila mmoja ameshajihusisha na sehemu zake na yuko mbele kuliko tungoje mzee yule anauza mashamba. Hakuna haki, hatuna nguvu ya kuzungumza. Mzee yule amekufa mnaweza kukosana na kukatana na mashoka.

Ningetaka pia Katiba iweze kufikiria jambo kama hili, haki za watoto kutoka kwa wazazi kabla ya mauti yao ama katika mali ambayo wao wanayo. Katika umri ambao mtu yule anasemekana amekuwa ama, kuwekewa ukosefu wa uhuru wa kuuza vitu vyake lakini kuwekwe mipaka na uhuru wa kujiendeleza.

Jambo lingine ni kuhusu university faculties, nafikiri kwanza tumenyimwa hapa Pwani hatuna university hata moja, hata branch ya university nafikiri hatuna. And I think Kenya is actually achieving most in Coast ambayo ingekuwa tuwekwe sasa sawa kama watu wengine katika sehemu ya nchi hii. Imekuwa tunatoa watoto ambao wanasoma vizuri, wanaenda university lakini katika faculty zile ambazo wao walikuwa wamepita pengine mtu amepita na nafasi nzuri ya maths. Lakini ukiangalia mtoto huyu ametoka kabila ndogo ni kwa sababu mara nyingi uhuru hatuna, uhuru uko na Kenya na Kenya inasemekana iko Nairobi. Sasa watoto kama hawa ambao wamesoma vizuru mtu amepita pengine na faculty ya maths pengine aende asome computer ya maths mtu yule hapewi anaangaliwa aah, huyu ametoka sehemu ya kabila ndogo yule. Kwa vile pale juu kuna mtu mkubwa sijui ni nani, sijui ni nani atapatiwa faculty mtoto anahitaji ambayo pengine ni fake.

Pendekezo langu kuwekwe review ambayo itatoka from district, watoto hawa watakusanywa sellection ifanywe na wapatiwe allocation zao wakiwa hapa kuliko ifike kule watu wakose uhuru maanake pengine mmoja ni Owira, mwingine ni Wafula. So right ya kuwa mtoto yule pengine apate itakuwa ni ngumu, lakini majibu yakitoka watoto wale wapatiwe haki zao wakiwa kwao ili mtu akienda aende akijua yeye ni nani.

La mwisho ni kuhusu security, nafikiri security hapa nitazungumza kuhusu polisi vile wanavyokuwa na harassment kwa wananchi wa kawaida na maoni yangu ni kuwa…nafikiri jambo lile limeweza kuzungumzwa na ndugu fulani ambapo wamesema kuwa polisi wanaonea mtu yule, yule na yule na hii si uongo ni kweli. Siyo riba, sio kuonyesha kwa njia moja ama nyingine. Kwa hivyo mimi ningeomba review hii iweke open sheria za Kenya, elementary studies za security this is to improve relations between wananchi and the police force, ambayo sheria hii pengine sasa itamaanisha mimi kujua haki yangu ni nini. Askari anapokuja hawezi kunishika pengine mpaka awe na warranty. Sasa yeye atakuja atakushika na kuweka mbao, anaenda kukuweka mahali ambapo kwa hakika haki kama hizi sisi hatujaziona. Nafikiri ndugu kwa hayo machache wenzangu pia watazidi kuongeza.

**Mohammed Budzo:** …(Inaudible)

**Speaker:** Wengine wameiingilia sasa kabla haijafika …..

**Cllr. Chirupi Sirisiri:** Bwana Commissioner na wenzangu wote waliofika mahali hapa, Salaam Aleykum.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Cllr. Chirupi Sirisiri:** Mimi kwa majina naitwa Chirupi Sirisiri nikiwa diwani wa Kikoni na Zombo Locations. Maoni yangu yanasimama juu ya Serikali za wilaya. Nikiwa kama diwani kuna mambo mengi katika sheria hizi za Local Government Act, Cap 265 ambazo kwa kweli zilikuwa zinatuumiza sisi kama madiwani au kama baraza. Kwa mfano kuko na vipengele vinavyotupatia uwezo sisi kama baraza kwa maswala fulani kwa mfano uwajiri. Kifungu kinatupeleka mpaka mahali fulani kinasema, scale fulani sisi kama baraza hatuwezi kuajiri na sisi ndio watu tutakaowalipa mishahara wale watu ambao wanaajiriwa katika mabaraza yetu. Ninaona nafasi hizi ilikuwa ni ufundi ambao nafasi hizo ziende juu ili zipate watu wa huko badala ya kuletwa hapa kwetu na kuweza vijana wetu ambao wana uwezo wa kuweza kufanya kazi hizo.

Kwa upande huo huo wa Local Authorities, nazungumzia upande wa resources. Sisi kama Local Authorities kwa mfano Local Authority ya Kwale. Katika Kenya nzima tourism industry hapa kwetu Coast Province ama Kwale tuko na mali nyingi sana lakini sisi kama baraza hakuna kitu hata sumuni tunapata pale. Ukiangalia kwa mfano wale wataalii wote wanaoingia nchini pale, tumejaribu kwa njia nyingi tuone kwamba labda tunaweza kupata at least share yoyote ya bed occupancy pale chini ili baraza liweze kujinufaisha na liweze kutoa huduma sawa sawa kabisa kwa mwananchi. Lakini utakuta kwamba pesa zote zinazotoka hapa kwa mgeni kuingia, kwa mgeni malazi, kwa mgeni chakula pesa zote zinaenda Central Government, ambapo sisi kama Baraza la Wilaya ya Kwale tunashindwa na rendering services za kisawa sawa kwa mwananchi wa Wilya ya Kwale kwa sababu pesa zetu zote zinaenda pande hiyo.

Nikirudi upande wa hiyo hiyo resources ninakuja upande wa national parks, sehemu hizi za wanyama wa pori. Tuko na sehemu nyingi ambazo tunajua sisi kama Baraza la Wilaya ya Kwale tungekuwa tunaweza kujipatia mapato ya hali ya juu. Kwa mfano, tuko na sehemu ya hapa Simba Hills National Park. Mzungu kuona mnyama mmoja analipa zaidi ya…sijuhi ni pesa ngapi hata sielewi, lakini utakuta ile pesa ya mnyama inayoenda kule na hiyo ardhi ni Wilaya ya Kwale na wananchi wa Kwale ndio sehemu yao. Hakuna chochote kinaweza kupatikana kwa mwananchi wa kawaida wa Wilaya ya Kwale ambayo ndio yeye amelinda misitu kule mpaka mnyama yule amekuja amepata hifadhi mahali pale.

Kwa hivyo kutokana na hapo kwa maoni yangu nitarudi niseme Waziri wa Serikali za Wilaya hastahili kuwa na uwezo mwingi namna hiyo, kwa sababu kama ni mapato yanatoka kwetu, malipo ni sisi tunaostaili kukaa na kujua kwamba ni nani anastahili kupata nini kuliko Waziri. Kwa mfano, tunapitisha mapendekezo yetu katika baraza, tunatuma juu kwa Minister wa Local Government na anaandika barua kwamba nimekataa maoni yenu na sisi wenyewe kama Madiwani ndio waakilishi wa wananchi hawa ambao wametutuma katika baraza hilo kuwawakilisha. Lakini baadaye tunapotuma barua mbele kule inarudi kwamba rejected, ambapo ni kitu kwamba imekataliwa na sisi wenyewe tumekaa, tumeonelea ni umuhimu tuwe na kitu kama hicho ili tuweze kujiendeleza. Kwa mfano, kuna vitu kama barabara mbovu ambazo sasa hivi tungekuwa na hali kama hiyo ama tunaruhusa ama kisheria tumepata nafasi hiyo, tungekuwa na vitu kama ma-grader hapa ambayo yangetusaidia. Kwa sababu tungenunua kutokana na kile tunapata kwa tourism industry na kuweza kusaidia wananchi wetu.

Hapo hapo pia imetusukuma mpaka imebidi mwananchi wa kawaida anayeuza maembe inastahili akate licence, kwa sababu hakuna njia zingine za mapato. Tunatafuta vinjia vidogo hata mwananchi wa chini ambaye anauza vitu sumuni sumuni ati akate licence ni kama kumwonea. So, Waziri wa Serikali za Wilaya apunguziwe mamlaka ya kuamua ama apunguziwe mamlaka ya kufanya mabaraza yasiweze kupitisha mambo yao ya kuweza kusaidia wananchi wa sehemu hizo wanazotoka.

Ya pili, ningependa kuchangia hapa kwa mfano ile Katiba ya zamani section 82 kama sijasahau of the Constitution of Kenya ambayo inasema una uhuru wa kutoa maoni, una uhuru wa kukusanyika mahali pamoja, kuna uhuru wa kuabudu. Nikifikia mahali hapo kulingana na ilivyosema Katiba ya zamani kwamba kuna uhuru wa watu kuungana pamoja. Ni kweli kabisa watu waungane lakini kama ilikuwa kuna uhuru wa watu kuungana pamoja na kuna uhuru wa mtu kutoa maoni yake jinsi anavyojisikia mbona mtu akitamka na mwenzake barabarani pale anashikwa? Au mbona watu fulani wakikaa pamoja wanaambiwa mpaka mchukue permit ndio muwe mukae pamoja? Sasa huu uhuru wa kukaa pamoja pale naona haujatimia kivile mimi nafikiria kwa maoni yangu. So, kulingana na maoni yangu labda ningependelea nisema kama kwa mfano kuna uhuru wa kutoa maoni kusiwe na vikwazo fulani, kwa sababu tayari imeelezeka katika Katiba ya zamani na hivyo ni sawa na kusema, ikiwa kuna uhuru huo uwe ni uhuru wa kisawa sawa bora usidhuru uhuru wa mwingine kulingana na vile ninavyoona kwa maoni yangu.

Mwisho, labda nikirudi kwa Katiba ile ambayo sasa hivi tunarekebisha hapa mimi maoni yangu. Katiba ile ya zamani ambayo iliundwa kwa wakati ule, sijui tulifanyiwa madhambi aina gani kwa sababu mimi kama Diwani kuna vipengele fulani sivijui, je

mwananchi nitamjulisha vipi? Sasa mimi katika maoni yangu nafikiria hata kwa watu wa nyuma waliwahi kuchangia kwamba, wakati mambo fulani yanatengenezwa ya muhimu ya kumsaidia mwananchi huku kwa mwananchi wa kawaida haitakikani ajue. Kuna vitu fulani vinazuilika ambavyo ndivyo pingamizi inafanya mwananchi huyu wa kawaida bado anazidi kurudi nyuma, anadidimia, na wale watu waliounda hicho kijisehemu na wakakataa kufikisha huku kwa mwananchi wa kawaida. Walikuwa wanafanya hivyo kwa manufaa yao ya kibinafsi.

Kwa hivyo, kwa sababu hiki ni chombo kimoja muhimu sana itazidiwa nguvu labda na wenzangu wengi Wakenya ambao watasema tuingie kwa uchaguzi na Katiba mpya. Lakini ki maoni yangu sitosheki na huo muda wa kuwa sisi Wakenya tukae na tuisome na tuielewe na tuitumie tujue kweli haki zetu zote zimelindwa. Mimi maoni yangu, labda ningesema tuingie uchaguzi na Katiba ya zamani ili hii…..ni maoni yangu. Wewe umetoa maoni yako wacha mimi nitoa maoni yangu.

**Speaker:** Sawa.

**Cllr. Chirupi Sirisiri:** Na ninasema hivyo kwa sababu kila mtu anatoa maneno yake na ndio mimi maoni yangu nimefikia mahali pale. Kwa hayo machache nasema asante.
***(Murmur in the background)***

**Athumani Riziki Kassim:** Asaalam Aleykum.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Athumani Riziki Kassim:** Kwa jina naitwa Athumani Riziki Kassim.

**Mohammed Budzo:** Ngoja ngoja.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Hii ndio ile tumesema hapa hapa hata tukiyapitisha tunaanza kuikeuka. Hiyo hiyo misingi ambayo tumesema hii ni mzuri, sasa tunaanza kiikeuka, tumesema kuna uhuru. Yule Bwana amekuja kuchelewa lakini Katiba hapa tumesema kuna uhuru wa kujieleza, kuna uhuru wa kuzungumza.

**Speaker:** Wale wamechelewa pia hao.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Sasa ikiwa…hatukuja hapa kusema kwamba maneno yote tunayozungumza lazima watu wote wawe wamekubali, huwezi kuridhisha binadamu wote dunia hii. Kwa hivyo, ikiwa kuna mwenzetu amesema wazo ambalo hatulipendi haki yetu iko vile vile, yeye ana haki yake ya kujieleza. Haki yetu ni kusema no, vile alivyosema sivyo kwa sababu ya a, b, c, d lakini sasa kisheria ya sasa Katiba yetu tunayoizungumzia haitaki aseme halafu usema no, haitawezekana

hivyo, hapana sheria ya hapa imekataza sasa. Aseme mpaka amalize, ooh, umesema hivyo, haya ngoja hasa tukufuate sasa, unaanza kumchambua moja kwa moja. Sasa mtu akisema maoni ambayo kwa wengi hayawapendezi pia mpatieni nafasi ndio demokrasia tulikuwa tukipigania hiyo, sio kwamba kama linapinga unazuiliwa usiseme. Kama linaudhi unazuiliwa au unafungwa, sasa ni kama tunamfunga sasa, haitakikani mwacheni aseme akimaliza wewe mtu wa kwanza kuinua mkono yule ambaye anampinga naye ainue mkono. Aseme msemaji alivyosema hivyo sioni ni sawa mimi ninapendelea kadha wa kadha sasa itakuwa imepindika hapo. Lakini kumuingilia na kelele hivyo tutarudi pale pale pa zamani.

Haya, endelea Bwana rudia jina.

**Athumani Riziki Kassim:** Kwa jina naitwa Athumani Riziki Kassim, mimi raia wa kawaida nikitetea haki yangu. Kwanza nashukuru Tume ya Katiba ilipokuja mara ya kwanza tulitoa mchango watu na ijapokuwa hatujasoma zaidi kuhusu hivo vitabu na hayo magazeti lakini sehemu fulani tumepitia ndani yake tumeridhika nayo wengineo. Na ningeomba wenzangu mliopewa hivyo vitabu na hayo magazetti msiyaweke kama picha myasome kwa utaratibu na kwa makini sana. Yana mambo mazito ambao huyamalizi leo wala kesho wala kesho kutwa na ni mambo ambao ni ya kuridhisha. Mambo yale tulioyataka mbeleni ndio yale yaliomo ndani isipokuwa kuna kitu kidogo ningetaka kujulisha Tume. Bwana Mwenyekiti, ningependa utafahamishe ama unifahamishe kumetajwa nyumba mbili, Upper House na Lower House. Je, nyumba mbili hizi zitakuwa sehemu gani?

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Pahali zitakapokaa?

**Athumani Kassim:** Zitakapokaa. Zikiwa zitapendekezwa, ikiwa moja itakuwa bara, ikiwa Upper House itakuwa bara, ile Lower House ije Pwani. Tungeomba hilo swali liwe hivyo.

Kitu kingine ni kuhusu ndugu yetu aliyesema tufanye uchaguzi na Katiba ile iliyoko mbovu. Hiyo Katiba hiyo sisi Wakenya ningewaomba tusiikubali maanake Katiba hiyo ni ya u-dictator yaani uimla na imeshika watu koo hivi sasa. Ndio kuna wengineo hatuwezi kuwataja mpaka sasa wanahara kwa hiyo Katiba hiyo. Kwa hivyo, kitu ningewaomba wananchi tupigeni kura kwa Katiba mpya na tui-support hii Katiba mpya. Someni hilo gazeti vizuri na hicho kitabu mtaona utamu ulio ndani yake. Shida tulizokuwa nazo inshala zitaondoka na mambo yatakuwa mazuri na watoto wetu ziku zijazo watafaidika kile kile tulichokililia.

Tumedhulumiwa kielimu, tumedhulumiwa kinjia nyingi, ki ufundi, ki mambo ya agriculture, mpaka leo niambieni katika Pwani matingatinga yale ambayo yanalimia raia raia wanakodesha ni mangapi? Mshapewa mbegu na Serikali ya kupanda, zile dawa za mimea, maofisa wa agriculture wako wapi? Hakuna, kulikuwa na vidimbwi vya kuoshea wanyama vimekufa vyote hata kimoja hakuna kwa sababu ya nini? Ya u-dictator, tembeeni muangalie huku bara, yule ambaye hajakwenda aende akatembee aangalie, Kericho, aende aangalie sehemu za Baringo aende aangalie. Tembeeni huko mwone, kuna mijitinga tinga linatokezea hapo utafikiri ni hiki farm ni cha Muisraeli, ni tinga tinga la kulima hilo. Miwa iko huko Nyando, huko Sony Sugar, huko

Mumias ni ardhi mbovu mpaka ulime na jembe ambalo linauma lile. Kwani miwa zilikuwa zinamea mpaka Shamu, leo ile ardhi imekwenda wapi?

**Speaker:** Ipo.

**Athumani Kassim:** Leo ile ardhi imekwenda wapi? Ama tukipanda miwa haimei. Vukeni ile barabara tunamashina ya miwa pale hapo mtaani kwetu hapo, ile ni midude gani ile, ni upupu? Kwa hivyo, tusikubali wananchi tupigeni kura kwa Katiba mpya, tusikubali swala la kuambiwa ati tungoje ile Katiba ya zamani tupige kura. Mkipiga kura na ile Katiba ya zamani hii Katiba imekufa, na mamilioni ya pesa imepotea na ni pesa zenu nyinyi raia. Msidanganywe kabisa.

**Speaker: Interjection.**

**Athumani Kassim:** Walahuakbhar. Msidanganywe kabisa.

Swala lingine Bwana Mwenyekiti ningekuambia hivi Bwana, tuliomba Kurani itolewe ndani ya Mahakama hatujuhi imetolewa au bado? Kitu kingine ni kuinamia hawa wanaojiita Mabwana, unaingia mahakamani umuinamie mtu hivi ama yeye ni boss ama yeye ni offisa wa ngazi za juu umuinamie ndio uingie ofisi yake. Hilo swala liondolewe, hiyo sio haki ya ubinadamu hiyo kuinamiana. Mwenyezi Mungu peke yake tumuinamie ndivyo tunavyotaka sisi, tunaomba hivyo Bwana.

Na swala la elimu Bwana, elimu tung'ang'anie sana sisi hasa hawa wa Pwani tumelaliwa sana hata chuo kikuu, hata chuo cha ufundi hatuna. Mombasa Polytechnic ukienda huwezi kuchukuliwa mpaka elfu arubaini na tano, hiyo sasa ni ya ku-register hiyo. Je, hizo zingine utatoa wapi? Kwa hayo machache nasema shukrani.

**Henry Adongo:** Asanteni sana. Kwanza ninaitwa Henry Adongo mimi ni mzaliwa hapa Pwani kwa huo muda huo wote na huu umri nilionao. Sana kwanza nawaambia wadungu sana wananchi, tunapoongea tuongee kwa upande wa watu, Wakenya wote, raia wa Kenya tusiongee kwa kitongoji. Usije ukawa na ubinafsi ukaongea katika kijiji hapana, tuongee kwa hii sheria ni msumeno inakata ikienda mbele ikirudi nyuma. Hilo kwanza nawasihi wananchi. Kwa hivyo natengeza kitu ambapo kitaongoza kitukuu na kilembwe na kilembwakeza wakati wewe hauko duniani. Kwa hivyo usione unazungumza leo kesho ikashika mjukuu wako. Asante.

Tunaendelea, nakubali moja kwa moja na hiyo Katiba lakini sikitiko ni kwamba ukizungumzia kila ambacho ukijui ni hatari kubwa, waweza kuzungumza kipengele fulani ambapo huwezi na kuifafanua hiyo tayari ni kosa. Ningeuliza kama vile Mwenyekiti amejaribu kutangulia kutuambia, kama vitakuwa vinaeleweka katika vijiji tutakuwa wananchi wanaokuja nyuma zetu watanufaika. Ni uwe unajua kile ambacho kinafanyika, kwa hivi sasa mwananchi wa kawaida hajui haki yake.

Mimi ningependa kitu kimoja, kama Katiba inaweza kupendekeza sura inayowekwa kwa pesa iwe ni mwanzilishi wa taifa peke yake. Tusije tukawa kila atakayekuja miaka mitano sura inatoka fulani, hatutakuwa tunajua tunafanya nini. Kwa hivyo pendekezo langu ni sura iwe ni hayati Mzee Jomo Kenyatta mwanzilishi wa taifa mpaka mwisho wa Kenya. Tunazungumzia ardhi, mambo ya ardhi hili swala linasumbua Kenya nzima lakini kuna ufafanuzi fulani. Yule anayekuja kuuza ardhi, ana sababu gani ya kuuza ile ardhi, ilo ni swali? Je, wakati wewe umekuta ile ardhi pale waiuza na wewe umezaa watoto wako watakaa wapi?

Kwa hivyo ningependekeza kama hiyo tume ingejizungumzia hiyo tungetazama kiurefu yule ambaye anataka kuuza ardhi ana sababu gani na kama kuna uwezekano awe na sababu mbili, tatu, nne tano sita na aeleze kinaga ubaga ili aweze kujua kwa nini anauza. Nasema hivyo kwa sababu yule anayenunua ardhi kwako yeye ana madhumuni fulani, ana dhamira baada ya miezi miwili mitatu amejenga nyumba watu wanapangisha. Wewe ambaye umeuza ardhi na pesa zako umeziweka ukila mandazi na mahamri na mbaazi, zikiisha unaona kijicho, unageri. Afadhali hata bombo ingerudi huyu Bwana akatimuliwa akarudi kwao akapata ile nyumba. Ninapozidi kuendelea miaka zinaenda, ile thamani alionunua mwaka huu sio thamani ya miaka miwili mitatu ijayo, tayari utakuta alikudhulumu kwa sababu mtoto wako alikuwa hukumshauri yeye alikuwa hana namna. Wewe unauza ardhi je babu yako angeuza, baba yako angepata? Babu yako angeuza hiyo ardhi, baba yako angepata? Hangeipata kwa sababu tulinde ardhi hii, tatanishi imalizike katika nchi yetu na vitukuu vinavyokuja.

Tunakuja kwa upande wa uajiri, tunakuta ya kwamba mara nyingi Mkenya halisi hapewi haki ya kuajiriwa. Mtu akiwa ni mweupe bora aonekane Mzungu anapatiwa wadhifa anaajiriwa na pesa nyingi ambapo hizo pesa angeajiri watu sita ama watu kumi Mkenya halisi lakini kwa kuwa ni ile ya rangi anapewa pesa nyingi, anapewa gari, anapewa nyumba na mfanyikazi, self-contained wanasema kwa Kiingereza. Ni kwa sababu gani? Yeye ni Mzungu na kumbe kule kwao yeye ni chokora, sisi hatujuhi. Tumempa wadhifa kwa sababu Kenya huwezi kuzungumza, ukizungumza haki tayari ni makosa. Niliona mfano moja pale ferry, kumewekwa kizuizi, Mzungu anapita na Mwaafrika anashikwa tyres za nyuma Mzungu anaingia ndani ya ferry. Mimi ilibidi ni-act kama maofisa wakiniuliza nawaambia twende, kama haki ni hii itendeke kwa binadamu. Kwa hivyo, hiyo Tume ichunguze mambo ya uajiri, kuajiri mgeni achukue elfu ngapi na Wakenya wanapata taabu mimi kwangu si haki.

Tunaenda kwa point ya pili ama swali lingine la malipo ya uzeeni. Malipo ya uzeeni unakuta mtu amezeeka, ame-retire bado anamaliza miaka mingapi ati ndipo anafuatilia. Maoni yangu ningesema kama ni malipo ya uzeeni iletwe katika kila mkoa si kwamba iende Nairobi, wengine wanatatizika wakifika kule majumba marefu hata hajui ameanzia wapi na anamalizia wapi. Hajafika kule unaambiwa mpaka uende Nairobi utafute mambo ya malipo yako, kwa nini tusiwe na malipo kwa kila mkoa? Kama kuna uwezekano ume-retire hapa nenda pale Kwale utazame marupurupu zako ulipwe mambo yaishe, si mpaka ufe uwaachie wao watumie, hilo ni kosa kulingana na mimi. Kwa hivyo tunaendelea.

Nikimalizia, tunazungumza kwa upande ya haki na hali ya watoto kwa upande wa jamii. Tumekuta chokora wanakuwa wengi, tusidanganyike ni sisi wazazi ndio tunafanya hayo. Kwa hivyo Tume itizame sheria ngumu sana ambaye atapatikana na msichana

ambaye hajaolewa au hajakubalika kindoa, mvulana ambaye anafanya mapenzi kiholela achukuliwe hatua kali tupunguze mambo ya chokora. Unakuta sisi tuko hapa mimi nina mwanamke nachukua mwanamke mwingine namweka kimanda huko nje namzalisha siwezi kumlea, huku nabania. Yule mtoto hawezi kulelewa na mzazi mmoja tayari anaanza kuwa chokora, imeleta mpaka tunafanya dhambi ya kuua kwa sababu msichana ameshika mimba hajafika umri, hajajua uzazi ni nini. Tayari leo ameshapashwa mimba anaenda kutoa ile mimba, either afe ama mtoto afe.

Sheria itolewe ngumu kama kuna uwezekano, ukipatikana umetoa mimba yule aliyehusika maanake mtu hawezi ku…hata ng' ombe wa gradi mpaka apate mwenziwe. Huyu msichana aweze kupata kuulizwa, hii mimba umetoa wapi? Zamani nilikuwa nikiona hapa kuwa ukishikwa na mtoto wa mtu analozwa, get me right. Yaani tayari anapewa jukumu, responsibility lakini wakati huu mtoto yeye mwenyewe……(Inaudible) la yule mamake anazifinika hana jiko, hana nini, anatongoza huku mkajuni. Mara amepeana mtoto wa mwenyewe mimba, mara unakuta amejaribu kum-confuse babake akapatiwa pesa akampa yule mtoto. Mtoto naye anaenda kutoa mtoto, anatoa mimba, what is this? Haya mambo yachunguzwe kikatiba tuweze kuwa ukipatikana nje ya ndoa kama wewe una mwanamke halafu uweze kufanya mwanamke mapenzi huko huwezi kulelea korti inaweza kuamua ni kitu gani unaweza kupewa. Asante sana mimi namalizia hapo wengine watachangia. Asanteni sana.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Haya, asante sana wale ambao wamechangia. Yale maswala mengi ambayo yame…

**(Interjection)**
**Speaker:** …(Inaudible)

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Nimeshaandika kumi mimi nani mwingini, huyu ni wa kumi. Zimefika kumi mwengine ni nani huyu Bwana.

**Mohammed Budzo:** Wamefika kumi huyu Bwana amechukua tisa, huyu Bwana akachukua kumi.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Haya basi nachukue kumi na moja huyu.

**Kassim Halifan:** Mimi nasema maneno kidogo tu.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Sema jina.

**Kassim Halifan:** Naitwa Kassim Halifan.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Mbona unaweka mbali sasa?

**Kassim Halifan:** Naitwa Kassim Halifan Momanga. Onyo langu mimi nasema katika dunia, nchi yetu ya hapa Pwani iko kitu kimoja tu umaskini na njaa nyingi. Na kitu hicho kinaletwa na rasilimali, rasilimali zetu za hapa ni mnazi na mkorosho. Vitu hivi vimekuwa na short ya fulani ya kwamba wako wengine wamesoma, wengine kama sisi hatukusoma yetu ni kupanda mimea hiyo. Sasa mimea ile haina bei yoyote, mnazi, vitu vyote vinapandishwa bei lakini mnazi hauna kazi na mnazi ndicho kitu cha hapa na kimeleta umaskini. Hata mtoto ukienda kazini ukapata malaki matatu lakini ukija hapa mnazi wako hauna bei utakula mali yako utamaliza na utakufa maskini. Kilio changu nasema mnazi uwe na bei ya kwamba mnazi hauendi kokote, soko ya mnazi uwe mnazi unapanda bei uwe usitiri wazee hapa.

Nazi zenyewe Bwana, basi hapo ni kitu kimoja. Vyakula vimepanda zaidi wako watu wazee wengi katika nje watu wanaumia. Sasa vyakula watu wakipanda, watu wengi ambao wanapandishwa mishahara yeye anapata pesa lakini watu wengi ambao hawana kazi, hawana nini na mwaka umebadilika huu vyakula viko juu zaidi. Sasa tajiri yeye ananunua samaki, tajari ananunu bei ya maskini na maskini hana chochote yeye anataka kununua nyama kilo moja shilingi mia moja na thelathini na tano, maskini hana chochote. Watu wengi hivi sasa Wadigo wengi watu wanakufa na njaa, ukimwona hana nuru yoyote lakini ni njaa tupu tu ile hana pesa na chakula. Haya, yangu ni hayo tu.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Nafikiri tukiyaangalia yale maswala yote au mengi ambayo yametajwa yanaweza kujibiwa kwa urahisi ikiwa tutasoma kile Katiba kinachosema. Hayo maswala mengi hayo yanayosemwa ya mnazi, korosho pia chakula, waajiriwa wa kazi, rasilmali, yote majibu yake yako katika Serikali ya jimbo na Serikali ya wilaya. Ukiangalia pale yote yametiwa pale ndani, kuajiri kwa kazi, kuajiri kwa polisi pia polisi wameandikwa pale. Uwaajiri wa polisi, uwajiri wa maofisa wa kufanya kazi ni kazi ya district sasa, si kazi ya kikosi kitoke Nairobi kije kuwazungushe mbio hapa halafu kichukue mtu mmoja, hapana. Sasa imeandikwa hapa section 8 (a), imeandikwa kabisa hiyo ni district sasa ndio itafanya kazi hii. Kuandikwa, kujua kwamba bei ya mnazi wetu utakuwa na thamani gani, nazi zitafanyiwa research namna gani, korosho zitafanyiwa research namna gani. Viwanda vya korosho sasa si kazi ya Serikali ya Kenya hiyo tena. Wale wale mtakaowachagua katika district na province ndio jukumu lao, limeandikwa kabisa, wazi kabisa wao ndio wanamajukumu hayo tena. Ndio tukasema kwamba vile mlivyotaka kwamba mjiamulie mambo yenu, sasa imekuwa ni hivyo hivyo hakuna haja tena kulaumu tena kule juu ikiwa Katiba hii itapitishwa. Hizo jukumu zote ni za Serikali za hapa chini.

Kwa mfano umesema habari ya bars, Bwana Mwakuyumba ameeleza habari ya bar ni nyingi hapa Ukunda. Sasa tumesema Serikali ya location na Serikali ya wilaya ndizo zitakaa chini, physical planning ni kazi yao. Physical planning maanake ni kupanga vitu vilingane na watu wako wangapi. Fiscal planning kwa mfano itasema ikiwa pana Misikiti pale huwezi kuwa na Misikiti hapo, ikiwa watu ni hawa hamsini kwa nini ujenge misikiti mitatu pale pa watu hamsini. Sasa Serikali ndio itasema hayo au Makanisa moja liko pale jingine liko pale, Musikiti uko kati kati, Fiscal planning na sheria imesema kwamba vitu ambavyo haviwasiliani haziwezi kuwekwa pamoja.

Ni kama kuwa na bar katikati ya shule, Fiscal planning hiyo inakataa hapa hatuwezi kuruhusu mtu kuja kuweka bar pale

kiwanjani na shule iko pale, sheria inakataza. Wenye jukumu la kufanya hayo, kutekeleza hayo si Serikali ya juu, ile Serikali ya tarafa, serikala ya district. Sasa si jukumu tena la Fiscal Planner atoke Nairobe aje aseme wewe jenga bar hapa au licence itolewe kutoka huko nje iletwa hapa. Wale wamepewa jukumu ya kuweka kamati zao za maendeleo, kila kitu kimeandikwa pale wakae chini waseme hapa nafikiri tunataka shule hapa. Wafanye estimate, wafanye hizo research waseme kweli ile shule iko mbali tuwekeni hapa na tukiweka moja hapa kule kuna watu wengi zaidi tutaweka hapo.

Ni wao sasa. Hakuna mtu kutoka juu atakuja kuingia aseme mbona mmejenga shule nyingi, mbona mmeweka hivi? Hapana, kwa sababu Katiba ndio sheria kuu imesema shule watu wapate lakini kwa mpango. Kwa hivyo mambo ya ma-bar kuwa ni mengi, mambo ya ma-disco kuwa ni mengi, mambo ya video zinafanywa mchana au usiku sasa hilo limetoka jukumu hilo kule. Mujue hivyo, limetoka jukumu msilauma kwamba wale wanatuletea, aah, Katiba hii ikipitishwa ni nyinyi wenyewe, ile Serikali utachagua ya kijiji itakuwa na jukumu la kusema, Serikali ya location itakuwa na jukumu la kusema, Serikali ya district itakuwa na jukumu la kusema, Serikali ya jimbo itakuwa ina-control mambo yote hayo. Tumeelewana hapo?

Itakuwa ni gharama kwa sababu kutakuwa na Wajumbe ni kweli lakini tulisema kwamba democrasy dunia nzima iko hai sasa. Democracy ni kitu ambacho kimejulikana kiko na ukitaka kuwapa watu haki zao wahusike katika mambo yao basi lazima hapo panatokea peza nyingi sasa. Hiyo imekubalika, wewe angalia nchi kama Japan, nchi kama India, nchi kama Italy wale uchaguzi ni kila mwaka maanake Waziru Mkuu akionekana hafai hakuna kungojea tena, uchaguzi chap chap upesi. Nchi kama Israel kama Waisraeli mia mbili wakiuwawa na Wapelestina ingawa halijatokea hilo Waziri Mkuu hafai, kura tayari anachaguliwa ambaye anaweza kuokoa Wapalestina mara moja, ni gharama. Kwa hivyo tumekubali kufanya demokrasia kwa wananchi. Kama hamtaki mtu mmoja afanye na mishahara wake ni milioni moja mwataka watu mia tano wafanye na kila mmoja ni laki mbili hizo nyingi zaidi kuliko milioni moja.

Sasa tumesema habari ya mtu mmoja kuamua tumekataa, mishahara yake ilikuwa ni milioni moja, sasa zote tuhusike hata kama ni shilingi ishirini ishirini zitakuwa nyinyi. Kwa hivyo tusikatae gharama kwa sababu tu tunasema kwamba itakuwa ni hali na wananchi wenyewe wamezaa. Sasa wao wenyewe wananchi waangalie eeh, halafu waseme jamani tiliyataka lakini weh! Haya magumu, sasa mtayabadilisha wenyewe Katiba tena lakini kwa sasa vile mlivyotaka ni hivyo, lazima kupatikane pesa na tumepatia Serikali ya Wilaya, ya Location, na ya Jimbo kutuma pesa. Wao ndio wataenda kwa ile Tume ya mishahara itasema kila Mbunge wa kijiji atalipwa elfu hamsini, kila Mbunge wa wilaya atalipwa elfu sitini, kila Mbunge wa Mkoa atalipwa elfu sabini, pesa zitapatikana kutokana na vile wanavyotoa zile kodi zoa, ni wao wenyewe.

Na umesema pia polisi watakuwa wengi, mahakama lakini si hiyo imeshaelezwa pale. Section 8 (a) na (b) ni jimbo litaandika polisi na kila mtu hao wenyewe kulingana na pesa zao walizonazo, wao wenyewe si Serikali tena. Na elimu pia ni hivyo hivyo mzee moja wa Chale akauliza wale Wabunge sabini wa Upper House. Tumesema wananchi, kila Wilaya watachagua mmoja hatukusema ni mwanamme au ni mwanamke tumesema watachagua mmoja maanake watatokea kama ishirini watupiganie sasa nyinyi wenyewa kama mwanamke atafaa, mama atafaa mtamchagua. Kama ni baba atafaa mtamchagua kati ya wale sabini,

Wabunge wa Kenya nzima wakiwa ni wanawake ni uwamuzi wa wananchi. Zile nafasi thelathini ziko vile vile za akina mama, ziko vile vile maanake tumesema kwamba akina mama huwa wananyanyaswa hawapewi nafasi na wao wengine wanaweza kuongoza sasa uhamuzi ni wenu.

Bwana Mwakulonda akaeleza habari ya chuo kwamba elimu ya chuo Kikuu na colleges pia ziwe under District Government. Hatukueleza hapo lakini tutaenda kwa kinaga naga. Mambo ya chuo kikuu cha Pwani yana historia ndefu sana, tuseme yana historia ya uchungu maanake mimi ni mmoja wa wale watu ambao wamejaribu kuanzisha chuo na nimekuwa kwenye kamati nne za chuo kikuu cha Pwani. Lakini ni mambo ambayo mimi naona utatuzi wake utatokea kwenye Serikali tu ya juu lakini hata hivyo sasa tutafanyaje sioni kwamba kuna uwezekano wowote kwa sasa. Tumejaribu kila njia hata kuanzisha kiji-college kidogo kiwe kimekuwa ni sehemu ya chuo kikuu cha wapi lakini bado kwa hivyo sasa jukumu limerudishwa tena kwa Serikali za mitaa.

Lease kwa foreigners, Bwana amesema kwamba ikiwa imefanyika kazi pale halafu kule mradi uwe umeshindikana kabla ya lease kuisha hiyo ile ardhi inarudi kwa wenyewe. Lakini wajua lease ni mkataba, Bwana Barua ameuliza pale, Barua yule mwingine. Ameuliza maana ya lease ni nini? Ni mkataba baina ya mwenye ardhi na ambaye anataka kutumia ile ardhi kwa muda fulani kwa pesa fulani, kwa masharti fulani na kila ardhi ikuchukuliwa kwa lease huwa mmeandikiana pale. Ardhi hii nachukua nitatumia kwa kulima au nitatumia kwa kujenga nyumba, au nitatumia kwa kufuga ng’ombe, huwa lazima katika ile lease agreement hizo zimeandikwa na huwa imeandikwa isipofanyikana vile utafanyika nini. Straight away, hiyo ndio lease maana yake nini, kwa hivyo ikiwa lease imeendelea ikifika katikati mambo yakaharibika ile lease agreement uwa inasema wazi Katiba kutafanyika nini. Lakini tunajua kwamba kama ni ardhi ya wananchi ile tunaita community land, ile trust land sasa ni yenu, kama ni lease ya ardhi hiyo, kama ni lease ya Serikali kila lease ikiisha sheria iko wazi, ardhi inarudi kwa mwenye ardhi. Kama ni Serikali 33 year lease ikiisha inarudi kwa Serikali, Serikali ina uwezo tena kukupatia nyingine au kumpatia mtu mwingine au kusema hakuna ardhi hiyo ni yetu tunatumia. Ardhi ya wananchi ni hivyo hivyo mkimpatia mtu lease ya miaka arubaine ikimalizika ile lease hana chake tena sasa nyinyi ndio mtaamua.

Halafu habari ya mashamba nimesema tu kwamba tutaangalia mikataba ya mashamba ya zamani ya Pwani na Rift Valley na sehemu nyingine halafu akauliza haikusema mtafanya nini baada ya hapo. Imeshasema pale, ukisema section 235 (b) (ii), imesema ikiwa kutapatikana kwamba watu walinyang’anywa ardhi zao kiholela bila si haki zitarudishwa kwa wenyewe. Imeandikwa hapo Bwana Mwakulonda sijuhi umesomea wapi? Umesomea wapi yako uliyosema lakini ukisoma hiyo yangu inakuonyesha imeeleza hapo wazi wazi kutafanyika nini. Umepitiliwa lakini imesema, ikipatikana kwamba ardhi ile imechukuliwa kimakosa hata kama ni miaka mia tatu, ardhi ile itarudishwa kwa wenyewe au watalipwa ridhaa, tumeandika hapo. Kwa mfano ardhi ile imechukuliwa imejengwa shule kama hivi hatuwezi kuvunja shule tukaondoa watoto, tutauliza wale wenyewe mnatakaje, hii tulichukua kwa makosa, mnatakaje. Lakini kuanzia sasa uwe huna lalamiko kwamba pale palikuwa mzee wetu lakini Bwana looh, wale jamaa walikuja wakatutoa, hapana hiyo ndio tumeandika.

National Conference Delegates wawe wanaeleza wananchi wanashauriana na wananchi kabla ya huo mkutano, mmoja wa hawa delegates wenu ndio huyu hapa mwengine yuko wapi, mwengine ndiye huyo. Hawa ni wawili wa wale delegates ambao walichaguliwa Kwale kwa hivyo hawa sasa kazi yao ni kukusanya maoni yenu sijuhi watakusanya namna gani, hayo sasa ni kazi yao sasa.

Suleiman zaidi …

**(Interjection)**

**Speaker:** …(Inaudible)

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Sasa ni yule Mbunge sasa, sio hawa.

**Speaker:** Sio hawa ni Mbunge sasa.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Oooh, nimeeleza kwamba Mbunge naye lazima hawezi kama mswada umeletwa Bunge na yeye hana uamuzi, mpaka arudi kwa wananchi wake. Huwezi kuwa kiongozi wa wananchi kulingana na Katiba hii, huwezi kuwa kiongozi wa wananchi ukawa unaamulia wao mambo yao, hakuna hiyo sasa. Ndio maana tukasema kama hafanyi mnavyotaka mnamtoa na kule kutofanya mnavyotaka ni kwamba amekaa kule akafikiria aah, wale wataka hivi mimi nitakwenda sema hivi. Mkishajua ni hivyo ooh, signature 30% anatolewa akiuliza ni nini. Juzi ulikwenda kusema maneno ambayo sisi hatukukuambia, pah, mbona hamkuniambia sema sheria imetupa ruhusa Bwana. Kama hufanyi tunavyotaka au hawafanyi ambavyo sivyo tunavyotaka basi automatically tunakutoa. Sasa hapa tumeweka kwamba lazima hawezi kuenda step yoyote mpaka arudi maanake atafikiria sasa nikienda hivi, labda nikifanya hivi…(vernacular) Sasa mpaka kila stage anayefanya arudi, wakati huu tunalalamika kwamba viongozi wanafanya mambo tu wanakaa wanafikiria, hawaambii, hawatapiga kelele siku ingine. Mtanyamaza utafanya nini, kazi yaendelea, sasa tumesema sio hivyo wakifanya hivyo nje.

Je leaseholder, yule ambaye amechukua lease anaweza kuuza? Mkataba hausemi huwezi kuchukua lease ya mtu halafu ardhi ukaiuza na wewe bado uko katika nchi haiwezekani. Salim Ali, Salaries Commisison tumesema kwamba wale wafanya kazi aina yoyote ile wana haki ya kupata mishahara inayotakikana. Angalia labour relations tumeandika hiyo kwa hivyo si wale wafanya kazi wa Serikali hata wale vibarua pia tumeandika. Lakini tujue kwamba tulisema siku ile ya kuchukua maoni kwamba kuna maneno mtayasema mtayaona katika Katiba, kuna mengine mtayasema tutayaandika ile sheria zibadilishwe tumeelewana hapo? Kuna maswala ambayo lazima yatokeee na yameshatokea kwenye

Katiba tunaiita broad principle halafu kuna zile jipya ambazo mnasema vile tuliziandika lakini tutazipeleka katika sheria fulani. Baada ya hii Katiba yetu kule nyuma tumeandika transitional mechanisms, tutaandika hapa watu walisema kwamba mishahara

ya wazee lazima iongezeke wakati mishahara ya wafanyakazi inapanda, sheria hiyo ni gani. Retirement benefits Act iko wapi tutawaambia rekebisheni hiyo maanake hii Katiba imesema watu wawe sasa, hivyo vitu ambavyo tunafikiria kufanya. Kwa hivyo haya mambo mengine mnayoyasema haya hayawezi mengi hayo yote, tuliseme tukiandika kila kitu basi hili litakuwa jitabu namna hii halafu mtaanza kusema nyinyi wenyewe kwamba mbona kubwa sana hii Katiba, huwezi kutia mfukoni pia. Sasa tumegawanya mara mbili, yale ambayo yanaweza kuonekane ambayo ukiyafuata hayo utakuwa umemaliza tutayaweka, yale ya undani sasa, kuna sheria ambazo lazima tutazibadilisha. Kwa mfano upande wa urithi Bwana amesema kwamba mzazi aliyeko hai aweze kumrithisha mtoto wake, hiyo tumesema ni sawa lakinu tumeachia dini na mila hatutaki kuingilia huku kuaribu dini za watu wala mila za watu. Kama kwenu mwarithiana bado ungelimzima fanyani hivyo, ikiwa lazima ufe kwanza ndio urithiwe fanyeni hivyo.

Halafu upande wa chuo kikuu nimeeleza. Swala lingine ni la Bwana Councillor aliyeleta zogo kwa kusema kwamba anataka uchaguzi usifanyike kwa Katiba ya zamani, hata mimi nilikuwa nimeeleza pale mwanzo. Nafikiri ametoa maoni yake kisawa kabisa, mimi nimeeleza hata sisi Tume tunaona haina haja kufanya kazi hii yote halafu Katiba tuiweke kando tufanye uchaguzi na Katiba ya sasa. Tumeshayasema mapendeleo yetu ni kwamba tunataka uchaguzi ujao ufanyike na Katiba hii na tumewaomba wale wanasiasa wasikilize maoni kwamba itakuwa ni hasara kubwa kufanya kazi hii, kuleta chombo hicho halafu tukiache tena. Asubuhi anayekuja kama atasema hii ni sawa au atasema anataka kuendelea na mambo yangu hatuna hakika hapo lakini hakika tuko nayo ni kwamba tunachombo hapa. Hiyo ndio hakika tulionayo sasa tunaomba kitumike hichi chombo hichi basi, hiyo tu. Kule kwengine kujako sasa hiyo itakuwa ni mambo mengine.

Local resources, mambo ya kodi kwamba tunataka vitanda, kila kitanda Mzungu akilala lazima tupate pesa sasa ni district straight away hiyo. Mara moja kabisa, hata mkutano wa kwanza kabisa wakikutana watasema wanapitisha. Hiyo haina dhambi maanake iko katika Katiba hii na nafikiri watu wa Kwale wamekuwa wakilalamika kutoka miaka themanini. Nakumbuka mwaka themanini tulifanya delegation kwamba tupatiwa ruhusa wakatu huo ilikuwa ni shilingi moja. Tuliomba shilingi moja ya kila Mzungu anayelala hapa tukakatazwa, ikaja mpaka tukafika shilingi ishirini ikakatazwa, mpaka leo imekatazwa lakini sasa Serikali ya wilaya na la jimbo imepewa mamlaka hayo hata pia kule kwa national banks.

Upande wa Madiwani, Madiwani watakuwa wapi, Waziri wa Local Government ana nguvu sana. Kwanza tumeeleza hapa kwamba madiwani wale wa Town Council na Urban Council sasa wale ni sawa sawa na Serikali ya location. Wale Madiwani wa Urban Council na Town Council ni sawa sawa na Serikali ya location, kwa hivyo watachaguliwa vile vile kama Serikali ya location. Wale wa Madiwani wa kijiji, City au Municipality watachaguliwa kama wa district kwa hivyo yule wanamuita Mayor atachaguliwa na wananchi direct, straight away ndiye District Administrator huyo. Atachaguliwa na wananchi, kwa hivyo kwa sababu ya kwamba powers tumezileta chini si tena waziri wa Serikali za Wilaya anaweza kuingilia hawa, imeandikwa wazi kabisa kila kitu ni chao wenyewe.

Uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kuabudu, uhuru wa kushirikisha watu ukisoma section 34, 41, 44, arubaini na tano arubaini na

nane, arubaini na tisa tulikuwa tumeshazisoma hizo uko uhuru wote huo. Halafu uhuru wa kupata habari ya za Serikali tumesema pia uko, halafu habari ya kwamba wananchi wajue hii Katiba yao tumesema kwanza kazi hii tumeipatia vyama vya kisiasa. Vyama vya kisiasa sasa ni lazima vifundishe wananchi mambo ya Katiba hiyo tumeandika wazi, Governance lazima wafundishe tena miaka yote mitano kabla ya kura baada ya kura. Wasipofanya hivyo hawapati registration au wanafutwa kuna account sasa kila chama kitachunguzwa mwaka huu kilifanya nini, tumeandika mwaka ujao kimefanya nini. Kama hakikufuata zile sehemu ni kama Company's Act kama haukufanya vile ikifika jina lako haliko ndio tumefanya kwa vyama vya siasa, mmoja ya kazi yao ni civic education. Tume ya uchaguzi mmoja ya kazi yao ni civic education hiyo tumeandika wazi kabisa.

Athmani Riziki, Upper House na Lower House ameeleza kwamba ile Katiba amependelea kwamba kama Upper House itakuwa bara basi Lower House iwe Pwani. Nimesema kwamba Capital City katika sheria yetu itakuwa ni Nairobi lakini katika section 2 tukasema Bunge lenyewe litaamua kama mambo hayo yataendelea kuwa pale au watagawanya. South Africa kwa mfano wamegawanya, Serikali iko Pretoria, Executive, Rais, ofisi ya Rais iko Pretoria. Bunge liko Cape Town, Mahakama yako Durban sasa zimegawanywa gawanywa vile, kwa hivyo sasa tumeweka sheria pale kwamba wale Wabunge wakikaa wakiona Nairobi sasa imekuwa too much wao wanaweza kusema Upper House ni hapa, Lower House ni hapa. Tumewapatia uwezo huo, ni kusema kwamba Nairobi haiwezi kuwa ina-dominate mambo yote kila siku.

Habari ya kulikuwa na vidimbwi, madawa ya wale wafanyikazi wa Serikali, mbegu, matingatinga. Tumerudi pale pale sasa ni wilaya na mkao, Serikali hizo mbili ndizo zitakuwa na majukumu kama ni matingatinga ni Serikali hizo mbili. Kama ni vidimbwi vya kuogeshea ni hizo Serikali mbili, ikishindwa ni wao.

Upande wa Quran kwamba, ametaka itolewe kortini, mambo ya kushujudia yule Judge sasa tumeyaondoa hayo. Section 44, kifungu nambari sita (a) na (b) imesema wewe si ruhusa kufanya kinyume na ile dini yako inavyosema, sasa dini yetu ya Kiislamu yasema huwezi shujudia mtu. Kwa hivyo automatically hiyo uwezi na hawawezi wakakuzuia wakasema contempt of court, hapana unamtolea tu nambari 44, (vi), (a), siruhusiwi mimi kushujudia mtu yoyote. Sitaki kitabu changu cha Quran kifike kotini, tumeandika hapo section (b), haiwezekani.

Halafu Bwana Henry Adogo, yeye amependekeza safaru iwe na picha ya Kenyatta. Sisi tulikuwa tumesema isiwe na picha ya mtu yeyote iwe ni milima ya Kenya au bahari ya Hindi au mnazi au nini lakini isiwe na picha lakini yeye amependekeza, hayo ni mawazo. Halafu akauliza swali nzuri sana, hawa wanaouza ardhi pia waeleze kwa nini wanauza ardhi. Nafikiri zile sheria ambazo tumesema tutaenda tutazipeleka kwenye sheria tumesema pia lakini hatukuandika hapa, tumesema kwamba ardhi haihusiki na mtu mmoja. Mtaiona itatoka shauri ya hii, huwezi kuwa wewe ni baba kwa sababu tunasema ardhi yote mtu anayemiliki kwa niaba ya, kama si niaba ya bibi yake ni kwa niaba ya familia yake na watoto wake. Hawezi kuuza mpaka akutane na wale watu wa family wakubali, hiyo sheria pia itatoka.

Wazungu ukasema wanapata kazi na Waafrika wanawachwa halafu sheria zinawapendelwa Wazungu, tumeandika sisi

wenyewe hapa kwamba hakuna ubaguzi wa aina yoyote including ubaguzi wa rangi. Na mambo ya mishahara, NSSF na kadhalika yapatikane hapa, ile Retirement Banefit Authority inafanya mambo hayo.

Habari ya chokora tulikuwa tumetaja, vijana wasitie mimba nafikiri tumeeleza vizuri haki za watoto ni nini, lakini mambo ya mila, desturi na dini zitawachwa kwa upande wa ndoa. Mzee Kasima hapa akasema kwamba kuna umaskini mwingi na habari ya njaa, nafikiria ikiwa tutatumia Serikali zetu zilizoko tulizoziunda sasa mambo haya yatapungua kama vile ambavyo zamani. Maanake tumewapatia jukumu hao pia kuangalia mambo ya mnazi na mambo ya mkorosho, kama wataunda Coconut Development Authority, Cashewnut Development Authority ilo ni jukumu lao, wamepewa nafasi hiyo. Sasa ikiwa wameunda vituo hivyo si lazima bei zitapanda juu, hizo ni kazi zao. Haya wengine kumi.

**Mohammed Budzo:** Nitaanza na mzee wangu uchukue nambari yako, wewe ni nambari moja, wewe kaa mimi nasema nambari. Nikisema nambari moja ujue ni wewe haya halafu mzee wangu pale nambari mbili, halafu kijana wangu wa mwisho nambari tatu. Haya, Bwana Amiri nambari nne, nyinyi watu wa Diani nyinyi mmekuja wengi sana. Haya Mzee Ali pale nambari tano halafu nitakuja kwako, nambari tano halafu kwako. Nambari tano halafu mzee wangu namba sita, nambari saba, halafu namba nane kijana yule young tacks, halafu nambari tisa mzee Amaji pale namba kumi. Nambari mzee wangu, eeh, nambari kumi. Mama yuko wapi, kuna mama ambaye anataka kuzungumza hapo? Mama, hakuna haya namba nane ni wewe, kumi na moja haya. Tutaenda, tusikilizaneni maanake najua kuna swala kidogo watu wana…haya number one.

**Hamisi Omari Kisusi:** Jina langu naitwa Hamisi Omari Kisusi, mzaliwa hapa Ukunda. Mabibi na mabwana salaam aleykum mimi maoni yangu, mwaka sabini na saba tuliwekewa baraza hapa Mbindeni na Serikali badala ya kuwekewa baraza tukaambiwa mashamba yatagawiwa halafu wapewe wananchi. Mimi ni mmoja wapo ambaye nimepasua mpaka sabini na nane halafu mashamba yakagawiwa, ikawa kila mtu ana mahali pake. Sasa punde nikaona hawa watu tena wanarudi, mfanya nini? Wanasema sisi tunapasua mashamba. Mnapasua mashamba mbona sasa hamkuweka baraza na tena mbona mnapasua kimakosa? Wanasema Serikali ile ilikosea sisi tunaelekeza, sasa ikawa sisi tunasukumwa badala mpaka ule wa zamani tulisukumwa.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Unapendekeza nini?

**Hamisi Kisusi:** Mimi napendelea maoni yangu, mipaka irudi ile ile ya zamani.

**Mohammed Budzo:** Nambari mbili, nambari mbili alikuwa ni nani?

**Juma Bwoga:** Asante sana Bwana Commissioner kunipatia hii nafasi ili nitoe maoni yangu kidogo. Nimefika hapa mapema.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Jina lako kwanza.

**Juma Bwoga:** Jina langu naitwa Juma Bwoga. Nimefika hapa mapema na nimesikia karibu Katiba yote iliyosomwa na mengi wenzangu wameyazungumza lakini mimi nina kitu kimoja ambacho ningependa kukitaja. Kitu chenyewe ni umri wa viongozi, katika Katiba kama nimesikia vizuru imesemekana kwamba mtu akiwa na miaka ishirini na moja anaweza kuwa kiongozi na President akaambiwa akiwa na umri miaka thelathini na mitano anaweza kuwa President. Jambo hili la umri ni jambo muhimu sana na linataka kuangaliwa vizuri kwa makini. Mtu wa miaka ishirini na moja kuwa Mbunge au Councillor au Senator mimi naona umri huo ni kidogo sana kwa sababu atakuwa yeye hanauzowefu wa kitu chochote ametoka shule tu, jana. Mimi nataka ianze kwenye miaka thelathini. Pili, President awe ni mtu mwenye umri wa miaka kuanzia arubaini kuenda mbele.

Na kuhusu mambo ya Katiba nasema kwamba itakuwa sasa hivi ni vigumu kujua uzito au urahisi wa hii Katiba na mabadiliko itakuwa ni lazima yatakuwako. Kwa hivyo naomba kwamba hii Katiba itakapoanza kufanya kazi, ikiwa itafanya kazi baada ya miaka kumi tutakuwa tumeizoea irudishwe tena kwetu tuje tuizungumzie tena tuangalie yale mabadiliko ambayo tunataka kuyafanya. Nafikiri ni hayo mawili tu Bwana.

**Joseph Lunani:** Haya mimi kwa majina najulikana kama Joseph Lunani. Kufuatana ingawaje nimekuja kuchelewa kidogo na mimi ningependa kuongea kuhusu migomo ya aina tofauti tofauti. Nikianza na mashule, miaka mingi sana tumeona kwamba shule zetu zimekuwa na mgomo kwa sababu moja au nyingine, na unapata kwamba wanafunzi wakilalamika huwa kwamba kuna sababu lenyewe. Kwa sababu wanafunzi hawawezi kufanya mgomo wala kuchoma madarasa bila sababu na hiyo hutokana na uongozi mbaya wa waalimu ama labda wazazi. Sasa hiyo kwa maoni yangu ningependelea, ingekuwa vizuri kama tungekuwa na Katiba ya kutetea haki ya mwanafunzi pia. Kwa sababu nataka hivi maoni yangu kwamba wale wasimamizi wa elimu kama divisional inspector wawe kwamba wanafunzi kama wanajisikia kwamba labda wanamalalamishi fulani ambayo yanawakera kabla hawachukua kitendo ambacho kitaletea wazazi hasara ya kuaribu shule. Wapeleke pale maoni yao ambapo wataisikiza nao wakuje wakae na wanafunzi, wanafunzi waeleze ni kwa nini wanataka hiyo. Kama ni headmaster kuondolewa ni kwa nini wanataka atoke na watafute sababu zenyewe, wachunguze ukweli uko wapi halafu waone kwamba watatekeleza vipi ili kupunguza hasara wazazi wanapata. Kwa sababu wanajenga shule wanapata zimebomolewa wanaenda hasara.

Kitu cha pili, inaenda kwa uwajiri wa kazi. Kile kitu kimeongelewa lakini sasa mimi najiaongelea kwa vingine kwa sababu mimi mwenyewe sijaridhika. Ni kwamba kuna parastatals nyingi na companies nyingi ambazo wanaajiri wafanyakazi, lakini wakati mwingine unapata kwamba labda mtu ameumia kikazi ama labda kuna mambo fulani fulani yametokezea ambayo inatakiwa mwajiriwa afanye nini, alivywe. Lakini kwa vile wewe mwajiriwa wewe ni mnyonge na vile tujuavyo baiskeli haina sauti mbele ya pikipiki. Sasa unapata kwamba wewe baiskeli hauwezi kufikia mahali pikipili imefika. Kwa sababu gani, wewe mwenyewa mnyonge hauwezi enda mbele. Kuna vile vitu ambazo kuna institutions zingine kama labour wanakwambia kwamba nenda kwa labour itakusaidia, ukienda kwa labour unapata kwamba pikipiki ilifika huko kabla ya baiskeli. Sasa wewe unapata kwamba wewe mnyonge umesimama. Sasa kwa maoni yangu ni kwamba, kama hii Katiba Serikali ingechukua wale ma-advocate wa Serikali ambao watalipwa na Serikali. Ambapo sasa huyu mnyonge wakata atakuwa kwamba amefikia mahali imekuwa ngumu

aende hapo atoe malalamishi yake halafu aone itakuwa vipi. Huyu advocate ambaye atakuwa akiyakilisha huyu mfanyakazi mnyonge kwa sababu pesa zake hata hazifikii huko, amenyanyaswa.

Kitu kingine, yule mwenzangu alikuwa ameongeza kuhusu ngozi nyeupe na ngozi nyeusi. Kusema ukweli hiki kitu kinakera watu wengi sana, unapata kwamba mtu anachukua mtu wa ngozi nyeupe kuwa wa dhamana sana kuliko yule wa ngozi nyeusi. Hicho kitu kinakera watu wengi sana lakini mimi kwa maoni yangu ningeonelea hivi, kungekuwa kama mnaweza kuenda mahali halafu kuonekana kwamba huyu ngozi nyeusi au ngozi nyeusi ameonewa vibaya ama amepewa ngozi nyeupe mwanzo halafu wewe bado, hapo haki haijatekelezwa, huyo mtu achukuliwa hatua na uwe na mahali ambapo atapelekwa. Kwa sababu wewe mnyonge kufuatana na majibu yako umesema kwamba umeachia district, sasa hii district hii lakini wewe ni mnyonge tu hivyo hata ukienda kwa hiyo district ungali unakanyagwa tu kama kunguni. Sasa ikiwa tunaweza kuwa na ile kamati ndogo ama wale ma-Advocates ambao wanajua sheria ambao wako mahali na ambapo ikiwa huyu mnyonge ataumiwa hawa ndio wakutetea haki ya wanyonge vile mwanadamu wa hali ya chini. Nina la mwisho.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** …(Inaudible)

**Joseph Lunani:** Sawa. Nina la mwisho, mimi naongea kuhusu pesa za Serikali. Serikali imekuwa ikipata pesa za ushuru mwingi sana kutoka kwa wananchi na unapata kwamba hizi pesa za Serikali zina-signinwa na watu wawili ambao ni Rais na Waziri wake. Sasa mimi ningependelea kwamba hizi pesa kitambo zisainiwe kutoka kwa bank ya Serikali Central Bank zikuje zifanye kazi. Inatakikana hizo pesa ziwe zisainiwe na hawa watu wawili, ziwe zinapitishwa na panel ya watu kama ni Parliament, halafu ziwe na signatory ya watu karibu watano, sita ambao Bunge limepitisha, ambao wataenda kutoa hizo pesa. Baada ya hizo pesa kufanya kazi then sasa wataleta katika Bunge vile hizo pesa zimefikia, kama zimefikia mahali zimeenda mgomo kidogo huyo mtu mwenye alikuwa anahusika na hizo pesa inatakikana achukuliwa hatua kali sana kwa sababu wakati wa kuja kuchukua hizo pesa za ushuru kwa wananchi wanakuja na kifua lakini wakati wa kuzitoa zitaelea msituni. Ni hayo tu tafadhali.

**Amir Hamisi:** Salaam Aleykum waraha matulahi Wabarakatu. Kwa majina naitwa Amir Hamisi Banda, Mwenyekiti wa Baraza la Maimamu, Pwani Kusini. Kwanza ninapongeza Commission hii ambayo inaendelea na urekebishaji wa Katiba kwa kuona kwamba wamejitahidi kuchukua maoni namna yalivyotolewa na t……tulivyosomewa naoni kama yalipungua basi ni machache lakini mengi tuliyotaka tumeyapata.

Pili, ningependa kushauri wenzangu pia kwamba tupige kura na Katiba mpya. Ikija Katiba kama utaitishwa uchaguzi na Katiba ya zamani tugomeni, kura ni zetu, tugomeni. Tusemeni inshallah, kwa sababu ndipo kuipa nguvu hii Katiba kuona kwamba yale maovu yote tuliyofanyiwa tumekasirika kweli na kama umekasirika onyesha hasira zako. Naam Bwana, mimi nimekuja kuchelewa na sijui mengi yaliongewa lakini ningependa kuzungumzia pesa za uzeeni. Kwamba kuna baadhi ya watu hufanya kazi mwisho wakawa hawana familia na amezeeka, mwisho anadai hizo pesa mpaka anakufa. Akishakufa zile pesa hazina mwenye kuzidai, matokeo yake ndio hubaki kwa wale Mabwana wakubwa wa kazi. Sasa pesa zile twazitaka sisi zirudishwe

kwa wilaya mpaka kufikia ile Serikali ya location.

Tatu, ni ardhi kuna wageni humu huja kununua ardhi wanaishi mwisho halafu wanaenda zao halafu wanaweka jengo tu, ikifikwa kwao pengine hufa na linabaki lile jengo. Kuwe na muda maalum, jengo lile au ardhi ile ikiwa harudi jengo lile lirudishwe katika Serikali ya location. Nikiendelea katika hiyo hiyo ardhi, ardhi isiuziwe watu wageni kwa sababu kuuziwa watu wageni kuwe na kifungu ambacho kinamtakaza awe ni Mjerumani au ni Muhindi au ni nani kununua. Kwa sababu wageni wanapokuja kununua kwa wingi hizi ardhi ndio husababisha baadaya itakuja kuwa limerudi lile lile colony la watu wale weupe halafu weusi watakuwa ni kinyume katika maisha yao. Kwa hivyo twasema kwamba kuwe na kifungu ambacho kinazuia, ikiwa ni …

**(Interjection)**

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Katiba ikipitishwa wageni hawaruhusiwi.

**Amir Hamisi:** Asante, as56ante.

Halafu hili swala la lease mini linanikera sana ingawaje naambiwa iweko lakini mimi nasema lease hii ililetwa na wakoloni. Kama ililetwa na wakoloni kwa nini isiondoke kabisa, sasa kama ni kutaka mtu anataka ardhi iwe ni mkataba ambayo itatemea yale kusikizana na isizidi miaka thelathini na tatu.

Jambo la nne nasema Madiwani waongezwe, waongezwe nambari yao na waongezwe mishahara.

Jambo la tano, katika mapimo yale yaliopimwa humu mlikuwa na vibarabara ambazo zimetengwa na survey lakini utakuta mpaka sasa zile barabara zote zimejengwa. Tungependa katika Katiba kuwe na kipengele wale ambao walijenga katika hizo barabara basi wakati wa mipimo barabara hizo zaanza kufufuliwa basi waondoe nyumba zao kwa sababu walijenga bila mipango.

Halafu juu ya usalama, katika hawa wakubwa wakati kuna jambo limetokea la kiinchi ama pengine kuanzia polisi kwa mfano mtu ameshikwa, polisi amekushika amekupeleka kule sawa, lakini uendeshaji wa mahakama mpaka mtu yule ima kumfikia mpaka kunyongwa. Mimi ningependekeza kuwe na Tume iuundwe Tume ambayo itashugulika kuchunguza hawa polisi pamoja na Majaji, hii itakuwa independent. Kwa mfano kule uzunguni sijuhi ina jina lake, sijuhi wanaita…limenitoka hilo jina maana mimi si Mzungu sana mimi.

**Speaker:** …(Inadible)

**Amir Hamisi:** Naam, sijui kama ndio hiyo, iko tayari. Ndio Bwana ili kulinda haki zile za dhulma. Nikimaliza nasema. Pale

ferry kuwe na utaratibu ambao unamfanya yule mwananchi wa kawaida asidhurike. Mfano, utakuta kiongozi bado yuko State House watu wanarundikwa pale, yeye atakuja saa tano ikiwa watu wamerundikwa tu hawavuki na akija avuka yeye peke yake kama gari moja ama watu wawili tu basi hili lisiweko. Pili, sasa hivi ikifika saa kumi watu hurundikwa ikawa ferry yaani saa tisa ferry moja ya petroli tu basi, watu wanarundikana mpaka na akina mama, watoto wadogo ikifikia wakati mwingine toka …pale pale. Kwa hivyo twataka kuwe na utaratibu wa ferry ambao wananchi wasiwekwe pale zaidi ya dakika kumi iwe tayari wanavukishwa pale.

Nikija katika upande huu wa umri ambao umezungumzwa, kwa kweli mtu kumpa wadhifa akiwa na umri wa miaka ishirini na tano huwa bado kwa mazingira yetu. Kwa sababu tukiangalia watu wa zamani na sasa mtu akiwa miaka thelathini bado damu yake inachemka. Halafu mtu wa miaka ishirini na moja apewe Ubunge basi huyu atayari anaweza hata ku….(Inaudible) mimi naunga mkono yule mzee. Kuanzia miaka thelathini kuendelea mbele na kama ni Uraisi kuanzia miaka arubaini vile vile kuendelea mbele.

La mwisho Bwana ni kuhusiana na museum. Kuna majengo mengi ya zamani ambayo yamehifadhiwa lakini utakuta Serikali imechagua baadhi na baadhi ya mengine yameachwa. Mfano ukienda kama Kazikazi pale huko Musikiti ya zamani lakini utakuta sasa Muskiti ule mimi leo kuingia siwezi maana mzingiwa kwenye maoneo yale ya tengo iachiwe. Kama ya Waislamu iachiwe wenyewe Waislamu kuyamiliki na kama ni Makanisa waachiwe wenyewe Wakriso sio jingo lile lawekwa pale lakini faida zaidi zatumika kwenye Serikali. Wewe Muislamu umeachwa kuenda kuabudu tu pale, sasa itakuwa pale bado twasema Katiba hii kuwe na kipengele hicho. Kwa hayo machache. Asante.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Nambari tano

**Speaker:** Nambari tano ni mimi hapa.

**Ali Omar Kweli:** Kwa jina ni Ali Omar Kweli ni mshauri wa baraza la Maimamu, South Coast. Mimi kwanza kabisa nitaingilia swala la mavazi, heshima ujiwekee mwenyewe ndipo mtu mwengine naye akuheshimu na Katiba inayopingana sana na Mungu ndio mashaka mengi hupatikana kama hivi nchi yetu ilivyo. Nikisema hivyo, kina mama kila siku wanaunda Tume tofauti tofauti wakitaka Serikali iwalinde kwa sababu vitenda vya huduma wanavyofanyiwa na wanaume wakishikwa kwa nguvu wakifanyiwa nini, lakini sijasikia hata siku moja wanaalani yale mavazi wao wanayoyavaa. Kiumbe wa kike ameumbwa na Mwenyezi Mungu na Mungu yeye ndiye aliyempatia tu nguvu zile za kuwa yeye na mume ni vipi. Pendekezo langu mimi nasema inastahili Katiba hiyo iweke vazi la kuheshimika ambalo litatumika hapa nchini, hususan kwa akina mama ili tulinde ule ubakaji ambao unaendelea.

Jambo la pili, nitaingilia pale nyuma kabisa kwa vile mimi nimechelewa na nikatulia sana lakini pia sijapasikia ikiwa pamesemwa nitazidishi. Sisi ingalau wengine wamedai kuwa tukizungumza tuzungumze kama Wakenya lakini mimi nasema tumetengwa

mapema sisi kama si wa Kenya na ukweli lazima uzungumzwe. Kule kutengwa kwetu bado hatujakuwa na matumaini mazito kuhusu Katiba inayoendelea kuwa itatufanikisha na kupitia malengo ya kuondoa huu unyanyasaji ambao tunanyanyaswa sisi wa Pwani. Tukiona Katiba haitufai tutaingilia mwambao basi tupambane tuone utapitia wapi, kwa hivyo huo sisi tunasema uwekwe kisawa sawa. Ikiwa Bwana Commmissioner hujauweka kisawa sawa nakuambia kama Mpwani, ikiwa hujauweka kisawa sawa kwa utafiti huo mwambao uweke kisawa sawa huo mkataba wetu utatufaa hapo mbeleni baada ya kuwa Katiba haitutumikii.

Jambo jingine ni habari ya lease, umeguzia hapo kuwa wewe ulizungumza kuwa Katiba inasema haiwezekana hizi kuuzwa lakini hivi lease zetu hapa zilipo ziliuzwa zote. Mtu anapewa lease tena hata hizi lease za sisi kwa sisi wacha wale wageni mnaowauzungumza. Mkikaa mnazungumzia Wakoloni waupe bure lakini wakoloni wabaya ni weusi, hawa wenzetu wote waliopewa zile lease. Mtu amepewa lease kwa bei chache kabisa na akaifanya sub-division, akaikata kata akauza akapata mabilioni ya pesa halafu akaanza kuenda zake. Sasa ni kusema kile kipengele ambacho kilikuwa kinalenga maswala kama hayo, ikiwa kimepungua kasi kiwekwe kasi kuhakikisha kile kifanye kazi tupate zile haki zile.

Jambo jengine na la mwisho ambalo nitamalizia, mimi nasema ukweli kabisa. Katika vile vipengele ambavyo mshavitayarisha hapo vinavyosema utaratibu utafuatwa kwa zile haki ambazo zilichukuliwa kinyume kutoka iwe ni haki ya ardhi, ni ya nini, ni ya nini na imeambiwa hayo maneno yalisemwa yatafuatiliwa baadaye. Naomba Tume ikienda ikikaa katika vipengele kama hivyo ambavyo baadaye vitachunguza zile haki zilivyoharibika, tukitaka nchi itulie vipengele hivyo viwekwa strong sana. Sisi tunazungumzia hivi kwa sababu tulidhulumiwa sana na pindi ikiwa haki zile hazikuwekwa sawa sawa na zikachungzwa zikawekwa sawa sawa huenda sasa muda huo tukigeuka tukisema Katiba haitufai msije mkatulaumu. Kwa hivyo tuwaomba Tume ikae sana ifikirie hicho kitu cha haki zilizoharibika zitafanywaje mpaka ziweze kurudi kwa wenyewe. Asanteni.

**Juma Gatimu:** Mabibi na Mabwana Salaam Aleykum. Kwa majina naitiwa Bwana Juma Gatimu mimi ni Secretary wa NARC Msambweni. Katika hii Katiba mpya kidogo ningeeleza kama hadithi kidogo. Katiba hii mpya tumelilia siku nyingi sana kwa vile Katiba ile inaongoza sasa ni Katiba ambayo ina unyanyasaji wingi sana. Kuna Mabwana walikuwa ni mahabusu wametekwa nyara kupelekwa nchi nyingine na walipofika jangwani ukawa tu twafanya fujo kule watu wetu waachiliwe, na wao kule wafanya fujo nao waachiliwe. Serikali yao ikapiga simu kwa wale walikuwa, na ndege huko wakaambiwa hapo hapo. Mlipo mteremshe hao hapo hapo mwawachilie hapo hapo. Wakasema Mabwana tuko jangwani tukiacha hawa hapa watakufa lakini wakaambiwa hapo hapo. muwawachilie hapo hapo, msiende na hao. Kwa sababu mkitoka hapo mtakuwa mmefanya makosa sasa tena, kwa sababu sheria ni waachiliwe sasa. Sasa wale Mabwana wakiachiliwa walilia uhuru wao wataachiliwa wako huru lakini kwa kweli hawana watakufa jangwani, na wakienda na ile ndege waregeshwe pahali pa salama pia ni makosa kwa sababu wenyewe watashtakiwa kwa vile wale ni mahabusu watakiwa waachiliwe. Sisi ndivyo tulivyo, tumelilia Katiba mpya na Katiba mpya tumeipata na imekuwa tuachiliwe sasa basi lakini hatuna safety net. Kitu cha kujitegemea sasa kuwa hii Katiba ni sawa sasa isije ikalegelewa katika mambo mengine ikawa bado tuko pale pale tulipoanza.

Maanake ni hivi, vipengele vingi vimeshikwa na hii Katiba mpya na tumewaambia basi wapeni, sawa wapeni na tumepewa, lakini Katiba mpya hii yetu kama Katiba ya Amerika inasema kwa Mungu na watu wa Amerika halafu wanasema katika Mungu sisi tunaamini. Lakini Katiba yetu katika pale kile kuzuli cha mwanzo mwanzo hakionyeshi ni Katiba yetu vipi na Mungu vipi. Kuna Bwana mmoja pale, Sheikh mmoja alisema mwanzo mpaka tujue tumweke Mungu mbele katika mambo yetu, Katiba yetu na mimi ningetaka ianze pale kuwa Mungu na watu wa Kenya halafu iwe. "Sisi watu wa Kenya tunaamini katika Mwenyezi Mungu", kichwa cha Katiba yetu ya Kenya iwe namna ile.

Halafu kuna Tume nyingi pale wameunda za kudumu lakini hawakuunda Commission ambayo itaongoza mambo ya kidini katika nchi ya Kenya. Tukiwa tuwatu wa mcha Mungu lazima tuwe na Commission ambayo itakuwa ikichunguza. Juzi kulikuwa na mambo tunaambiwa oh, kuna watu wanaabudu shetani kuna watu wanafanya nini, yale ndio……….(Inaudible) janga hizo zote. Tukapata njaa tukapata mambo mengi kwa sababu labda sisi tumeasi Mwenyezi Mungu. Tukiwa na Commission ambayo inaongoza watu katika mambo ya dini, nyingi zimezuka duniani hapa Kenya mwanzo nyingi sana. Kutoka mwaka wa sabini, themanini tumekuwa na dini nyingi sana zingine ni commercial sasa tuseme ni mishahara tu, si Mungu anaabudiwa ni mishahara. Hapo Commission ya kuangalia mambo hayo ningeliomba iweko.

Kabla sijaenda sana ningelisema kabla ya kusahau, uchaguzi ujao tufanye chini ya Katiba mpya, tusifanye chini ya Katiba iliyopita na pia hapo hapo pale hatari inaweza kuja hapo kwa hatari iliyoko. Tuwe na njia ya kwamba Katiba hii mpya haitahujumiwa kwa sababu tukishaingia katika uchaguzi na Katiba mpya kuna petitions zitafanywa, petitions zile zitaenda kwa mahakimu walioko sasa ndio watapelekewa zile na Majaji walioko kwenye viti sasa maofisi tunajua ndio maana wanaitwa Majiji wa kisiasa. Walichaguliwa na nafasi, si kuwa watu walikuwa wamehitimu chochote, walichaguliwa na mtu kwa manufaa yake mwenyewe.

Kwa hivyo kitu tungelisema ni hivi, kabla Serikali nyingine haijaingia mambo ya mahakama ndio mwisho kwa sababu naambiwa ilipitisha na ndio mwisho na hiyo imeishia hapo. Je, kama ni hawa watu walichaguliwa vile vile wao kushikilia masilahi ya watu wengine, wakiweko vile vile tutakuwa hatukupiga hatua chochote. Hii Katiba hii hii itapelekwa mbele za hawa hawa mahakimu hawa na itakuwa haifai ilikosewa. Katiba ile ilifanywe kinyume cha sheria pia na itakuwa haifai tena na hakuna pahali mtaipeleka tena. Itakuwa ndio mwisho itaanzwa tena Katiba nyingine ianzwe kutengezwa tena. Pesa ambazo zimetumima ni nyingi sana, pesa sasa ni yetu, za zule na za yule, ni zetu zote na ni pesa ambazo zingefanya mambo mengi sana, zingelipwa waalimu hawa wamegoma. Ningelipenda kama tutaenda katika uchaguzi na Katiba hilo mpya tuwe na majaji wapya katika yale maofisi tena. Chief Justice aondoke aliwekwa pale juzi kwa lengo la KANU, KANU ndio wameweka yule Judge pale kwa sababu yeye awe pale mambo yote yatakaokuja awe akishikilia kwa hivyo, wale ma-Judges wote katika Kenya waondolewa. Tuwe na ofisi mpya ya majaji sasa ndio itakuwa Katiba mpya itakuwa iko safe.

Hapo katika mambo ya kwamba sasa sisi tumeongea mambo ya elimu, elimu ya bure vitu gani vya bure hiyo pia hairidhishi. Kenya yote itakuwa kitu kimoja na bado nafasi aliyenacho na ambaye hana bado ni kubwa sana. Kizungu wanasema the have'

s and the have nots, yule anacho na yule hana, bado ile nafasi ni pana sana na sasa tumeletewa usawa kuwa wewe na mimi tuko sawa. Aliye Garissa, aliye Lamu, aliye Kwale, aliye Bungoma, aliye wapi sote tumewekwa sawa sawa sasa. Ndio kama tume kuwa sawa sawa tumeambia Kwale District italipia mapolisi wake italipa kila kitu, yule yuko Garissa vile vile na yule yuko wapi vile vile atalipa vile vile. Mpaka pawe na njia, ipangwe njia mwanzo ya kwamba sawa watu. Namna ya kukisidia wale, mishahara italipwa vipi kwa sababu itakuwa ni vigumu kulipwa wakati ule ule wakati mmoja wengine wanacho na wengine hawana. Itakuwa ngumu na wengine wata-fail tukiendelea mbele wengine watashindwa namna ya kufanya, watashindwa pia kulipia hao waalimu. Watashindwa kulipia hao mapolisi wao pia ambao watakuwa wameandika, mpaka pawe na njia imetengwa mwanzo ya kwamba hivi ndivyo itakuwa watu wasije wakakosa kuendelea kwa sababu mpe tu mpe, ametaka mpe.

Nyingine ni mambo ya uwezo katika uwezo wa kupata, uwezo wa kununua. Uwezo wa kununua ndio maisha ya mwanadamu, ule uwezo wa kununua sasa ule uwezo tungelipenda kwamba kuwa na njia, kuwe na Tume ambayo itakuwa ikiangalia ama itapanga namna ya ni kushukisha vitu bei iwe sawa sawa. Ni kuongeza thamani ya pesa iwe inaweza kunua kwa sababu ilipopote na duru ikapotea, maskini alimazwa. Maskini pesa yake ni nduru, sumuni, shilingi zile ndizo pesa za maskini. Shillingi ishirini kutoka zamani si ya maskini ni ya tajiri sasa yale mapeni ya kumwezesha maskini kufanya kazi alegezewe ile uwezo. Asante sana.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Numbari saba.

**Saidi Ali Mwanjama:** Ndugu Waislamu, mabibi na mabwana Asalaam Aleykum.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Saidi Mwanjama:** Machache niliyo nayo, kwanza nijilaumu kwa kuchelewa kwangu.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Jina, jina Baba.

**Said Mwanjama:** Jina ni Saidi Ali Mwanjama. Kwanza nijilaumu kwa kuchelewa kwangu. Pili, maoni yangu. Mimi napendekeza Katiba ambayo yatengenezwa sasa ifanye kazi kupitia uchaguzi wetu na pia kwa niaba ya wenzangu nasema hatuna haraka ya uchaguzi ili ufanywe chini ya Katiba ya zamani. Haraka hiyo hatuna hata kama kutakuwa na muda mwingine wa miezi sita lakini uchaguzi ufanywe chini ya Katiba mpya.

Pili, ningependekeza katika retire za makazi, mapendekezo yangu katika retire za makazi. Mtu huwa yua-retire labda kuanzia miaka hamsini na mitano ama hamsini walakini anapo-retire labda apewe laki zake mbili lakini laki zake mbili hizi hawezi kuzitumia miaka mitatu. Mapendekezo yangu, Serikali ijaya, retire kama hii ama mzee aki-retire aweze kupata ama kuwe kuna uwezo wa kuweka either ni mtoto wake, ni mjomba wake vile ambavyo aweza kusukuma tena maisha hapo mbeleni. Either

kama ni yule atakayependekeza labda ni mtoto wake, mjomba wake ama ni ndugu yake.

Halafu tatu michezo, nitaenda kwa michezo kwa sababu katika taifa letu la Kenya mfano kama mchezo wa mpira tutasikia kuna timu ya taifa lakini timu ya taifa ile haihusishwi wananchi Wakenya wote, ama wananchi wa kwenye mikoa ya Serikali ya taifa. Labda ni makabila fulani waliondani ya hiyo mechi ya kitaifa. Kwa hivyo maoni yangu nasema kama ni timu ya kitaifa ihusishwe wananchi wa mikoa kote nchini katika taifa letu.

Nne, ni bahari nikasema bahari Serikali ijayo ya majimbo tungependa kuwe na uwezo wa kustarehe ama waku-enjoy kwenye bahari yetu kulingana na taratibu za Serikali yetu ya majimbo kinyume cha vile ilivyo saa hii. Ukionekana either baharini kuoga ama kutembea kwenye hoteli wewe either uwe ni mkora ama ni mtu mwingine ambaye huweleweki. Maoni yangu kiSerikali ya majimbo kama sheria itafanya kazi tuwe na uhuru wa kutembelea bahari yetu, kuoga bahari yetu na pia kutembelea mahoteli yetu vile ambavyo tunaweza ku-enjoy katika mahoteli yetu.

Kabla haijafika mwisho Mweshimiwa Officer ningeomba katika kitabu chetu cha Katiba nimeona vitabu vyote viliandikwa kwa Kizungu na wote hawakusoma Kizungu. Wengine hawakusoma Kizungu, ningependelea kama kuna uwezekano kuwe na vitabu vya kuandikwa Kiswahili na vya kuandikwa Kizungu. Jengine..

**(Interjection)**

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:**

**Saidi Mwanjama:** Ni la mwisho.

Jengine, wazee wapate marupurupu kupitia Serikali yetu mpya ya majimbo. Nikisema wapate marupurupu, kufikia miaka sabini mzee aina yoyote huwa hawezi uzito wowote tena wa kujimiliki. Serikali yetu ya Majimbo kama tutafanikiwa wazee wetu kufikia miaka sabini Serikali iweze kunakili hawa wazeee na kuwapatia marupurupu hata kama ni shilingi elfu tatu au nne kwa mwezi. Kwa hayo machache asanteni.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Nambari nane.

**Saddiq Juma:** Mimi kwa majina naitwa Saddiq Juma Sefu nimetoka shirika la Asimilani Development Organization. Mimi kwanza ningependa kutoa shukrani zangu kwa dhati kwa niaba ya shirika langu kupongeza Tume ya Marekebisho ya Katiba kwa kazi walioifanya kufikia sasa. Ni maombi yangu kwa Mungu kwamba chombo hiki kiweze kufanya kazi na tuweze kukitumia kiukamilifu. Mambo yangu ambayo ningependa kuongezea ambayo naonelea kwamba hayakuguziwa katika ile draft iliyowekwa ya Katiba ni manne.

La kwanzi ni ile mwenzangu aliyetoka hapa ameguzia kidogo kuhusu mambo ya pension. Mimi naonelea pension iweze kupewa kwa wale watu ambao wamefanya kazi na pia wale wazee ambao kwamba wamefika umri kwamba hawajimudu. Kwa sababu tukifikiria kwa undani sana yule mtu aliyefanya kazi na yuke ambaye bado hajafanya kazi kwa maisha yake yote, ayenastahili kupata pension zaidi ni yule ambaye hajafanya kazi kwa maisha yake kwa sababu yule ameshajipangia. Kama ni kujijengea nyumba amejijengea na kusomesha wale watoto wamesomesha. Je, huyu ambaye kwa maisha yake yote hajapata chochote twaona kuna haja yeye kupata chochote? Kwa hivyo naonelewa ile Katiba ingehusisha kwamba muda kama wa miaka sitini na tano ama sabini kama vile mwenzangu alivyotangulia kusema haweze kupata marupurupu haya.

Jambo lingine ni kuhusu vifaa vya Serikali, tunaona kwamba kuna sehemu zingine kuna vifaa vya Serikali kama magari, nyumba na mambo mengine. Baada ya kwamba Serikali imetumia vifaa hivi halafu baadaye uwachwa bila kutumika tena na huwa ni hasara kwa Serikali. Tukichukulia magari mengi hutumika halafu yakawa kuna vifaa vidogo vimeharibika badala yakuwa yale yarekebishwa yanawachwa pale halafu baadaye yanafanyiwa auction. Ile auction na huwa inafanywa kwa njia ambayo sio ya halali, ile action ingefanywa kwa njia ambayo kila mtu muhusika wa sehemu ile apatishwe habari na kama ana uwezo wa kupata kifaa kile aweze kukipata.

Jambo lengine ni kuhusu mawakili, kuna haja sana hii Katiba igusie kwamba mtu ama mwananchi wa Kenya ambaye hana uwezo wa kupata wakili kumwakilisha katika mahakama, Serikali iwe na mawakili special ambao watakuwa wakiwatetea haki zao hawa maskini katika hizi mahakama.

Halafu jambo la mwisho ni kuhusu mashirika yasiokuwa ya ki-Serikali. Kuna mara nyingi mashirika haya yasiokuwa ya kiserekali huja kufanya utafiti katika sehemu za vijijini ama mashambani, baada ya pale katika sehemu zile huwa na mashirika madogo madogo ambao wanaitwa community based organizations ambao pia hutekeleza kazi kama zile. Kungekuwa na kipengele katika Katiba ile ambao tunaitarajia kwamba mashirika haya yasiokuwa ya kiSerikali yakifanya utafiti yaweze kushirikiana na mashirika haya madogo madogo kule, yaweze kuwapatia ule ufadhili ili waweze kutekeleza kazi ile ambao wao nao wanaweza kuitekeleza ili nao waweze kunufaika. Asanteni.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Nambari tisa, ilikuwa ni nani sasa. Haya zungumza nambari tisa haonekani.

**Abdalla Boga:** Ni mimi. Asalaam Aleykuma Warahamatulahi wa Taala Wabarakatu. Tume ya Katiba nashukuru sana mko hapa kama mlitia ahadi siku ile mlitoka lakini…

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Jina.

**Abdalla Boga:** Abdalla Boga, chairman ya … Hii Tume ilipoondoka siku ile ilisema itakuja tena hapa, na ikija itatusomea yale

marekebisho ya Katiba ambayo mtu ambaye hakusikia mambo kama yake ndio atasema ni sawa, lakini tangu nije hapa sijasikia kitu kama hicho. Ni watu wanatoa maoni sasa nimechelewa lakini mimi maoni yangu sijasikia mpaka sasa hasa kuhusu misitu ya kaya, kuhifadhi kwa makaya. Tangu hapo nikisikiza sijasikia swala kama hilo, hii misitu ya kaya na kuhifadhia wanamakaya sijasikia kitu kama hicho. Na pia vile ni kusema yale maduka ya maskini na ya matajiri yatengwe sikusikia kwa hivyo hilo swali nakupatia Bwana. Naendelea sasa.

Sasa Bwana Tume inasema hivi sisi uhuru tumepata 1963 lakini wenzetu kila ukiangalia mwenye pajero nzuri amevaa vizuri, mashati mazuri, na uhuru ni huo huo lakini tukiangalia hali ya Pwani ni maskini kabisa. Huu uhuru ulikuja namna gani watu Pwani wakae ni maskini sana na wenzao ni matajiri? Maanake ukifika pale ferry utakuta pajero za huko tupo mpaka huko beach ni pajero tupu lakini maskini atatafuta kigari kimoja hicho tayari ni cha mtu fulani. Hebu hiki kitu itarekebishwa ama hizi pesa zikitoka huko za msaada zinamiminiwa huko peke yake huko juu kwa peak. Swala la kwanza ni hilo.

Swala la pili, tunataka hawa ma-DC wasiwe na uwezo kabisa wawe wanafanya kazi ya Serikali lakini uwezo lazima wapewe wenyewe. Kama ni mzee huku amewekwa awe anashikilia hiyo, DC yuko lakini pana mzee hapo, kama DO, hapo kama ni polisi kuwe na mtu wa hapo wa kikwetu maanake haya mambo yatakuwa yana tamaa. Bila hivyo itakuwa hii Katiba imetengeneza umaskini itakuwa pale pale, maanake hizi pesa zikija wao tu wananyakua. Kuna misaada mingi sana imekuja sijui ya Moi, ya nani lakini yakija ni weeh, inakuja kwa Njuguna hapo anaita wenziwe huko wanagawanya peza hizo anapea mtu mmoja tu pesa zote zimerudi huko. Kwa hivyo, hili jambo lazima liangaliwe.

Na jambo jengine ni kuhusu mila na desturi, mila na desturi shule zetu hizi zinafundishwa lakini hazifundishi mila na desturi. Watoto hawajui mila yao siku hizi. Hata watu wa vipande wanapata taabu mtu anaulizwa, wewe jina lako ni nani anasema, je mlango gani? Anasema mlango wa Pwani, cha mwisho hicho hajui ni pahali gani wala ukoo gani, kwa hivyo shule ni lazima wafundishe mila na desturi.

Na jambo jengine kuwekwe korti za Kiafrika zile za zamani zile ambapo watu wenyewe watahifadhi mila yao, mtu akikosea anakwenda kwa korti ya kimila pale kama moja iko Gatna. Vile zamani nyingine iko pale anakwenda kusikiza kimila mpaka anaelewa makosa yake basi ndio apelekwa uzunguni. Na jambo jingine askari anaposhika mtu kama inawezekana sikatai iandikwe tu huyu ameshikwa kwa sababu ya drunkedness and disorderliness anapelekwa mpaka huku anasoma karatasi yeye mwenyewe wa kumshika hayuko. Ni yule askari alimshika na mtu wake ndio kule aka-state hii mambo lazima ifanywe, yeye ndiye alikamata mtu wake ndio aende huko aka-state vile alimshika ni saa ngapi na amefanya kosa gani. Si karatasi zisomwe tu, huo si uhuru Bwana uhuru lazima ustarabwe na kule kutia pingu mtu anashikwa na anawekewa pingu ya meno barabarani akipita. Hili jambo liondoke, liondoke kabisa maanake hivyo si uhuru Bwana.

Vile vile kama kuna makoso hii Kenya ilipotawala kweli tulikuwa na uhuru lakini watu hawakuelimishwa maana ya uhuru ni nini. Hii ni jambo hatukuelimishwa kabisa Bwana maana ya uhuru ni nini, watu walifikiri uhuru kitu gani kwetu ofisini. Ule utaratibu

wa uhuru na nidhamu wa uhuru na ustarabu wa uhuru ni kitu gani, mpaka sasa hakuna kitu kama hicho ndio kwani farakano lote limeingina. Na hii Coast katika kila kijiji ama katika location lazima kuwe kuna mzee, mzee wakutajika wacha chifu lakini kuna mzee kama vile zamani. Mtu kama anashida anasema nenda kwa mzee fulani, kama kwetu Faida hatuna haina mzee yoyote ni taifa tu, mpaka kuwe na mzee kama Mzee Bambori alikuwa hapo zamani. Mzee Bambori huko hapo.

Jambo jengine, mimi nilitoa memorandum yangu huku …..(Inaudible) nilikuambia hizo pesa hizo zote zirudi katika Mkoa wa Pwani tena zinatakina huku…...(Inaudible)

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** …(Inaudible)

**Abdalla Boga:** Nilisema habari ya ushuru na forodha bandari, zile pesa kwetu za zamani hizo zimekwama ziko juu siku hizi zote. Kwa hivyo tumewaambia tangu 1962 mpaka zile pesa tunazitaka wenyewe zije huku Pwani zifanye kazi Bwana. Kwa hivyo kwaheri.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Nambari kumi, haya na mwengine yule ambaye alikuwa …

**Suleiman H. Setu:** Ndugu waheshimiwa Salaam Aleykum. Mimi ni Suleiman Hassan Zetu, mwandishi wa ndoa za Kiislamu, Diani na Kinondo Location. Mimi maoni yangu yanapitia katika kazi yangu tu, mengi yamezungumzwa na wenzangu ambao yahusiana na kila upande, lakini mimi nitazungumzwa mambo matatu ambayo yahusiana na kazi yangu. Kwanza ni gharama za korti zipunguzwe, hiyo ndio fikira yangu kwa sababu kuna wengi akina, mama ambao huwa wana matatizo na wakienda katika koti ya Kadhi sasa zile gharama wanazobandikwa huwa hawaziwezi na hurudi nyumbani na haki zao zikapotea. Kwa hivyo gharama za korti ziwe chini ili kila mmoja aweze kumudu kuzigharamia ama si hivyo niungane na wenzangu kwamba kuwe kuna wakili wa Serikali ambaye atawasaidia hawa akina mama. Hilo ni jambo la kwanza.

Jambo la pili vile vile, katika ofisi ya Chief Kadhi kuna Makadhi halafu kuna ma assistant registrar, waandishi wa ndoa, kwa hivyo naomba kitu kimoja. Pia hawa Waislamu wapunguziwa taabu ya kumwona Kadhi ama Chief Kadhi wakati anataka kuoa mke na hana walii, ma-assistant registrar wawe na uwezo kama vile Kadhi. Baada ya kuhakikisha kuwa mambo haya hana walii wake awe na uwezo wa kuweza kumwoza kama vile Kadhi anavyoweza kumwoza mwanamke.

Halafu la tatu kuongezea ni kusema kila location kuwe kuna mwandishi wa ndoa na talaka badala ya kuwekwa mtu mmoja tu katika Kwale. Halafu vile vile nikiongezea hapo ma-assistant registrar hawa wawe wanawaajiri kama wanavyoajiriwa wafanyakazi wengine wa Serikali. Kwa sababu wao pia wanaandikwa kwa Mkuu wa Sheria lakini utaona wao hawalipwi kitu kwa hivyo nao wawe wakipata malipo.

La mwisho nataka kuwe na kijitabu cha kujifunza uraia ambacho kitatoka katika kila baada ya miezi mitatu ili watu wasome

Katiba wajue haki yake ni nini.  Asante.

**RashidaBakari:** Jambo.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Sema jina lako kwanza.

**Rashid Bakari:** Jina langu ni Rashid Bakari.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Utakuja hapa karibu…(Inaudible)

**Radhid Bakari:** Nishasema Rashid Bakari mimi.

**Mohammed Budzo:** Haya endelea.

**Rashid Bakari:** Mimi haya maneno uliyosema ni mengi sana lakini yangu ni mawili nataka kusema.  Hapa kwetu ilivyo kuna mtu amepanda miti kama hii tangu kuanzia mwaka sitini na moja sasa miti imekuwa mikubwa namba hii, hajaona mtu yeyote kusema hii shamba ni yake lakini hivi sasa kuna mtindo hapa atakuja mtu wa Serikali atasema hii shamba ni ya huyu Njuguna. Huyu Njuguna alipata wapi hii shamba alilima lini, anasema ni yake kwa sababu ya hii karatasi ili awe ni yake kwa sababu ya hiki karatasi.  Sasa hii karatasi mimi siwezi kununua hii karatasi, naweza kununua?  Sasa sisi wanyonge twapokonywa mashamba na hawa wakubwa wetu hapa hapa, ndio wanakuja na Njunguna na unamwambia wewe unataka shamba, haya twende tukamnyonge kule kijana moja anaitwa Mwanamfanya huyu hana nguvu.  Basi hiyo shamba itakwenda kweli kwa Njuguna na si watu wengine kutoka bara, hawa hawa wenzetu hawa wa hapa.   Jambo la kwanza hilo.

La pili, hatutaki iwekwe wire ile bahari vitu vyetu ni viwili ni shamba na ile bahari hatutaki iwekwe wire ile.  Mbona mimi sijuhi kusoma lakini nikisikiliza naambiwa utatiwa wire, tangu lini mbona tangu hapo ilikuwa hakuna wire.  Kwa hivyo poleni nyote wananchi ni nyinyi wakubwa ni maneno mawili haya.  ***(Applause***)

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Haya, maneno mawili lakini mengi, haya.  Hayo ni maneno mengi sana.

**Mohammed Budzo:** Tuwe watulivu, tuwe watulivu kidogo.

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Sikilizaneni mbona wainua mkono nimesema kumi halafu nitaenda kwa wengine, kama umechelewa utatungojea Bwani nijibu haya halafu nitakuja kwako.

Kwanza kuna maswala ya ardhi, tumesema kwamba maswala ya ardhi tutarudi tena tuangalie ile mipaka nafikiri tunarudia rudia

sasa yale maswala. Tumesema kwamba katika miaka hii miwili ijayo ni lazima haya maswala yote ya ardhi yangaaliwe, hiyo tumeandika.

Miaka ishirini na moja tutaenda kuangalia, maoni tutasikiliza wale wanasema viongozi hawafai Wabunge kuwa miaka ishirini na moja, iongezwe iwe thelathini, uraisi uongezwe uwe arubaini hiyo ni sawa.

Halafu, mzee Boga amesema tuwe na kurekebisha Katiba kila miaka kumi, sisi tunasema kwamba haina haja kungojea miaka kumi lakini Katiba hairekebishiki mpaka wananchi wenyewe wasema basi ni miaka mia moja, miaka ishirini, ni miaka mitano ni wananchi wenyewe waoni ile haja ndio watasema watarekebisha.

Haki ya wanafunzi tumesema kwamba sasa hizi ni sheria ambazo zitaingia katika Education Act haina haja ya kuzieka hapa. Hata upande wa kazi za hawa wale wa parastatals hata hizo sheria ziko hazifuatwi tu. Lakini tukiangalia upande wa pendekezo kwamba tuwe na mawakili wa raia, hilo ni pendekezo nzuri tutalichukua, kama mtu ameshtakiwa basi akuwe na wakili wa Serikali.

Halafu kule ubaguzi wa rangi, tumesema kwamba ni hatia sasa kubaguliwa kwa ajili ya rangi, tumeandika hiyo. Zamani ilikuwa haiko lakini si kitu ambacho ni rahisi sana kuondoka sasa sisi wenyewe tukazane sasa. Kwa sababu hili ni neno ambalo limejenga misingi katika akili za watu tunaita atitude. Nimesoma gazeti leo hapa kule Wiingereza ni Ulaya kuna hizi timu za mipira siku zina Wadigo wengi, tunawaafrika wengi tunaita Wadigo wengi sana zile timu. Lakini leo nimesoma gazeti, kutoka wiki jana hayo maneno yanaandikwa, kila akiuguza mpira yule Mdigo watu wanamtoroka. Kuna mmoja alifunga mabao matatu, nafikiri jana lakini kila akiguza weeh. Na lile kundi la FIFA ambalo linasimamia mpira limesema kwamba litafanya uchunguzi halafu watu watashtakiwa ambao waligoma, wataleta sheria.

Ni neno ambalo ni vigumu sana kuilimaliza sasa wale vijana wa-kafrika wanaocheza mpira kule wao ndio wanawaletea sifa, wao ndilo wanafunga mabao lakini bado wanaangaliwa ngozi yao. Ni jambo la kusikisha sana, kwa hivyo hata hapa petu tume tumepitisha ni mwanzo wa kusema kwamba haiwezekani lakini ni kweli mpaka tukazane kama alivyosema Bwana Henry pale. Lazima tukazane ni kweli tutasema kuna usawa lakini tukifika ferry Mzungu anapita pale pale wewe unazuiliwa, hiyo ni kweli. Sasa ni wananchi wenyewe waseme Katiba yetu haikusema hivyo, tumesema tuko equal, tuko sawa mbele ya sheria kwa hivyo si jambo ambalo litakatika leo hilo itachukua muda. Ikiwa kule Ulaya mpaka lao Mwafrika akipiga bao bado yuazomwa tuko na kazi nyingi ya kufanya.

Pesa za Serikali ni lazima kuna watu wa-sign hiyo kwanza tumeyaandika mapema kabisa. Public finance and revenue, mfuko wa Serikali pesa hazitoki mpaka watu fulani watie saini, hiyo iko tayari.

Bwana Amiri kwa bahati mbaya umekuja kuchelewa uliyoyataja yote tumeshazungumza. Habari ya ardhi tumezungumza,

malipo ya uzeeni tulikuwa tumezungumza, mambo ya lease tumezungumza. Madiwani waongezwe na mishahara yao iongezwe, sasa hiyo automatically itakuja kwa upande wa Serikali zile za Wilaya na Serikali za location. Kwa mfano tumesema kwamba madiwani sasa tutakuwa na diwani mmoja, Locational Administrator lakini wale wanaunda council ya district watachaguliwa na wananchi wote. Kwa hivyo mishahara yao tayari hiyo imeshakuwa-taken care of.

Mambo ya Public Defender nimekuambia tumeshaweka. Ferry sheria ziko pale hazifuatwi tu lakini sheria ziko halafu. Hatuwezi kukuamba kwa sasa kwamba ile ferry ifanye kazi dakika kumi tu kwa sababu wenyewe ni biashara wanafanya wale. Kwa hivyo wakiona kuna watu wengi wao wanafanya maanake sisi hatulipi pale tunalifanya kulipiwa, wale wana-charge kulingana na nambari ya magari ambayo yanaingina, ni biashara hiyo. Kitu ambacho tunalilia ni kwamba kuwe na daraja letu, tunataka tuwe na daraja, hiyo ndio litatatua ile problem iliyoko pale.

Misikiti, Museum: umesema kwamba kuna musikiti kazi kazi pale hilo tayari tumeandika lakini hatujaliandika kulingana na vitu vya zamani. Kwa upande wa vitu ambavyo ni vya waislamu na mali zao tumeshaandika kwamba ni wao wenyewe watalinda.

Ali Omari mzee wangu, mavazi, hilo ni swala ambalo kweli litabidi tuliangalie kwa akina mama wanaovaa ambavyo sivyo hiyo ni kweli. Halafu ule mkataba wetu wa mwambao uliyosema siku ile ni kweli tumeandika katika upande wa ardhi ni kwamba lazima uangaliwe. Halafu haki za ardhi za zamani pia hiyo tumeshaandika na vile ambavyo umesema umechelewa.

Mzee Juma Gatimu, utangulizi kweli lazima tuingize pale jina la Mungu, hiyo ni sawa. Dini tumesema tumepewa uhuru lakini umependekeza tuwe na Religious Commission, hilo ni wazo ambalo hatujalisikia tutaliangalia.

Halafu majaji wamesema tuanze na majaji wapya, tumeandika hata utaratibu wa ule kuondoa wale wa sasa na kuandika wageni, tumeandika. Ukisoma hiyo transitional mechanism, tumesema wale ambao wamefika zaidi ya miaka sitini na tano sasa tutawaambia waondoke.

**Speaker:** Majaji hawa….(Inaudible)

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Ndio tumesema hivyo, ndio nakuambia nenda ukasome transition mechanism ninakuambia, tumeandika yote hayo.

**Speaker:** …(Inaudible)

**Com. Dr. Mohammed Swazuri:** Hapana, tumeweka hizi taratibu za kuondoa. Wale majaji ambao pia ni corrupt na incompetent tumeandika hapo, unataka zaidi ya vipi. Tumeandika hapo na maana ya corrupt na incompetent tunaijua, tumeshaandika hiyo ndio maana wakatushtaki kwa sababu hiyo unayosema wewe. Tulifanya exactly hivyo unavyosema ndio

maana tumeshtakiwa na majaji.

Elimu ya bure na mambo ya mishahara umesema haya itakuwaje. Ninafikiri tumeeleza katika transitional mechanims na Serikali zile za chini zitafanya hiyo kazi. Tume ya kuangalia bei, hii ni Tume ambayo hatujaiangalia kwa hivyo tutakwenda kuiangalia kwamba maskini ananunua mkate ule ule na tajiri na vipato vyao ni tofauti, haya hapo tunakubali.

Bwana Mwanjama amesema wafanyakazi kama mtu ame-retire basi mtoto au jamii yake, hilo sasa litategemea tajiri mwenyewe. Upande wa sports umesema kwamba hakuna haja ya kubaguana, Harambee Stars iwe na wachezaji kutoka kila mahali. Tumeandika lakini hatukuandika hilo neno hilo, tumesema kwamba kusiwe na ubaguzi. Mtu yoyote kama ni mchezaji mzuri atajulikana, kusiwe na ubaguzi kwamba huyu anatoka Pwani, asicheze yule anatoka Nyanza. Lakini ikiwa ni kweli ana haki ya kufanya anavyotaka Katiba imempa uhuru huyo kama ni mzuri ataonekana.

Wazee wapatiwe marupurupu, tumeitaja hiyo lakini indirectly kwamba wazee wana haki zao ambazo lazima watimiziwe wakifika umri wa miaka hamsini na tano na zaidi.

Tutaenda kuliangalia swala la social security, tumeandika hapa lakini itabindi tuliandike kwa uwazi zaidi. Vifaa vya Serikali kama magari, nyumba zinauzwa kiholela, hiyo iko tayana na ile haikutumika. Magari kwa mfano yanauzwa kwa bei ya chini sana na pia yanauzwa mtu na fulani hiyo si siri tunajua hiyo. Mwananchi wa kawaida ukitaka kuipata hiyo gari haupati, kwa hivyo sasa Serikali ya chini iko kuangalia. NGO's na CBO's, nafikiri NGO Act itabidi iangalie mpango huo.

Bwana Bwoga, kaya, kaya hazikutajwa katika Katiba. Jina hilo kaya haliko lakini ukiangalia section 324 inasema kwamba ardhi yote, community land ambayo ni ya kimila au ni ya kuabudu ni ya nani? Ni ya wananchi wenyewe, wataziangalia wenyewe hizo na kaya hazikutajwa majina. Hata section 239 (ii) pia imetaja sehemu ambazo wananchi watamiliki including sehemu ambazo ni shrines hizo ni kaya. Halafu akauliza, kuna ma-pajero mengi yanatoka bara sijui nitalijibu namna gain na sijui pesa hizo wanatoa wapi. Lakini pengine Serikali yetu itatusaidia hapa sasa kutengeneza pesa na sisi tuendeshe mapajero mengi.

Traditional courts, amesema kwamba tunataka mahakama zile za wazee, ukiangalia sura nambari 185, (iii) C, iko hiyo tumeweka traditional courts lakini kuna yale mambo ya kinyumbani, hizo tumezipatia nguvu pia.

Upande wa judiciary, halafu pesa za kilindini ulitaka ziletwe nyumbani, hatukusema, tumesema kwamba tumegawanya. Kuna national resources, vitu ambavyo ni provincial resources ni za province. Halafu tunaeleza vitu ambavyo ni district resources kwa hivyo vyote hivi vimeelezwa vitaganywa vipi. Zile percentages ndio hatukuaandika lakini tunasema wilaya itapata, mkoa utapata na nchi nzima itapata.

Suleiman Hassan:- nakubali kwamba gharama za kwuenda mahakamani ziko juu sana hilo ni swala ambalo ni lazima tuandike.

Tumeandika lakini lugha yetu haieleweki, tutaandika kwa ufazaha zaidi maanake hata kule kupeleka kuenda kusema ile kesi pia ni pesa.  Wewe umepigwa kisu lakini kama hauna shilingi mia tatu sasa yameisha pale pale.  Kwa hivyo tumesema mtu aruhusiwe kuweka hiyo, tumeandika kwanza a-file ile kesi yake basi hizo gharama ni baadaye, hiyo tumeweka.  Sasa tutaenda kusema kwamba ziwe zimepunguzwa.

Kadhi's Assistants, nafikiri sasa tumezungumza vizuri sana, ofisi ya Kadhi tumeirekebisha, majukumu yake tumeyaweka na hawa ni watu ambao ni wafanyi kazi.  Watachaguliwa na Judicial Service Commission, kwa hivyo mishahara yao automatically iko.

Halafu mzee wangu wa mwisho alisema maneno mawili mazito.  Wanyonge wapokonywa ardhi na maafisa makuu.  Hili ni swali ambalo tunasema limetoka huko, limekuja kwa Serikali ya wilaya na ya jimbo. Halafu bahari lisiwe limefungiwa, wawe wananchi wafanye wanavyotaka.  Sasa hiyo ni kazi ya Serikali ya nyumbanni, kwa hivyo uhuru ni wetu sasa.  Haya tutachukua watu wengine kumi wa mwisho, naona watu wanaanza kusinzia, njaa pia nayo.

**Mohammed Budzo:**  Kumi lakini tafadhali yule ambaye hajaongea.  Kumi ambao hawajaongea.

Wa kwanza ndugu yangu, wa pili, wa tatu, wa nne, wa tano, sita, saba, nane, tisa, kumi.  Kila mmoja ashike nambari yake vizuri.

**Swaleh Ali:**  Salaam Aleykum, kwa majina ni Swaleh Ali Mwamalumu.  Yangu mimi nafikiri nitazungumza maneno machache kwa sababu mengi yameshazungumzwa.  Kwanza naunga mkono Katiba hii ilioanzwa au ilioandikwa kiirafu.

Pili, nafikiri nimetatizika kidogo kwa Chairman alikuwa akizungumza baadhi ya maneno alikuwa akisema hilo liko lakini halitumiwi.  Hilo liko lakini halitumiwi, sasa sielewi kwa haya ambayo tunaandika pia yatakuwa yako katika kitabu lakini matumizi hakuna?  Hilo kidogo limetatanisha na ikiwa basi itakuwa baadhi za sheria itawekwa lakini hazitumiki, kuwa na uwezekano au katika Katiba hii iwe inawezekana.  Raia yeyote yule awe ana kibali akiona kitu au mfano mtumishi wa Serikali anaenda kinyume na kifungu cha Katiba inavyosema awe ana sheria ya kumchukulia hatua kali yoyote.

**Com. Mohammed Swazuri:**  Iko hiyo nimeandika hiyo, ama wewe unataka kuwa kuna mtu wa kuacha sheria, sheria inavunjwa na wewe unaona automatically, straight away, unaenda unashtaki.

**Swaleh Ali:**  Na kushtaki unashtaki wapi?

**Com. Mohammed Swazuri:**  Kuna ofisi maalum ya kuenda, si kwa polisi tena.  Jingine?

**Swaleh Ali:** Na jinginelo, mengi yamezungumzwa lakini nitasema katika ardhi zilizoko ziwe, tittle deed zote zimetolewa ziwekwe…….. Zote yaani zipigwe marufuku zote, zisitumike zote halafu baada zikipigwa uchaguzi ule ambao Katiba umezungumza uishe. Huo ndipo tutaangalia ni kuchukua title deed au kuwe tutafanya taratibu gani zinginezo.

Pili, la kumalizia nafikiri ofisi ya Kadhi sikuona kitabu kusema kuwa je, ina zaidi ya kesi au kesi ni zile zile mbaili au tatu ziliwekwa, urithi na nini. Hapo pia sijajua kwa sababu yangu nilizungumza kuwa au Chief Kadhi ana uwezo wa kuamua kesi aina yoyote iwe tu yule mlalamishi. Nikiamua kuwa kesi yangu nataka nipeleke ofisi ya Kadhi au atamshtaki mtu wake na ofisi ya Kadhi kwa kesi yoyote ule ni waamuzi ile ya Kiislamu huu utapitishwa na utafanywe tu huo bila kuingiliwa na mambo yoyote. Hapo hapo Salaam Aleykum Chairman.

**Mohammed Budzo:** Wa pili.

**Bakari Mohammed Bundo:** Kwa jina mimi Bakari Mohammed Bundo, Nitachangia hii Kaitba tunafanya kwa muda mrefu, wafanyaje vibarua katika kule beach au mahali popote. Wahindi wanaandika watu vibarua na mtu huyo huyo anapanguka kutoka juu either avunjike vunjike au afe laki

Ni tajiri hamtambui kama huyo ni banadamu. Atatoka hivyo hivyo akijingusha mwenyewe hatalipwa chochote. Hilo naona ni maadhulumu upande wangu mimi kwa sababu hakukataa kubiridikwa kazi ya mwezi isipokuwa kazi yake ni ile ya kibarua na amepata hasara juu ya hiyo kazi hiyo hiyo. Kama ni kwa Muhindi au Mzungu lakini hapa Kenya mtu wa kibarua huwa hatambuliwi, kwa hivyo ningeomba atambuliwe mtu kama huyo anapopata hasara au ni binadamu hawezi kuangaliwa shida zake.

Jambo lingine, tunashikwa hapa na polisi kna makosa madogo madogo, makosa yale matu anaweza kupewa free bond afe nyumbani halafu kesho aende kotini lakini hapo huwa mtu anawekwa tu mpaka utoke kitu kidogo ndiyo uachiliwe. Hii kitu inatuumiza hasa mimi nwenyewe nazungumza, kushikwa kwa mtu si kwa makoso madogo, kwa mfano kushikwa na vinyagu. Anauza mali yake vinyagu hii mkosa madogo lakini badala apewe free bond aende kotini anawekwa pale ndani. Sasa hiii inatuumiza na ambalo si kosa kubwa ambalo hawezi kutoroka, ambalo ni kosa la kawaida kwa hivyo jambo hili naliomba lishughulikiwe sana.

Jambo la tatu, ngoja kidogo madam. Tunapelekwa kortini, kesi hiyo ni ndogo baada ya kujitetea kusema mimi hayo maneno sikufanya. Unataka uje ueleze ukweli unawekwa rumande hata mwezi mzima au miezi miwili. Kesi ukija ukiulizwa baada ya mwezi kumalizika ukirudi kortini ukuulizwa swali hilo ukikataa unarudishwa tena kortini mpaka inakulazimu mtu kukubali useme ni kweli, sasa hiyo ni maneno makubwa sana. Tafadhali kidonda kama hicho kitafutiwe dawa.

Narudia tena upande wa polisi, tunaona mtu anaposhikwa awe na mtu anaweza kuangalia ule uzito, pawe na mtu pale anaweza

kuangalia uzito wa raia naona hii kikosi ni ya kimaana sana au si jambo la muhimu mtu aweze kuachiliwa si kujengewa orundo orundo tu hiyo ni kuumizana. Yangu ni hayo machache

**Mohammed Budzo:** Nambari tatu.

**Rashid Mmemo:** Ndugu Salaam Aleykum.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Rashid Mmemo:** Mimi maoni yangu, ooh, jina ni Rashid Omar Mmemo. Maoni ni kwamba hata mimi ningefurahia iwapo mabilioni yetu imetumika katika Tume hii ya Katiba, na wakati ikiwa wametukamilishia shuguli yetu hii ingekuwa bora ikiwa tutafanya ule uchaguzi wetu kwa Katiba yetu hii. Hayo ndio malengo yetu. Ni hilo fupi.

Lingine ni kuhusu wizara ya afya na madaktari wake. Ukweli ni kwamba mahospitali mengi hasa hapa Msambweni unaweza kifika hapo ukapata hata mpira ule wenyewe wa kutolea damu ukweli ukanunua, hali ya kwamba unaposhikwa na polisi ule pingu unazofungiwa hukununua mwenyewe na ile rungu utakapopigiwa hakuna rungu utakaonunua, lakini katika Wizara hii ya Afya kila kitu utakapotumia pale utajifanyia mwenyewe. Lakini mimi naona sababu wote wanachangia hivyo ni kuhusu hizi clinics za private kwa sababu ukifika pale utapata kila muuguzi nyumbani ako na clinic yake. Hivyo mimi ningeonelea vile kuliundwa Tume za kila aina uundwe Tume ambayo hua nayo itashugulikia kupeana vibali kwa hawa madaktari na kuchunguza jinsi dawa inavyochugulia.

Pengine nikimalizia ni kwamba katika nchi yetu hii uhalalisha ulevi fulani kuwa ni halali na pombe zingine ni haramu ilhali nafikiri zote hizo hakuna pombe ambayo ni halali. Hivyo basi katika Katiba hiyo ikiwa inaruhusu ziwe pombe zote zitakuwa halali na ikiwa ni kuharamisha hizo zote zitakuwa haramu. Ni hayo machache, asanteni.

**Kassim Hassan Yanga:** Kwa jina ni Kassim Hassan Yangu. Maombi yangu nililonalo nafikiri wakati tulipigiwa mbiu ya kunakuja katiba au unakuja Commissioner wa Katiba kama Bwana Ghai kuuliza maoni ya wananchi wanatakaje, nafikiri Bwana Ghai alitumwa na Serikali kutafuta maoni ya raia au ya wananchi na hukusita ulikuja hapa hapa kwa mwembe huu huu. Tulizungumizia mambo ya Katiba nafikiri pia tukauliza Bwana Ghai hayo mambo ni ya ukweli au watafuta mbinu zetu hao wananchi wanasema nini halafu.

**(Interjection).**

**Speaker:** (Inaudible).

**Kassim Hassan Yanga:** Haya, ndiye huyu pia Bwana Swazuri tukamuuliza haya maoni yaliotuleta hapa ni ya ukweli au unatafuta undani wetu ujue hawa watu wanasema nini. Ukasema aah, mimi nilikuja kutengeneza Katiba kulingana na watu wanalalamika, watu wanalalamika, wa upinzani wanataka vifungu vibadilishwe kwa hivyo nimekuja kutafuta maoni kwa nyinyi wananchi raia nafikiri watu walichangia sana. Mimi maoni yangu nataka hivi, ikiwa Serikali ilituma maoni ya Katiba ibadilishwe na punde si punde unakuta kwa gazeti huyo huyo anatuma Katiba ibadilishwe kama Raisi amekataa Katiba hii itumike anataka ile ile yake anayotaka. Je, mambo haya yatakuwaje na ikiwa atakataa hii tuliokubaliana nayo sisi, sisi tuna haki nasi tukatae tutapiga kura? Kwa hivyo maoni yangu nasema, ikiwa hata kubali mtaro huu uliozungumziwa na uma wa watu basi sisi hatutapiga kura na kadi ya zamani, tunataka kadi hii hii mpya ambayo tumeletewa tupige nayo kura la si hivyo tunakataa. Kwa hayo machache asante sana.

**Peter Chani:** Commissioner wa kurekebisha Katiba, Bwana Swazuri, maofisa wenzake, wananchi wenzangu habari zenu. Yangu ni machache, nashukuru baada ya sisi kutoa maoni yetu juu ya kurekebishwa kwa Katiba mambo mengi wananchi walioyasema kuanzia yale nilioyoyatoa hapo ijapo siku hiyo sikuzungumza yamewekwa kwenye Katiba mpya. Kwanza jina ni Peter Chania mfanyibiashara hapa na pia ni mkaazi wa Kwale Simba nne.

Nimeanza na kuwapongeza kwamba kinyume cha yale yanaoongewa kwamba mambo yala ambayo yamechapishwa kwa magazeti kwamba ni mambo yenu si kweli, wananchi ni yale ambao wamependekeza kuanzia yale niliowapatia written presentation mengi yake yako na nashukuru. Kwa hivyo pongezi sana kwa hayo na naomba katika hilo jambo ikiwezekana Rais mpya ambaye atachaguliwa katika Katiba mpya ama chini ya Katiba mpya aweze kuwatumikia national honours nyinyi ma-Commissioners nyote badala wa waizi kuona katika sherehe ya kitaifa wakitunukiwa mambo ama shaada ama zawazi kwa mambo ambayo hawajafanyia taifa hili. Hiyo ni kwa njia ya kushukukuru au kuwashukuru kwa yale yote ambayo mumeweza kujinyima, na pia kutumia wakati wenu kuweza kutekeleza katika historia ya maendeleo ya Katiba katika nchi hii. Na pia ikiwa kuna watu ambao wamefanya mambo muhimu ambao mtaweza kuwatambua pia mnaweza kuwapatia certificate of appreciation.

Point yangu ya kwanza ni kama reaction kutokana na baadhi ya mambo ambayo yametajwa haswa juu ya Katiba mpya, je tuende kwa kura na Katiba ya zamani ama mpya. Moja ambalo pia napenda kusema ni kwamba Raisi anapoapishwa hua anahapa kwamba atalinda Katiba na tukifanya makosa ya mumuhapisha Rais kwa Katiba ya zamani siku ambapo anaambiwa sasa chukua uskani wa Kenya. Kwa miaka mitano atahakikisha atalinda ilinda ile ile Katiba ambao ameingia nayo na hicho ndicho kitu kinamsumbua Moi. Tusimlaumu sana, yeye alinde hiyo hiyo na aendelee na hiyo hiyo ya zamani lakini tusithubutu kumpatia Katiba ya zamani Raisi mpya basi tutakuwa tumejiingiza kwenye shida ambayo itakuwa ngumu kutoa maanake amehapa mbele yetu wananchi na mbele ya Mungu kwamba atailinda hiyo Katiba hamwezi kumwambia baada ya wiki mbili badilisha kwa hivyo yangu ni kusema kwamba uchaguzi na Katiba mpya.

Ninapendekeza kwa training ijapo nafanya biashara sasa ni mwalimu na napendekeza katika vyuo vyetu vyote kuanzia primary,

secondary, university na teritiary institututions kama hiki chuo hapa pawe na mafunzo ya Constitution. Ninaelewa kwamba nchi fulani fulani katika Afrika ziliweza kumiliki Katiba nzuri sana kama Nigeria na nchi zingine lakini, kwa sababu ya ujuaji mwingi na mambo mengi kama hayo, ijapo Katiba ni nzuri na kuwa haikubaliki ama watu hawaielewi basi wameishia mizozo na ikawa ni vita. Kwa hivyo kuwezesha jamii ya Mkenya ama Wakenya waweze kuelewa Katiba yao itabidi waikubali na kuikubali ni mtoto akiwa mdogo vile anaanza kufunzwa Quran ama Bibilia pia Katiba ya nchi yake aielewe, hivyo ndivyo itafanya aikubali au anaiheshimu, au anaifuata na hatakuwa ni mtu wa kupelekwa pale polisi tuende tukamtoe tumlipie bond na vitu vingine. Kwa hivyo nimependekewa kwamba tuwe na support subject hata kama si somo hasa lakini iwe kama somo la ziada, support subject katika levels zote za elimu, hiyo itasaidia sana kuweza kufanya wananchi waweze kueshimu Katiba yao na tutaanza kuishi kwa umoja.

Ile nyingine ni shida ya umaskini, nafikiri mengi yametajwa na nafurahi maanake nimekuja kuchelewa Bwana Swazuri amefafanua kwamba tutakuwa na distribution yaani magawanyiko ama kugawanya vizuri mapato ya kitaifa hasa mali ya taifa. Lakini nilikuwa napendekeza Central Bank iwe decentralized kama vile politics, mambo ya siasa uongozi wa kisiasa utakuwa decentralized mpaka district level pia Central Bank iwe ni hivyo hiyo ndio hizi pesa tunazolilia zinazotoka kwa hoteli na kuenda direct kwa consolidated fund huko Nairobi na ziwe signatory ni watu wawili, President na Minister. Basi iwe iko benki inayo-receive hizo pesa hapa na zile za hapa zinabaki hapa hapa, zile chache za kuenda mbele zinaenda mbele. Nafikiri hiyo itasaidia kuweza kutoa mikopo humu humu na pesa zinazotoka humu humu zinaendeleza humu humu.

Ile nyingine ni shida inahusiana na ukabila, ninapendekeza kuanzia January mwaka ujao iwe labda sheria ikiwezekana kwamba hatutaruhusu mtu yeyote ambaye alioa baada ya January mwaka ujao kuweza kuongoza hii nchi ikiwa hajui ama haelewi wananchi wa kabila zingine. Na labda nina pendekezo kama hili maanake nimeona nchi kama Brazil wao sijui walifanyaje lakini ukiangalia picha ya wachezaji wa Brazil utaoni si Mwaafrika wala si Muhindi wala si Mzungu, nasikia ni kama wame-cross breed yaani wameoana na kuchanganyikana. Nasikia pia Zanzibari ni kama walifanya hivyo, Waarabu na Waafrika wa huko kwa hivyo sasa imekuwa hata rangi si hoja watu wote wanaongea lugha moja, ngozi pia hakuna tofauti na mambo ya aibu kama hizo Bwana Swazuri ametaja.

Kwa hivyo nilikuwa napendekeza labda baada ya miaka ama katika miaka ijao iwe yoyote hataruhusiwa kuongoza Kenya ikiwa ameoa mtu wa kabila yake maanake ndio akisimama kila wakati anasema mambo ya kabila yake, anaongea kikabila yake na kadhalika. Yaani Mkikuya anajua Wakikuyu, Mkalenjina anajua wakalenjia, Mjaluo anajua Wajaluo, iwe tuna-mix yaani tunachanganyikana sisi kwa sisi. Watu wengi wakistarabika wanaoa Mzungu ama mtu wa nje lakini inakuwa ni jirani yako ambao mmepakana pia hamwelewi. Kwale hapa watu wemeingiliana vizuri sana na nafurahia sana, wameoana wao kwa wao mpaka mambo ya ukabila hata inapungua sana. Kwa hivyo, ikiwa sisi tunaweza kutangamana kwa njia hiyo pia yoyote asiruhusiwe kuongoza hii nchi ikiwa ameoa mtu tu wa kabiala yake maanake mtu kama huyo atatuingiza kwa shida. Asante.

**Jasho Mwadarashe:** Mimi jina ni Jasho Mwadarashe. Mimi hoja yangu ni kuchangia kidogo tena naona haziko katika

sehemu kubwa ni katika hii sehemu yetu ya Kwale ama kwa mkoa wa Kwale kwa jumla. Kwanza ningependekeza katika Wilaya ya Kwale, hii Wilaya ni kubwa sana maskini wanapata taabu kuenda Kwale, mtu anatoka Taru mpaka Kwale, mtu anatoka Banga mpaka Kwale, mtu anatoka huko Kilimagodho mbali kabisa. Ningependekeza katika Kwale iwe na district tatu kama Kinango, Kwale na Msambweni ili kupunguza zile msafara na ni sehemu kubwa ambayo ingetoshea kama sehemu nyingine ambazo ni ndogo na zina district zile zile nyingi. Kwa hivyo napendekeza Kwale iwe na district tatu.

Swali la pili ni kwamba katika mkoa huu kuhusu shida za wakulima kupata mkopo ya kawaida, kwanza wakulima hawajulikani kama wanalima nini na vile vile maofisa wa agriculture wamepotea hatuwajuhi na ukilima umekuwa hasifu na haueleweki kama zamani. Zamani ulikuwa ukitafua mtu wa agriculture utampata, siku hizi humjuhi anafanya kazi gani na wala yuko wapo hayo mashamba yenyewe pia hayaangaliwi na mtu huyo anapata mshahara na tunaona hiyo pia ni shida.

Swala la tatu, nafikiri mengine yameongewa kuhusu mambo ya mahospitali, cost sharing. Hii mambo yametia watu wanakufa na ugonjwa ndogo ndogo siku hizi sasa ukifika huko KD utapata watu kama tisa na wagonjwa kwa zaidi ya mia mbili wamelala nyumbani hawana pesa za kuenda hospitalini. Ningeomba hiyo idara ya hospitali iwe kama zile zile zamana madawa yawe free maanake watu siku hizi wanakufa na magonjwa kidogo kidogo kwa sababu ya gharama ya utabibu baada ya shilling hamsini imekuwa hata mia mbili. Unatibiwa private mia mbili, unakwenda KD unatibiwa mia tatu hio ni kama kutuumiza, kama unyanyasaji, kama kutuuibia.

Mwisho ni bahari hii kubwa tena namba….bahari hii tunaona katika sisi watu wa sehemu ya Pwani tuna bahari ya kutoka Kiunga mpaka Vanga na hii Bahari tumeambiwa na Serikali tukipasua hivi ni mile mia mbili ambapo ni kutoka hapa mpaka Mtito Andei pia kuwe karibu na tunajua kwamba kuna mikopo ya uvuvi. Kuna mikopo tumeambiwa Serikali inaweza kutoa pesa za mikopo na mashirika, tumeambiwa kuna zaidi ya bilioni kumi na mbili zimeletewa watu wa Pwani katika Bahari kubwa wanunue mashua, wanunue nyavu, wanunue mishipi. Maanake ni taabu kama sisi tuna bahari na tunakula sukuma wiki, tunapata taabu na huku bahari tunaambiwa tuachie Wazungu iwe kioo.

Tungeomba ikiwezekana Serikali itukubalie tupate ile mikopo ya mashua kubwa ya kuvua maji mengi huko maili mia mbili tufike, sio hapa hapa tu tukisumbuana. Tukifika maili mia mile huku tukiwa na mashua kubwa h……hasara kidogo hapa karibu sio lazima, tutakwenda wote huko. Kwa hivyo hiyo nafasi iko maanake hatuwezi kupata uhuru tunavua mile matano, mile sita, mile kumi na hapa kuna mile mia moja tisaini yamebakia. Huko tunaona kuna Wakorea wanakuja kufanya huduma ya bahari ya Kenya na wakichumia Kenya bahari. Kwa hivyo nataka hii bahari tuvue wenyewe kutoka huko mpaka huko, kutoka Lamu mpaka huku tuvue mile mia mbili na tumekubali pia kulipia mikopo tukipatiwa zile mashua kubwa.

Ya mwisho ni kuwa tunaomba wakati wa kupimwa sehemu ya kule beach kulikuwa kuna road reserve, zile road reserve zimeuzwa tunaambiwa zimeuzwa na watumishi wa Serikali na viongozi, wanasiasa. Kwa nini wazee wetu sasa akitaka kuenda baharini azunguke kutoka huko mpaka apite huko hakuna njia, arudie huko mpaka afike huko sijui Mwepe hakuna njia na hizi

barabara zilikuwa kwa watu kufika baharini ni taabu. Kwa hivyo tunataka zile njia zote zipasuliwe watu waende baharini, akitaka mtu anakuenda baharini kuangalia bahari asipotaka na mgeni wake anakwenda baharini mara moja kuliko kufungwa zote na kuuzwa na watu waliouza. Wale ambao tumewachagua watutumikie, wakijulikana ni watumishi wa Serikali wanatufanyia makosa maanake bababara zote kwenye rahamani zipasuliwe. (Murmurs in the background – Inaudible)

**Rashid Mwakuguzwa:** Asante sana Bwana Swazuri Commissioner wetu, maofisa, mabibi na mabwana. Asaalam Aleykum. Kwanza nashukuru sana kwa Katiba ambayo saa hii tunaijadili mara ya pili na ninaomba iweze mambo yawe sawa sawa tuje tupige kura na Katiba yetu mpya.

Kwa jina naitwa Radhi Juma Mapambo Mwakuguzwa. Neno langu la kwanza, ninaomba Tume ya Katiba kupitia registrar wa vyama vya political parties. Nasema kwamba vyama vipunguzwe na vyama ni arubaine na mbili ama na tano lakini nataka viwe vinane yaani kila Mkoa uwe na chama chake. Kuanzia arubaine na tano huko mpaka vinane, viwe vinane tu.

Ya pili, kila chama kina manifesto yake ooh, mimi nikichaguliwa nikuwa na ma-Prime Minister wangapi, lakini nasema kwamba kwa sababu ya kuwa Katiba imeeleza kila kitu kulingana na administration. Upande yote immeleza kila kitu, kile chama ambacho kitaingia kwa Serikali ifuate hiyo Katiba sio ya mambo ya kuwa ati mimi nitakuwa President nitachagua hivi hivi hapana kwa sababu tumepoteza pesa mingi na Katiba imemaliza kila kitu. Mambo yote ifuate vile vile Katiba inavyotaka hapana kuongeza mambo yao hapa.

Halafu upande wa refugees, kuna desturi ya kuwa kumekuwa na fujo hapa nchini sasa badala ya kuwa mtu anafujo amekimbilia nchi nyingine usalama anafuatwa huko huko, unaletwa tena huku. Sasa wewe mwenyewe umekimbilia usalama tena unarudishwa tena huko, kwa hivyo hicho kifungu cha refugees nasema kwamba mtu akikimbia amekimbia usalama wa maisha yake sio arudishwe tena pale chini.

**Com. Mohammed Swazuri:** …(Inaudible)

**Rashid Mwakuguzwa:** Kutoka Kenya, kwa mfano kutoka Kenya kuenda kama Tanzania ama kuenda Uganda, iwe ni sheria kuwa mtu akikimbia amekimbilia usalama wake.

Halafu upande wa international laws, tumesema kwamba tumegawanya mamlaka from kijiji mpaka headquarter, kwa hivyo kulingana na hii mikopo nasema kwamba kama ni jimbo kwa mfano hapa Coast, na kulingana na kuwa jimbo hilo litahusika na mambo yote, wilaya ikihusika na mambo yote sasa vipewe kipawa mbele kwamba vinaomba mikopo kulingana na ile nchi wenyewe ni marafiki nayo. Kama mimi na rafiki ya Mjerumani, Coast kwa mfano ni rafiki wa Mjerumani aombe straight na hiyo mkopo ije straight kwa hiyo province badala iende headquater huko itagawanywa gawanywa. Ije hapa kwanza ifanye mambo zao na watalipa wenyewe sio iende huko. Kama ni hiyo mambo regional iwe ni ya regional si mambo ya regional tena

ipelekwe huko headquater. Kwa hayo machache nafikiri yatosha.

**Mohammed Mwambiti:** Asaalam Aleykum.

**Audience:** Aleykum Salaam.

**Mohammed Mwambiti:** Jina ni Mohammed Bakari Mwambiti, mimi langu ni swali, katika sehemu za hivi ardhi kuna kitu kinaitwa squatter, squatter ni kitu sisi hatukijuhi. Squatter ni mtu wa kuzaliwa hapa ama squatter ni mtu wa kuja kutoka sehemu nyingine. Hiyo ni moja.

Ya pili pia ninashukurani leo nimevishwa hili shaada hapa lakini silielewi ile nimevaa nia sijui inaeleza nini katika ukivaa hichi kitambara cha yellow. Hilo lazima tuelimishwe pia maana kinaweza kuwa kina maana yake.

La tatu, sisi katika Katiba yetu inalilia jimbo na wananchi wote wanalilia jimbo lakini kuna watu wengine ambao wamelewa na Serikali ya KANU, na ni maofisa hasa kuhusu hapa Pwani wako. Kuhusu Wabunge wetu wa hapa Pwani hata mavifu wa hapa Pwani ukieleza kitu jimbo watu wao na vyama ni village huwa watu wanakunja uso kuangalia baharini au kuangalia bara. Hili jimbo sisi twalitaka kweli lakini kunao wenzetu waliopigwa shindani na KANU, hiyo maneno hayaingii kwa akili zao. Kwa hivyo mimi sina zaidi yangu ilikuwa ni hayo matatu.

**Com. Mohammed Swazuri:** Maoni yako ilikuwa vipi.

**Mohammed Mwambiti:** Maoni yangu mimi nataka wale viongozi wa hapa na wale Wabunge wa hapa Pwani waungane na Katiba yetu mpya vile watu wakizungumza nao waseme hiyo ni sawa katika maoni yangu.

**Mohammed Budzo:** Tisa.

**Ramadhan Dzitsai:** Mimi naitwa Ramadhan Juma Dzitai ndio naroga sana hawa watu. Jambo la kwanza, yamezungumzwa mengi sana lakini nitarudia nyuma kulingana na vile wakati nilivyozaliwa nilioyaona na ninavyoyaona sasa.

Jambo la kwanza nagombania hali nilivyoiona, nikiwa ni mtu na adabu zangu na tayari ambapo nilikuwa hata nimeshazaa na naingilia land. Mambo ya land tumeletewa kwamba ardhi zipimwe na sisi watu wa Pwani hatukujua maana ya ardhi kupimwa ni nini. Tulikubali tu ukweli tupime ardhi lakini kumbe ilikuwa ni ubovu wa kuHaribiwa sisi akili tutete mjomba na mwana na baba na ndugu mpaka dakika hii tunagombana. Kwa hivyo naona chochote kile ambacho tunazungumza hakitakuwa sawa mapendekezo yangu mimi nasema, hii land ilikuwa ni ya watu binafsi. Nasema kuanzia hivi kwamba mapendekezo yangu mimi ila lingeondolewa mbali yote ya Kenya hata ya Coast kwa sababu tuna madhulumu makubwa yaliofanywA. ***(Applause)***

Nikianzia hivyo jambo hili halikutokana na Pwani ya kuwa ardhi zipimwe, ilitoka huko huko kwa uwizi kwamba kulikuwa na lease zilizokuwa na uingereza. Baada ya kupata uhuru walipiga picha wakakuta hizi ardhi tutaziiba kivipi ndio wakaleta mambo ya kuwa ardhi zipimwe. Ikiwa basi ni ardhi kupimwa tumepata uhuru kwa nini zile ambazo zilikuwa za lease na sisi wenyewe zilizuiliwa mpaka sasa wakapeana wao, wakafukuza Wazungu ambao walikuwa wakipatia watu makazi wakachukua wao wakawa ni zao halafu wanasema kwamba wameuziwa. Wameuziwa na akina nani kwa sababu yule Mzungu aliishi hapa kwa sababu ya lease hakununua. Je, Serikali yetu ya KANU yasema wale wakina Matiba walinunua wakamnyan'ganya Dena, na Dena hakuuziwa alikuwa akitumia lease? Je, tukimwambia Matiba atupe ile karatasi aliyemuuzia ardhi hii ya hapa atatupatia? Hana, kwa hivyo sababu yenyewe nizema hiyo land ifutiwe mbali zote. Badala ya kupata ardhi yetu ama Pwani yetu, jimbo letu ikiwa kuna haki ya kwamba tugawanye ardhi zetu tutazigawanya kuanzia beach, tutajua hapa ni kwa nani.

Pili, hilo hilo uwizi huo huo viongozi wetu wakaona ni sawa, kuna watu kama mimi nilipewa sehemu na babake huyu nilime ama kupewa mahali na babake huyu nifanye biashara, wakati huo huo nilikuwa mimi niko kwangu tayari yule aliyenipatia ni mjinga. Kwa hivyo hayo madhulumu hayana Wakikuyu peke yake mpaka sisi wenyewe tumedhulumiana, na ndio maana nikasema huu tuliofanywa hautamalizika kwa sababu mimi nilimuibia wewe kwa sababu babako alinipatia mali nijenge utezi, wakati mpimo ilivyokuja tayari nilipima kwa sababu baba yangu alikufa wewe wanyakua hiyo ardhi. Je, ni haki ikiwa sisi Waislamu?

Jingine cha kuchangia kabisa ni kwamba hakuna ambayo itawezekaniwa ila ni jimbo letu kwanza tulipate halafu hiyo mikataba ndio itakuwa, lakini kabla ya jimbo kupatikaniwa halafu ndio tukakaa tukafanya hii mikakazi yetu itakuwa ni nyimbo tu.

**Com. Mohammed Swazuri:** Si jimbo liko lakini…(Inaudible)

**Ramadhan Dzitsai:** Sasa ikiwa lipo ni jimbo sisi wenyewe kwa nini twasumbuana. Wewe wataka mwengina anasema sitakitutaenda wapi maanake jimbo tunalo, wewe wasema ndio, huyu anasema hatuliwezi …(vernacular) sasa huyo ni mgonjwa ama ni mzima?

**Com. Mohammed Swazuri:** Sasa hayo ni maneno yetu ambayo sisi wenyewe tutakaa lakini ujue ni kwamba lipo.

**Ramadhan Dzitsai:** Lipo.

**Com. Mohammed Swazuri:** Eeeh.

**Ramadhan Dzitsai:** Basi ikiwa lipo lazima tuwe pamoja watu wa Pwani wote. Kitu kingine naongezea hapo. Wakati walivyopata uhuru kuna sauti moja ilivyotoka mama ninavyosema. Serikali ya Kenya iliahidi maneno kwamba kuna wazee walioenda vitani, ulileta huo mlolongo kwamba mwandikishe majina ya wazee wa Kidigo. Wale walio Pwani nzima

waliokwenda vitani kuna pesa wataka kulipwa, hizo pesa hazikutoka mpaka sasa na watu walienda wakafa ama walienda wakafanya kazi na hawajalipwa mpaka sasa.

Pili, kuna wengineo waliongea kwamba wazee wapewe marupu rupu. Ikiwa tuna umoja kweli, na watu wote wako sawa, sisi ingawa tunaitia faida kubwa sisi ambao hatuna makazi sio tupewe marupurupu hapa. Tulipwe kama mfanyajikazi.

**Com. Mohammed Swazuri:** Haya, sawa tumeelewa.

**Radhid Dzitsai:** Tumeelewa, hiyo yatosha. Asante.

**Mohammed Budzo:** Kumi. Ni wa tisa, kumi ni wewe.

**Mohammed Mwachaunga:** Mimi naitwa Mohammed Said Mwachaunga kwetu ni Diani mimi niko kwenye ardhi. Ardhi wakati wa 1972 ilipimwa na kulikuwa na Act, Act yenyewe ni section 300, Act section (iv). Hii section ndio iliyotuibia mashamba na hii section nilikuambia Bwana Swazuri wakati ule wa Commission, hii section iondolewe kwa sababu hii section ndio inaleta matatizo katika mashamba.

**Com. Mohammed Swazuri:** Section gani sasa?

**Mohammed Mwachaunga:** Registered Land Act halafu kuna registered land act pia ya Commission.

**Com. Mohammed Swazuri:** Ingine.

**Mohammed Mwachaunga:** Kuna registered land ya Commission pia 280 na 281 hizi zinatakikana pia ziondolewe kwa sababu hizi ndizo Commission inatoa title deed huko inakuja huku kuchukua mashamba yetu.

Swali la nne nikuambie ni mambo ya ardhi ya lease, ardhi ya lease wazee walikodisha hawakuuza na hilo swali naregesha tena kwamba wazee wa zamani 1914 tarehe moshi mwezi wa pili. 1914, hii record iliwekwa kwa agreement na wazee na nawajua majina yao, mwambie Serikali ya KANU kwamba wa Pwani wamesinywe, hizi ardhi zetu ambazo zote zilikuwa leased tunazitaka maanake tulikodisha kwa 99 years. Kwa hivyo hizi ardhi lazima zitolewe kwa mkataba na wazee wetu tunawajua na tunaomakaratasi hata wewe nilikupatia. Kwa hivyo nakuambia kwamba wa Pwani wamesinywe na tunataka jimbo letu mambo mengine hatutaki. Yangu ni hayo matatu tu, sina mengi lakini nawauliza sheria lazima ifadhiwe.

**Cllr. Mohammed Budzo:** Basi kwa wale ambao wamechelewa mimi jina langu naitwa Mohammed Budzo, Councillor wa Kinondo. Niko na maoni mawili ambayo nitaanzia, moja ni la elimu. Maoni yangu katika kuchangia hii Katiba ningependelea

kwanza ule mfumo wa elimu wa zamani wa darasa la saba, kidato cha kwanza hadi cha nne, halafu vidato viwili cha tano na cha sita, halafu na university viregelewe na kwa masharti. Masharti yake ambayo ningependa kuingiza kwa Katiba mpya ni kwamba kusiweko na mtiani kuanzia darasa la saba hati hiyo form four na form five na huko kwingineko. Kwa sababu Serikali wakati ikifanya mtiani mfano wa darasa la saba hawa watoto ambao wameanguka huwa Serikali imewapangia kitu gani ikiwa kweli tunaangalia masilahi ya watoto, wale wato walioanguka mara nyingi wanawachiwa pale na wanazidi yaani uwa imehesabiwa kwamba maisha yao yameisha wataishilia hapo hapo hawajaangaliwa baada ya kuanguka wafanyiwe nini. Ndiposa naomba…

Lakini kwa technical services huyu mtoto ni mzuri ni vile tu uchunguzi haujafanywa. Kuna watoto wengine madutu sana lakini ukiwaweka uwanjani mtoto huyu ni mzuri. Kwa hivyo zile talents zao ni Serikali hazijagundua kwamba huyu mtoto huyu yuko na talent gani, kwa hivyo ndio nilikuwa nasema waanzie darasa la kwanza bila mtihani mpaka university. Sasa yule anayetaka kuchukua course ya somo lake mwenyewe aanze hapo, ikiwa ni udaktari uanze hapo akishafika university sasa apatiwe miaka mitano ya huo udaktari lakini hii academic qualification iwe kila mmoja anapatiwa nafasi ya kuenda university. Hilo ni chango la kwanza, daktari anasema nienda haraka haraka.

Chango langu la pili ni kwa upande wa majimbo, tumeambiwa na tumesoma kwamba yale majimbo tunayotaka tumepatiwa isipokuwa mimi naona uwakilishi wa jimbo kulingana na wenzetu ma-Commissioners walivyopanga. Kwa maoni ya watu mimi binafsi maoni yangu, wawakilishi wa jimbo wanavyochaguliwa sikupendelea kwa sababu ilivyo nafikiri ikiwa sijakosea ni kwamba kila wilaya itatoa representative wawili ambao watachaguliwa na waakilishi wa mabaraza ama madiwani. Ningependelea maoni kwamba Wabunge wale wa jimbo wawe wanachaguliwa na wananchi na kwa idadi ya kila constituency uwe kuna wawakilishi wasiozidi watatu ili kila constituency iwakilishwe katika jimbo lakini wasiwe watu wawili wanachukuliwa kwa district wanaenda huko. Kwa mfano district yetu iko na division tano, asipochaguliwa mmoja wao katika Msambweni division itakuwa hii Mswambweni Division haina uwakilishi. Kwa hivyo ni kila constituency kwa maoni yangu ichague wenyewe Mjumbe wa baraza la mkoa. Asanteni.

**Com. Mohammed Swazuri:** Nafikiri maswala ambayo yameulizwa katika huu mkondo wa mwisho karibu mengi tumeshayajibu lakini tutazidi kueleza ili watu waelewe zaidi. Kwanza ni mambo ya title deed, Bwana Swaleh amependekeza kwamba title deeds tuondoe zote tuanze a-fresh. Hilo hatuwezi kusema inawezekana moja kwa moja lakini tumesema kwamba tutachunguza. Ukisoma kifungu hicho cha ardhi kimesema tutachunguza ikiwa kwa mfano ardhi ambazo ni za Serikali za uma hiyo automatically tutaondoa tuchunguze wale ambao wamenyakua ili tuwapokonye, lakini kwa hizi za private hiyo hatujasema na itakuwa ni vigumu sana kwa sasa kufanya hivyo lakini tutaenda kujadiliana zaidi.

Ofisi ya Kadhi, nafikiri majukumu yake tumeyaeleza vizuri kwamba sasa ukiangalia kifungu nambari mia mbili, nitakusomea namba mia mbili. Inasema kwamba, mahakama ya Kadhi ya Kiislamu sasa itaangalia maswala ya kibinafsi – personal status, marriage- ndoa, divorce – talaka, mambo ya urithi baada ya talaka, mambo ya urithi – inheritence halafu na mambo ambayo

yanayowahusu Waislamu. Halafu pili ikasema mahakama ya Kadhi itaangalia civil and commercial cases, kwa hivyo maswala ya biashara pia sasa yameingia pale si yale ya mwanzo peke yake pia maswala ya biashara yameingia pale. Halafu pia tumesema Kadhi pia ataangalia maswala ya mali zinazohusiana na wakfu. Zamani walikuwa hawahusiki ilikuwa mambo ya public trustees sasa limerudishwa kwa upande wa Waislamu kwa hivyo tumepanua, tumeongeza kazi za hakimu wa Kiislamu.

Bwana Bundo akaeleza kuhusu wafanyakazi, wafanyakazi wale ambao ni wa vibarua huwa wananyanyaswa, hilo tumeshalisema pale mwanzo tumeshalijibu kwamba sasa wafanyakazi wote tumewapatia haki zao. Mambo ya polisi kuwashika watu vibaya tumeshaeleza, hongo tumeshaeleza na polisi, nafikiri nilikuwa nimeshajibu maswala hayo. Halafu, kesi inachukua muda mrefu tumesema kwamba tunaangalia, tunatafuta ule muda kesi iwe kwa muda gani hiyo imemalizika hatujaandika hiyo.

Rashid Omar amesema kwamba madaktari wasiruhusiwe kufanya kazi nje ya hospitali, hiyo tumeiandika. Ukiangalia schedule ya tano nitakusomea maanake watu wasije wakaiuliza tena. Schedule ya tano ukurasa mia mbili na arubaine na sita utakuta tumeandika pale kwamba public officers, madaktari wa Serikali ni public officers hatukutaka kuwaandika wote, public officer ni huyu ni huyu lakini tunajua mfanyikazi wa Serikali hata akifanya kazi hatafanya shuguli ambazo zitaingiliana na interest ya public officer yule. Hiyo ni wazi kwamba wafanyakazi wa Serikali kama interest yake ni kutibu wagonjwa wa uma hawezi tena kufanya kutibu wagonjwa private wazi kabisa nikasema hapo. Halafu tena kusitiliwa ikasema mfanyakazi wa Serikali haitalipwa mshahara au malipo yoyote ambapo yeye ni mfanyikazi kazi wa Serikali akifanya kazi nyingine kama ile ile. Section 2 (a) imeandika hiyo, kama wewe ni mfanyakazi wa Serikali, daktari utalipwa tena au hutapokea mshahara mwengine wa kazi ya udaktari nje na pale, imeandikwa hapo. Kwa hivyo wale madaktari itabidi waamue watabaki kule kwa Serikali au watatoka waweke clinics zao hata ukienda section 2 (b) pia inatilia mkazo hapo zaidi. Ikiwa mtu huyu atafanya kazi nje ya kazi ya Serikali basi kazi ile itakuwa ni ya kuongeza ujuzi wake kama wa-reasearch. Kwa mfano tuna dakatari anafanya kazi katika hospitali lakini kumetokea ma NGO yamekuja kuna ujuzi fulani tunataka madaktari wa upande ili aje afidie pale, sasa yule anaruhusiwa kuenda kufanya research ile miaka miwili, akirudi pale anafanya kazi ya Serikali kwa hivyo ni mwisho huo tumeshafunga hapa.

Halafu wengine wamechangia uchaguzi ujao iwe na Katiba mpya nafikiri nimeeleza kutoka mwanzo. Katiba ifundishwe shule hiyo tumekubali, Central Bank iwe decentralized hilo ni wazo tutakwenda kuliangalia hatukuliangalia. Lakini kwamba kila kiongozi anayeoa asioe katika kabila lake hatukuliandika. Kwanza yeye mwenyewe akishakuwa kiongozi tayari huwa ana bibi yake sasa ikiwa bibi yake ni wa kabila lake tuseme tumpe talaka kidogo tutakuwa tumeondoa uhuru tena wa kufanya anavyotaka. Nafirikiri sisi tusema tu ukabila hakuna na tumeshaandika hapa, hakuna ukabila katika Kenya sasa.

Kwale iwe na district tatu sasa hili ni swala ambalo ni upande wa Serikali iangalie wakati wako na Boundary Commission kuangalia, lakini sio swala letu tena. Kwa sasa kuna watu wamelalamika kwamba kuna districts nyingi ambazo zimetengenezwa tulikuwa na districts arubaine na mbili sasa zimefika ngapi? Sabini, tumeongoza ngapi, ishirini na nane. Kuna kesi ya kusema kwamba hizi ishirini na nane, John Michuki alitupeleka kotini hata sisi kusema kwamba mmeongeza districts ishirini na nane, hizi

ishirini na nane zote zilitengenezwa kisiasa, kikabila. Nafikiri kuna makabila ambayo sasa yana-districts zao, sasa tumesema sisi hatuna uwezo wa kuzifuta lakini tumesema hapo ndio mwisho hakuna tena kutengeneza za namna hiyo. Kwa hivyo zibakie hizi hizi tulizonazo sasa, sasa ukisema Kwale igawanywe iwe district tatu kidogo itabidi ingonjee, tuangalie kwanzo huu uongozi wa district utakaokuja mpya utafanya nini, ikiwa watashindwa basi watapigania wananchi wa Kenya au watutengenezee yao.

Loans kwa wakulima wadogo wadogo, kwanza haya maswala ya Bwana Jasho, maswala ya loans, maswala ya hospitali, free education, maswala yako yote majibu yake yako katika Serikali ya wilaya na Serikali ya jimbo, tumeshasema hivyo. Beach access kwa mfano ni mambo ya Serikali ya wilaya sasa kufungua hizo beaches. Halafu political parties, Bwana Rashid Juma ameeleza kuhusu political parties, amependekeza kwamba ziwe nane moja ya kila mkoa. Sisi tumesema hatutaki hivyo, tumesema ziwe zozote zinazowezekana lakini tumetoa vikwazo, tumetoa vikwazo ambazo tunakuta ni vigumu hivi vyama vitakufa vyenyewe maanake chama chako kama hakina wale viongozi wa kutoka Kenya nzima wawe katika …(inaudible) yako kama hakuna hapo tayari deregistered. Kila miezi mitatu chama kinapeleka hesabu ya pesa zake na matumizi yake, wengi hawawezi. Kila miezi mitatu kuna audit.

Uchaguzi ufanyike na Electoral Commission, uchaguzi wa kile chama uwe free and fair. Hapo hawatakubali maanake pengine chama ni cha family moja viko, vyama ni vya kabila moja hivyo haiwezekani. Hawatakubali maanake wataondolewa family ile, chama hicho tayari kinakufa. Tumesema kazi ya vyama ni kufanya civic education vieleze wananchi, vihusike katika maendeleo. Harambee wangapi waweza? Wao wangojea uchaguzi kama hivi viko tayari basi zimefufuka sasa, campaign sasa na vyote utavijua. Tumesema kama kinafanya kazi hiyo iwe de-registered tayari, automatically tunaenda. Kwa hivyo hatuna haja kusema ni vinane, ishirini, arubaine ni natural…(Inaudible) itakufa tu pole pole.

Refugees, umesema kwamba mtu anatoroka hapa halafu anarudisiwa nilikuwa nitakujibu kwamba wengine ni wakora na iko sheria ya kimataifa inayokubali kwamba ikiwa mtu ni mkora ametoroka kwao na anaweza kupatikana ashikwe arudishwe. Kwa hivyo usifanye jambo ukatoroka ukajua kwamba sasa watanifanyaje wale nimevuka nchi nyingine no, sheria ya kimataifa si ya Kenya ya kimataifa. Mtu akitoroka hapa akienda kifanya ukoroa ashikwe arudishwe na yuajibu maswali, tumeona wale wa Rwanda, wale waliofanya yale maafa kule Rwanda wametapakaa dunia mzima lakini wameokotwa moja moja unasikia yule yuko Brazil, yuko Ujerumani, wote wameletwa hapa Arusha sasa wanashtakiwa. Halafu Bwana umeeleza pia kwamba inawezekana kwamba majimbo yatatafuta misaada kutoka nchi za nje yenyewe hiyo hatukuiandika lakini tutaiandika. Hiyo nimeangalia haiko hapo

Mohammed Bakari ameuliza ni nani squatter? Squatter ni mtu ambaye amekaa pahali ambapo si pake, hiyo ndio maana ya squatter. Lakini, tumesema kwamba tunaondoka u-squatter Kenya maanake tumeandika sheria inayosema kwamba mwananchi yoyote wa Kenya ni lazima kama anataka ardhi apatiwe ardhi. Pia tukaandika kwamba ikiwezekana mikopo ya kununua ardhi pia itolewe iko hapa hivi, hatuwezi kusema kila mwananchi apatiwe heka mbili, kuna wengine tayari wana heka mia moja, kuna wengine pia pengine hawataka wanaishi kwa wazazi wao. Lakini tumesema kwamba kila mwananchi wa

Kenya anayetaka kupata ardhi apate.

**Speaker:** (Inaudible)

**Com. Mohammed Swazuri:** Bwana nimekusikiliza tafadhali nisikilize.

Halafu mzee akauliza hii yellow ribbon ni ya nini? Hii kitambara cha manyano hichi kilikuja na wale wanasheria ya mawakili, Law Society, wale mawakili wa Kenya walipoona kwamba Tume inashtakiwa sana. Ni ma-Judge na viongozi wengine na mawakili wenzao kwamba tunawaingilia uhuru wao wakasema kwamba tutafute hichi kitambara cha rangi ya yellow hicho maanake ni alama ya umoja, solidarity, kuunga mkono. Kwa hiyo anayevaa hii anaonyesha kwamba anaunga mkono Katiba mpya na kwamba anaunga mkono Tume inavyofanya kazi yake. Basi ndio maana watu wakasema anayetaka aonyeshe kwamba anaunga mkono. Nafikiri mlisikia kuna Judge alikataa kusikiliza kesi alipoona wakili mmoja amevaa hii maanake Judge anasema yeye aungi mkono.

Bwana Dzitsai, mchawi huyu limesema linawaroga watu wote hawa na likasema kwamba mambo ya land yote yafutiliwe mbali lakini sisi tumesema kwamba tumeandika sheria kwamba tutachunguza tukikuta kweli ni maonevu tufute mbali kweli, hatukatai hiyo yako imeshaandikwa hapa na nimeeleza mara nyingi. Wazee wa vitani walipwe, nafikiri sasa hayo si mambo ya Katiba tena hayo, hayo ni mambo ya sheria ambazo ziko za mikataba.

Registered land Act na Act 280 na 281 za mashamba, tumesema katika sheria moja ya mashamba tumesema kwamba kitu cha kwanza tutakachofanya katika miaka miwili ya kwanza ni kuzitengeneza sheria zote za mashamba ziwe sawa na Katiba kwa hivyo automatically hizo tayari ziko.

Bwana Councillor hapa ametoa pendekezo la kwamba mfumo wa elimu ule wa zamani, ni kweli hatukuandika. Tutaandika vile watu wanavyotaka lakini sasa kuenda ndani kusema wasifanye mtihani naona hapo kidogo tutakuwa tumeenda mbali sana. Kwa sababu ule mfumo wa zamani ulikuwa mzuri kwa sababu kila mtu alikuwa akifika kiwango fulani kazi zake zilikuwa ziko tayari. Ulikuwa ukimaliza standard four unajulikana, wewe ukishindwa kuenda standard five uwalimu wa primary tayari wewe ushapata, ukifika standard eight ukimaliza pale ulikuwa ukianguka wewe watu wote wanajua wale walioanguka wataenda polisi au wapi. Kulikuwa na KJC, form two, pia form two ukishaanguka watu walikuwa wanajua zimeshapangwa kazi zao, form four namna hiyo, form six namna hiyo basi ukifika kule kweli wewe umejipangia kazi yako. Basi maana ya mitiani ni kwamba tunaweka viwango.

Kwanza sababu moja watu wamelaumu 8-4-4 ni kwamba watu wote wamefanya viwango viwili tu either of Standard eight au form four umati mzima waishia hapo sasa viwango vimepunguzwa ndio kilio kikubwa hicho. Sisi tunataka viwango vipanuliwe viongezwe ili kila mtu ambaye anajuhudi zake zaweza kumfanya akafika kule basi afike. Kwa hivyo hii habari ya mitiani, mitiani

lazima afanye hivi vile viwango vijulikane. Upande wa kuchagua viongozi wa jimbo tukasema kwamba hawa lazima wachaguliwe watatu kwa kila constituency hilo ni swala ambalo tutalitilia maanane kwa sababu saa hizi ni kweli hawachaguliwi na wananchi.

Kwa hivyo nafikiri tutakomea hapo kwa leo, kwanza nataka kuwashukuru wale wote ambao mmefika na kutoa maoni yenu, lazima niseme kwamba hii kituo cha Diani katika wale watu ambao walitoa maoni katika Kenya tuliongoza. ***(Applause*)** Hatukupata watu wengi kama tuliopata siku ile ya kusikiliza maoni. Hapa Diani nafikiri tuliandika wale ambao walitoa maoni walikuwa mia moja na ishirini na tisa, kote Kenya tumezunguka hatukuweza kuandika watu mia moja ishirini na tisa mbali na wale ambao walikuja kusikiliza maoni ya wenzao wakitoa. Kwa hivyo mko na record kwamba nyinyi ndio watu ambao mlifuzu, Kenya nzima Diani walioshinda.

**Speaker:** Shida.

**Com. Mohammed Swazuri:** Ni kwa sababu ya shida lakini shida ni mwalimu, shida ndio inayokufundisha kufanya kufikiri. Mtu ambaye hana shida Mungu atampa uwezo wa kufikiri basi ni kidogo sana, lakini mtu ambaye ana shida ndio ambaye anaweza kufikiria nifanye nini, itawezekana vipi, haiwezekani, itawezekana. Nafikiri hadithi ya mnyama gani yule fisi ndio ambayo inatoa mafundisho vizuri sana. Fisi aliamka kwake nyumbani hakuna chakula, akasema mimi ninaenda kutafuta nikipata nitashukuru nikikosa …… Akaenda akakosa akarudi tena njaa watoto wanalia, akasema watoto wangu nyamazeni laleni lakini kesho mimi nitaenda tena, alipoamka akasema mimi naenda lakini nikipata nitakuja kula, nikikosa Mungu mwenyewe yuko akaenda akakosa.

Sasa siku ya tatu ilipofika watoto wafa sasa, shida sasa, njaa akasema leo naenda lakini either nipate au nipate maanake mnajua hiyo. Mimi leo naenda nikirudi hapa nitakuwa either nimepata au nimepata maanake sikosi leo. Kweli alipoenda alikwenda fanya lakini akarudi na nzoga. Kwa hivyo shida ikakufundisha kwamba ukitaka neno lako utafanya akili zozote lakini lazima uzipate. Sisi tumekuwa na shida lakini sasa Mungu ametujalia mambo yale tuliosema kwa wengi wetu sasa wameona matunda yake yametoka kwa hivyo lazima tujipongeze kwa hali tuliopata na kuomba Mungu kwamba sasa zile Serikali ambazo tutaziunda sasa ndio jukumu liko hapo. Hakuna haja ya kusherekea mwanzo mpaka tuhakikishe kwamba yale tunayoyataka yanatekelezwa na Katiba yenyewe imetusaidaia kuhakisha hiyo. Kama hawa watu hawafanyi kazi tunawatoa, hiyo sheria iko wazi kabisa ule uhuru mliopigania kama mtu anavyochezea sheria hivi straight away, out maanake sasa ni kwamba mmepewa na iwe hivyo, mmepata au mmepata ni hivyo hiyvo. Kwa hayo machache nashukuru sana na naomba Sheikh mmoja atusomee dua ili tuweze kuenda nyumbani kwa usalama. Nani atatusomea dua?

**Mohammed Budzo:** Sheikh Zaid.

**Prayer.**

**Sheikh Zaid Yanga:** Ndugu Waislamu, wazee, watoto na wakubwa, Asalaam Aleykum. Mimi jina langu naitwa Saidi Yanga kutoka hapa tulipo hapa. Nimefurahika sana kupata nafasi hii kumwomba Mwenyezi Mungu lakini hapa mpaa wazee tumewachiwa na wazee, …..(vernacular)

**Audience: …**(vernacular)

**Sheikh Zaidi Yanga:** …(vernacular)

**Audience: …**(vernacular)

**Sheikh Zaidi Yanga:** …(vernacular)

**Audience: …**(vernacular)

**Sheikh Zaidi Yanga:** …(vernacular)

**Audience: …**(vernacular)

**Sheikh Zaidi Yanga:** …(vernacular)

Tutatoa shukrani kama alivyosema Bwana kwamba majimbo hayo tumeshaletewa, tumeletewa au hatukuletewa?

**Audience:** Tumeletewa.

**Sheikh Zaidi Yanga:** Utumizi sasa, kuviada si kazi lakini kazi ni nini.

**Audience: …**(vernacular)

**Sheikh Zaidi Yanga:** Bwana Swazuri, lugha hiyo tuipate Bwana. Kuviada si kazi, kazi ni nini. ……(vernacular)

**Audience:** …(vernacular)

**Sheikh Zaidi Yangu:** …(vernacular). Kwa hivyo kuzidisha …….. ***(Maombi kwa Kiislamu)***. Mwenyezi Mungu utupee maelewano mazuri ….(vernacular) Naomba dua hilo kwa sababu tumeachiwa hapa wazazi wetu waliokufa nao Mwenyezi Mungu awasamehe huko aliko ……..(Kiislamu).

The meeting ended at **4.00 p.m.**

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**